-

# USAWIRI WA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI

**MOGONDO ERICKSON OKORA**

**C50/CE/34433/2016**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA SHULE YA SHERIA, SANAA NA SAYANSI ZA JAMII KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2023**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kuku chochote

Sahihi........................................Tarehe....9/11/2023....

**Mogondo Erickson Okora-C50/CE/34433/2016**

**Idara ya Kiswahili**

**Msimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyechaguliwa na Chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahih........................................Tarehe....9/11/2023....

**Dk. Beth N. Mutugu.**

Idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Kenyatta

## TABARUKU

Kwa baba yangu, marehemu Samwel Mogondo Nyoenda, kwa kazi ngumu uliyoifanya kunisomesha kwa mapenzi makubwa. Ulitamani sana niwe hivi nilivyo leo. Pumzika kwa amani. Vilevile kwa mamangu mzazi, Callen Moraa, kwa kuniombea na kunipa matumaini ya nilipokumbwa na changamoto za hapa na pale. Aidha, natabaruku kwa mke wangu, Grace Nyanchoka, kwa kunipa mazingira tulivu niliyohitaji kukamilisha utafiti huu.

## SHUKRANI

Mosi, ninachukua fursa hii kumshukuru Maulana kwa kunijalia siha njema na nguvu za kukamilisha utafiti huu. Wewe ndiwe humpa mwanadamu hekima, maarifa na vipaji vya kuusoma na kuuongoza ulimwengu.

Pili, namshukuru msimamizi wangu mkuu, Dkt.Beth Mutugu, kwa kunipa msaada, fikra, mwongozo na maarifa ya kila namna yaliyoniwezesha kufikia kiwango hiki.

Pia nawashukuru wahadhiri wangu kama vile Prof. Githinji, Dkt. Kisurulia, Dkt. Mayaka, Dkt. Sawe, Dkt. Jessee na wakufunzi wengine katika idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mlinipa elimu, mwongozo, nasaha, maarifa na matumaini ambayo yaliniwezesha kukamiliza utafiti huu.

Vilevile naishukuru aila yangu kwa kuniombea na kuniongezea ari hadi nikakamilisha utafiti wangu. Shukrani mahsusi kwa mke wangu, Grace, ndugu zangu Peter, Richard, Douglas, Alex, Evans na dadangu, Linet, kwa msaada wenu wa maombi na ushauri. Mwenyezi Mungu awabariki.

Nawatambua wasomi wenzangu, Kigen, Nyaboke, Kilel, Caro, Quenter na Eddah. Kwa pamoja tulihimizana na kushauriana kwa kipindi hiki cha masomo. Nawatakia kila la heri kwa masomo yenu.

Mwisho ni kwa rafiki na mwalimu mwenzangu, Bw.Okonji G, kwa usaidizi na mwelekeo nilipokuwa nafanya utafiti huu. Sitaweza kumtambua kila mmoja aliyenifaa katika utafiti wangu. Kwenu nyote, ninasema shukurani na Mungu awabariki.

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........ **ii**

**TABARUKU** ........ **ii**

**SHUKRANI** ........ **iv**

**UFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU** ........ **ix**

**IKISIRI** ........ **x**

**ABSTRACT** ........ **xi**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Usuli wa Mada ........ 1

1.2 Suala la Utafiti ........ 3

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 4

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 6

1.8 Misingi ya Kinadharia ........ 15

1.9.0 Mbinu za Utafiti ........ 18

1.9.1 Muundo wa Utafiti ........ 19

1.9.2 Eneo la Utafiti ........ 19

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 19

1.9.4 Ukusanyaji wa Data ........ 20

1.9.5 Uchanganuzi wa Data ........ 21

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ....................................................................21

1.9.7 Maadili ya Utafiti....................................................................................22

**SURA YA PILI..............................................................................................23**

**KUBAINISHA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII**

**KATIKA RIWAYA ZA CHOZI LA HERI (2014) NA KUFA KUZIKANA (2003) .23**

2.0 Utangulizi ....................................................................................... 23

2.1 Kuainisha Waathiriwa kwa Misingi ya Kitabaka.................................................. 23

2.1.1 Wahusika wa Tabaka la Juu ............................................................... 24

2.1.2 Wahusika Waliokuwa wa Tabaka la Chini...................................................... 30

2.2 Kuainisha Waathiriwa Kijinsia ..................................................................... 38

2.2.1 Wahusika wa Kiume........................................................................... 38

2.2.2 Wahusika wa Kike............................................................................. 46

2.3 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Elimu ..................................................... 49

2.3.1 Wahusika Waliokuwa na Elimu ya Chuoni..................................................... 49

2.3.2 Wahusika Wanafunzi wa Shule za Msingi na Upili ........................................ 54

2.4 Kuainisha Waathiriwa Kiumri ...................................................................... 58

2.4.1 Wahusika Wazee .............................................................................. 59

2.4.2 Wahusika wa Umri wa Makamo ................................................................ 61

2.4.3 Wahusika Waliokuwa Vijana .................................................................. 63

2.4.4 Wahusika Waliokuwa Watoto .................................................................. 65

2.5  Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo chaUongozi ................................................. 67

2.5.1 Viongozi wa Kisiasa........................................................................... 67

2.5.2 Viongozi wa Kidini ........................................................................... 69

2.6 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Ajira na Taaluma .................................... 69

2.7 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Ndoa........................................................ 73

2.8 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Matatizo ya Kiafya. ................................. 77

2.9 Hitimisho ............................................................................................................ 78

**SURA YA TATU ...........................................................................................................80**

**USAWIRI WA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA ZA CHOZI LA HERI (2014) NA KUFA KUZIKANA (2003)...........................................................................................................80**

3.0 Utangulizi ............................................................................................................ 80

3.1 Wahusika Waliosawiriwa Kama Watu Waliokata Tamaa ...................................... 80

3.2 Wahusika Waliosawiriwa kama Wachochezi ......................................................... 87

3.4 Wahusika Waliosawiriwa kama Wakimbizi. .......................................................... 98

3.5 Wahusika Waliosawiriwa kama Wajane na Mayatima........................................ 102

3.6 Wahusika Waliosawiriwa kama Watu wenye Madharau na Chuki ...................... 108

3. 7 Hitimisho.......................................................................................................... 109

**SURA YA NNE ...........................................................................................................110**

**KUTATHMINI MAUDHUI YALIYOKUZWA NA KUENDELEZWA KUPITIA KWA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA ZA CHOZI LA HERI (2014) NA KUFA KUZIKANA (2003) ..............110**

4.0 Utangulizi .......................................................................................................... 110

4.1 Ubaguzi wa Kimbari na Kikabila......................................................................... 110

4. 3 Nafasi ya Vijana Katika Jamii............................................................................. 116

4. 4 Nafasi ya Mwanamke Katika Jamii .................................................................... 122

4. 5 Siasa ........................................................................................................ 126

4.5. 1 Athari za Migogoro ya Kisiasa........................................................................ 127

4.6 Umaskini ........................................................................................................ 139

4.7 Elimu ............................................................................................................. 143

4.8 Hitimisho ........................................................................................................ 151

**SURA YA TANO ......................................................................................................152**

**MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........................152**

5.0 Utangulizi ....................................................................................................... 152

5.1 Muhtasari wa Utafiti........................................................................................ 152

5.2 Matokeo ya Utafiti .......................................................................................... 154

5.3 Mapendekezo ................................................................................................. 156

5.4 Mchango wa Utafiti......................................................................................... 157

5.5 Changamoto za Utafiti. .................................................................................... 158

5.6 Hitimisho ........................................................................................................ 159

**MAREJELEO ..........................................................................................................160**

**VIAMBATISHO ......................................................................................................168**

Kiambatishi A: Barua ya NACOSTI.......................................................................... 168

Kiambatishi B: Kibali cha kufanya utafiti.................................................................. 169

Kiambatishi C: Idhinisho la kufanya utafiti ............................................................... 170

# UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Mbari:** Watu wenye asili moja ambao lugha, mila na utamaduni wao kwa ujumla unafanana; kabila, ukoo.

**Nathari:** Maandishi ya moja kwa moja ambayo si ya kishairi, uandishi wa mjazo kama insha na hadithi.

**Tahakiki:** Uchunguzi wa ndani kabisa wa jambo au maandishi na maelezo yake kwa nia yakuonyesha uzito, udhaifu, yaliyomo na uhusiano wa mambo yaliyomo; uhakiki, uchambuzi.

**Kigezo:** Kanuni au sifa inayokubalika kama msingi wa kupimia au kutolea maamuzi ya jambo.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (Matei, 2014) na *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003). Riwaya hizi ziliteuliwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu kwani zinadhihirisha matukio na wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii na zilitosheleza mahitaji ya uhakiki huu. Lengo la kwanza la uhakiki huu lilikuwa kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Lengo la pili lilikuwa kuchunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya teule. Lengo la tatu lilikuwa kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Mihimili ya nadharia ya nadharia ya uhalisia ilifaa utafiti huu katika kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha matokeo kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo data ilikusanywa kupitia usomaji wa riwaya teule kisha kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa mtindo wa maelezo. Utafiti huu umegawika katika sura tano; sura ya kwanza inahusu utangulizi wa utafiti ambapo tuliangalia usuli wa mada, malengo ya utafiti, suala la utafiti, na maswali ya utafiti. Aidha sura hii ilionyesha upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu za kuchagua mada, mbinu na nadharia ya utafiti. Sura ya pili inahusu ubainishaji wa wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Kufa Kuzikana*. Sura ya tatu ilichunguza namna wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya teule. Sura ya nne inahusu kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Sura ya tano inahusu muhtasari wa tasnifu nzima, matokeo, mapendekezo, mchango wa utafiti na changamoto za utafiti.

## ABSTRACT

This research investigated how the characters of political and tribal violence have been portrayed in the novel of *Chozi la Heri* (Matei, 2014) and *Kufa Kuzikana* (Waliaula, 2003). The two novels were selected using random sampling method because they portrayed characters of political and tribal violence and contained data which was used in this research. The first objective of this research was to identify the characters of political and etnnic violence in the selected novels. The second objective was to investigate the manner in which the characters of political and tribal violence were portrayed in the selected novels. The third objective was to evaluate various themes developed and discussed through the characters of political and tribal violence in the selected novels. This research was guided by realism theory. The tenets of realism theory were used to investigate the characters of political and tribal violence as presented by the authors. The data for this research was collected in the library, analyzed and presented through descriptive method. This research contains five chapters of which chapter one involve the introduction of the research. This chapter involved the background of the study, objectives of the research, statement of the problem and research questions. It also involved the research limitations, reasons for topic selection, research theorem, literature review and research methodology. Chapter two involved identification of the characters of political and tribal violence in the novels of *Chozi la Heri* and *Kufa Kuzikana*. Chapter three investigated the manner in which the characters of political and tribal violence were portrayed in the novels of *Chozi la Heri* and *Kufa Kuzikana*. Chapter four assessed various themes developed by the characters of political and tribal violence in the selected novels. Chapter five involved the summary of the whole thesis, findings, recommendations, contributions and challenges of the research.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu umechunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003).Kwa mujibu wa Chimera na Njogu (1999), wahusika ni viumbe au watendaji katika kazi ya sanaa. Wahusika ndio mhimilimkuu wa maudhui na dhamira kwa kuwa, kupitia kwao maudhui na dhamira ya kazi ya fasihi hujitokeza. Syambo na Mazrui (1992) wanafafanua kwamba wahusika huwasilisha mienendo ya maisha ya binadamu katika jamii. Mchango wa mhusika huonyeshwa kupitia kwa matendo yake, maneno yake, malengo na mawazo yake.

Ghasia za kisiasa na kijamii ni suala ambalo limekuwa likiyakumba mataifa mengi ulimwenguni. Tafiti zilizofanywa kuhusu ghasia za kisiasa na kijamii zinaonyesha kwamba waathiriwa hukumbwa na changamoto nyingi na waathiriwa hao huweza kusawiriwa kwa namna mbalimbali. Kukosekana kwa amani katika jamii kunaweza kuzua hali ya msukosuko. Kulingana na Chumbow (1987), wakati jamii inakumbwa na misukosuko ya kisiasa na kijamii, maendeleo ya jamii huathiriwa mno. Ghasia za kisiasa na kijamii zimekuwa zikiyakumba mataifa mengi ulimwenguni. Mathalani, nchini Guatemala, kulishuhudiwa mapigano ya kisiasa na kijamii mwaka wa 1981. Machafuko hayo yalisababisha umwagikaji mwingi wa damu ambapo halaiki ya watu waliuawa, (Oettler, 2006). Wanamgambo wa kivita nchini Guatemala walitekeleza mauaji ya watu na uharibifu wa mali. Watu takribani elfu mia mbili waliuawa.

Wengine walipata ulemavu na wengine kulazimika kutafuta uhifadhi katika nchi zingine. Hali ya usalama ilirejea nchini humo mnamo mwaka wa 1986 kutokana na juhudi zilizoongozwa na jamii za kimataifa. Katika bara la Afrika, nchi nyingi zimewahi kukumbwa na ghasia za kisiasa na kikabila. Mathalani, nchi ya Rwanda ilikumbwa na mauaji ya kimbari yaliyosababishwa na tofauti za kikabila mnamo mwaka wa 1994. Makabiliano kati ya wanamgambo wa Wahutu na Watutsi yalisababisha mauaji ya halaiki ya watu wasiopungua milioni moja (Ogechi, 2011) huku wengine wakitorokea mataifa jirani. Aidha, kulikuwa na uharibifu mkubwa wa mali na kukwamishwa kwa maendeleo nchini humo (Magnarella, 2001). Ekuam (2006) anasema kwamba, mizozo hii ya kisiasa na kijamii huathiri watu wasiojiweza katika jamii. Wanaoathirika zaidi ni wakongwe, watoto, wanawake na hata wagonjwa wasio na uwezo. Makundi haya ya watu huathirika kutokana na kupungukiwa kwa huduma muhimu za kimsingi huku wengine wakiuawa, kubakwa na kufurushwa kutoka makazi yao. Nchi ya Kenya ilikumbwa na ghasia za kisiasa na kikabila mwaka wa 2007/2008. Waki na Krieglar (2009), wanaeleza kuwa takribani watu zaidi ya elfu moja waliuawa katika ghasia hizo huku wengine wakibaki wakimbizi.

Wahusika hutekeleza majukumu muhimu katika kutosheleza mahitaji ya kazi ya mwandishi katika utanzu wa fasihi. Wahusika ni vyumbe wananaoumbwa kisanii na msanii ili kufanikisha kazi ya sanaa. Kupitia kwa wahusika, fanani hupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Dhana 'mhusika na uhusika' imefasiliwa na wataalamu mbalimbali ili kuonyesha maana yake na dhima ya mhusika katika kazi ya sanaa. Ndung'o (1991), anafafanua kwamba mhusika ni kiumbe aliyefinyangwa na fanani kiufundi ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Mtunzi anaweza kutumia wahusika binadamu, wanyama, miungu au vitu katika

kazi ya sanaa katika huwasilisha ujumbe wake katika jamii. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), wahusika hutumika kuwasilisha dhamira na maudhui katika utanzu wa fasihi kwa hadhira. Wamitila (2012), anafasili kuwa mhusika ni mtendaji katika kazi ya sanaa hata kama anaweza kukosa baadhi ya hulka sawia na za binadamu wa kawaida. Mhusika ni kiumbe aliyepewa jukumu la kuwakilisha tabia au mawazo ya binadamu kupitia kwa kazi ya sanaa (Senkoro, 2011). Utafiti huu ulichunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* (2003) na *Chozi la Heri* (2014).

## 1.2 Suala la Utafiti

Wataalamu mbalimbali wamechunguza usawiri wa wahusika katika riwaya za Kiswahili. Miongoni mwa waliotafiti usawiri wa wahusika katika riwaya za Kiswahili ni pamoja na Vuai (2018), Ndung'o (1985), Wanjiku (2018), Muindi (1990), Maobe (2011), Fakih (2017) miongoni mwa wataalamu wengine. Tafiti hizi zilihusu usawiri wa wahusika katika riwaya kwa misingi na vigezo mbalimbali. Hata hivyo hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za Kiswahili. Kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu suala hili ikizingatiwa kuwa vita vya aina hii vimekuwa vikizuka mara kwa mara katika mataifa yanayoendelea. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Riwaya zilizochunguzwa katika utafiti huu ni *Kufa Kuzikana* (Waliaula, 2003) na *Chozi la Heri* (Matei,2013). Utafiti huu uliongozwa na mihimili teule ya nadharia ya uhalisia.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

i) Kubainisha waathirika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*.

ii) Kuchunguza namna waathirika wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*.

iii) Kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathirika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i) Ni waathiriwa gani wa ghasia za kisiasa na kijamii wanaojitokeza katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*?

ii) Waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii wamesawiriwa vipi katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*?

iii) Ni maudhui yapi yamekuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri*?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu yamekuwa yakikumbwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Mada hii ilifaa sana hasa nyakati hizi ambapo mataifa mengi ulimwenguni ikiwemo nchi ya Kenya yamewahi kukumbwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Imedhihirika kwamba vita huyakumba mataifa yanayoendelea punde tu baada ya uchaguzi. Nchi ya Kenya ilikumbwa na tatizo la ghasia baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007/2008 ambapo

watu wengi waliuawa huku wengine wakipata changamoto nyingi ikiwemo ukimbizi. Utafiti huu wa kifasihi umetuwezesha kutoa mchango wetu mwafaka katika kusawiri waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

Riwaya za kisasa za Kiswahili zimefafanua kwa mapana maswala mbalimbali yanayoibuka katika jamii. Wahusika wanaojengwa katika riwaya za kisasa za Kiswahili wanazidi kuwa na matakwa pamoja na changamano nyingi ambazo haziwezi kuangaziwa kwa kutumia njia sahili pekee. Hali kadhalika, wahusika wa kisasa wanamsawiri binadamu halisi zaidi kuliko wale waliotumika katika riwaya za hapo awali. Hivyo basi, ili kuwaelewa wahusika zaidi wa fasihi na kuelewa ploti ya riwaya za kisasa wahusika wanaokumbwa na ghasia za kisiasa na kijamii wanapaswa kuchunguzwa.

Mbali na kutafiti kuhusu wahusika wa riwaya za Kiswahili, hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kuhusu usawiri wa wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii. Usomaji wa kazi zinazoshughulikia ghasia za kisiasa na kijamii unaweza kuwafaidi wanachuo wanaonuia kuendeleza tafiti zao kuhusu masuala yanayohusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za Kiswahili. Utafiti huu utawapa maarifa zaidi ya kufanya tafiti kuhusu masuala halisi yanayoathiri wanadamu. Wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii wanapochunguzwa, ploti ya riwaya inaendelea kujengeka kwa mapana. Uhakiki huu utakuwa wa kufaa katika kuendeleza ploti na kuikuza zaidi ili watunzi wa baadaye waweze kushughulikia wahusika wanaosawiri masuala mengine yanayoathiri jamii.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Waandishi wengi wameandika riwaya za Kiswahili kuhusu masuala mbalimbali. Katika kufanya utafiti wa awali ilibainika kuwa riwaya teule za waandishi Waliaula na Matei ambazo ni *Kufa Kuzikana* (2003) na *Chozi la Heri* (2014) zilifaa utafiti huu.Waliaula ameandika kazi kama vile *Siku Njema* (1996), *Kidagaa Kimemwozea* (2012), *Ndoto ya Amerika (2001)*, *Ndoto ya Almasi(2012)*, *Nasikia Sauti ya Mama (2014)*, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (Mhariri, 2013), *Kiti Cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007), *Innocene Long Lost* (2005), *Waja Leo* (2012) na *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* (2012).

Matei ameandika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014). Kwa sababu utafiti wetu ulihusu usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii, tuliteua riwaya za *Chozi la Heri* (2014) ya Matei na *Kufa Kuzikana* (2003) ya Waliaula.Tulifanya uteuzi wa riwaya hizi baada ya kusoma kazi zote za wandishi hawa na riwaya za waandishi wengine. Riwaya hizi ni maalumu kwa sababu zilitupatia data ya kutosha iliyotumika katika utafiti wetu na kufanikisha madhumuni ya utafiti. Data iliyohitajika ni kuhusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii. Riwaya hizi zilidhihirisha data hii kwa maneno, sentensi, vifungu, semi za wahusika walioathirika na ghasia na vilevile wahusika wengine ambao hawakuathirika na ghasia za kisiasa na kijamii.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mlacha (1985), alihakiki wahusika waliotumiwa na watunzi katika riwaya teule za Kiswahili nchini Tanzania kuanzia mwaka wa1970 hadi1982. Utafiti wake ulibaini kuwa wahusika hupewa lugha na wasanii inayowasaidia kueleza mambo anayokusudia

mwandishi. Mhakiki huyu ameonyesha kwamba mhusika anatumia taswirazinazojengwa mawazoni ili kuathiri hadhira. Tofauti iliyoko kati ya utafiti wetu na wa Mlacha ni kuwayeye anachambua wahusika wa riwaya kwa jumla ilhali sisi tulijikita katika kuchunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwetu kwa sababu ulituongezea maarifa yaliyotusaidia katika kuchanganua waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Tulifaidika kwa kupata mbinu za kudondoa data za wahusika, kuchambua na kuwawasilisha matokeo ya utafiti wetu.

Muindi (1990), amechunguza jinsi suala la ukahaba lilivyojitokeza katika baadhi ya wahusika wa riwaya teule za Said A. Mohamed. Uhakiki huu ulichunguza sababu zinazowachochea baadhi ya watu kujihusisha na ukahaba. Aidha, alichunguza hisia za jamii kuhusu suala la ukahaba na kuonyesha namna mwandishi alivyojaribu kuwaondoa wahusika wake kutoka maisha ya ukahaba. Mhakiki alitumia nadharia ya Utekelezi na ile ya Kisaikolojia kuendeleza utafiti huu. Utafiti huu ulikuwa muhimu kwetu kwani ulituongezea maarifa kuhusu namna ya kusawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Mbinu alizotumia kusampulisha wahusika wake zilituwezesha pia kuwateua wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika utafiti wetu.

Mavisi (2011), ametafiti kuhusu namna wahusika wa kike walivyosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili. Utafiti huu ulisawiri makundi tofauti ya wahusika wa jinsia ya kike. Katika kazi hii, mtafiti alitathmini kumbo la wanawake wa kisasa na lile la wanawake wa zamani na kubainisha tofauti zao katika kupambana na hali zinazowakumba. Nadharia ya

ufemisti wa Kiafrika iliongoza uhakiki huu. Utafiti huu ulichanganuliwa na kuwasilishwa kwa mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yalitufaa katika utafiti kwani yalitupa vipengele muhimu ambavyo hutumika katika kuwasawiri wahusika katika riwaya. Utafiti wa Mavisi ulihusu wahusika wanawake katika riwaya teule za kiswahili ilhali wetu unahusu usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule.

Maigizo kama mbinu ya maudhui imehakikiwa na Ochieng (2011) ambapo kazi teule za Waliaula zilitumika. Mtafiti alibaini kuwa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Ndoto ya Amerika* zina sifa za kitamthilia na hivyo matendo ya wahusika yanaigizika. Utafiti huu umeonyesha kuwa Waliaula amewaumba wahusika wake kufanana na binadamu wa kawaida na wanapowasiliana, riwaya zake zinawasilisha maudhui kwa mtindo wa uigizaji. Mtafiti ametumia nadharia ya uhalisia na uigizaji kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Uhakiki huu ulitufaa kwa sababu Ochieng ametathmini masuala kama vile ukabila, uhalifu, ukatili na ubinafsi, masuala ambayo pia yaliwaathiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kikabila.Uhakiki huu umetofautiana na tulioufanya ambapo wetuulisawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za kiswahili.

Gahnstrom (2012) akihakiki siasa nchini Tanzania, anaeleza kuwa, ukabila, dini na mirengo ya kisiasa ndivyo huchangia ghasia za kisiasa na baguzi za kimbari katika mataifa yanayoendelea. Utafiti wake ulitumia mbinu ya uchanganuzi maktabani na utafiti nyanjani kuchunguza hali ya ukabila, dini na siasa nchini Tanzania kutumia kigezo cha uchaguzi wa eneo la Mwanza mnamo mwaka wa 2010. Ameonyesha kwamba, ukabila, dini na siasa ziliathiri matokeo ya uchaguzi huo. Utafiti wao ni muhimu kwetu kwani baadhi ya masuala

yaliyojitokeza katika utafiti wao kama vile ukabila na mirengo ya kisiasa yamejitokeza vilevile katika utafiti wetu. Mtafiti alitambua kuwa matukio ya vurugu na vita vya miaka tisini na tofauti za kisiasa na kidini vilisababishwa na matatizo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania miaka ya themanini na tisini. Aidha ilibainika kuwa kudidimia kwa dhana ya utaifa nchini Tanzania kuliwafanya wanasiasa kuchochea maeneo fulani ili kupata uungwaji mkono. Pia, ameonyesha namna nchi ya Tanzania ilivyolikabili suala la ukabila na ghasia za kisiasa. Uhakiki huu ni tofauti na wetu kwani sisi tulihakiki usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

Mosha (2013), amesawiri mhusika padre katika riwaya teule za Kezilahabi. Ameonyesha kuwa mhusika padri anatekeleza majukumu mbalimbali kupitia kwa uhusika wake. Aidha uchunguzi huu umebaini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na mhusika padri. Kazi hii ya kitaalamu ilihakikiwa kwa kutumia mwongozo wa Uhalisia wa Kimarks. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwetu kwa sababu ulitupa maarifa yaliyotusaidia kusawiri wahusika katika utanzu wa riwaya za Kiswahili. Maarifa hayo yalitusaidia kutathmini maudhui yaliyojengwa na kuendelezwa na wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule.

Matara (2014) katika tasnifu yake, amechunguza namna muziki ulivyotumiwa kuendeleza amani na maelewano katika nchi ya Kenya kuanzia mwaka wa 2008 hadi 2012. Mtafiti amebaini kwamba, wanamuziki walitumia lugha mahsusi katika muziki kuhimiza amani na maridhiano ili wakenya wajihepushe na hali ya misukosuko kama iliyoshuhudiwa nchini Kenya mwaka wa 2007/2008. Uhakiki wake uliongozwa na mihimili ya nadharia ya

majukumu ya lugha na kuwasilishwa kwa mkabala wa kimaelezo. Uchanganuzi huu ulikuwa muhimu kwetu kwa sababu baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika utafiti wao kama vile vurugu za kisiasa, amani na maridhiano, ubaguzi wa kimbari yamejitokeza katika utafiti wetu. Tofauti na wao, sisi tulijikita katika kusawiri waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Aidha tulitathmini maudhui ambayo waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuza na kuendeleza katika riwaya teule.

Ghasia za uchaguzi nchini Kenya kuanzia mwaka wa 1992 hadi 2013 zimehakikiwa na Yego (2015). Uchunguzi wake umebaini jinsi ukabila ulivyochangia ghasia za baada ya uchaguzi kuanzia mwaka wa 1992 hadi 2013 nchini Kenya. Ameonyesha kwamba, vyama vya kisiasa huundwa kwa misingi ya kikabila. Mtafiti ameonyesha kuwa, kila baada ya uchaguzi vyama vya kisiasa hupinga matokeo ya uchaguzi kwa kutoamini matokeo ya uchaguzi na kutuhumu udanganyifu na wizi wa kura katika uchaguzi. Kutokubali matokeo ya uchaguzi mkuu huzua ghasia za kisiasa na ubaguzi wa kikabila ambapo kilele cha migogoro hiyo ilikuwa ghasia zilizoshuhudiwa nchini Kenya mwaka wa 2007/2008. Utafiti huu ulikuwa muhimu kwetu kwa sababu ulituchorea taswira halisi ya mambo yanayotokea katika ghasia za kisiasa na kikabila baada ya uchaguzi na kutupa maarifa yaliyotuwezesha kutekeleza utafiti wetu. Tofauti na utafiti wao, tumechunguza usawiri wa wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

Vurugu za baada ya uchaguzi nchini Kenya mwaka wa 2007 zimetafitiwa na Hamdi (2015). Katika utafiti wake, masuala ya ndani yaliyozunguka vurugu za kisiasa zilizoshuhudiwa mwaka wa 2007 yamebainishwa. Anaeleza kuwa, sio udanganyifu katika

upigaji kura tu ulichochea ghasia, bali kuna masuala mengine nyeti yaliyochangia na kuchochea ghasia za baada ya uchaguzi. Amebaini masuala kama vile ugavi usio sawa wa raslimali, ukosefu wa uwakilishi sawa na katiba ambayo haijafanyiwa marekebisho kama baadhi ya vichocheo vya ghasia za kisiasa na kijamii. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwani ulitupa maarifa yaliyotumika katika kuhakiki taswira za wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za *Chozi la Heri* na *Kufa Kuzikana*. Utafiti huu umetofautiana na wetu kwani sisi tumechunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za kiswahili.

Faki (2017), amechunguza uwakilishi wa mhusika wa kike katika utanzu wa riwaya za Kiswahili. Mhakiki huyu amebaini jinsi ambavyo mwanamke amebadilika kwa kipindi cha miongo mitatu katika riwaya za Kiswahili. Ili kufanikisha malengo ya uhakiki wake, alitumia riwaya teule za miaka ya sabini na riwaya teule za miaka ya tisini. Mhakiki huyu alilinganisha kufanana na kutofautiana kwa mhusika mwanamke kwa kutumia mwongozo wa ufeministi wa Kiafrika na ule wa nadharia ya fasihi linganishi.Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani yeye amesawiri mhusika mwanamke ilhali sisi tulisawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Utafiti huu ulitufaidi kwa kutupa vipengele muhimu tulivyotumia katika mada yetu ya usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

Munyasya (2017) amechunguza majukumu na changamoto zinazowakumba wahusika vijana katika jamii kwa kutumia riwaya teule za Kiswahili. Utafiti huu umeonyeshamatatizo yanayowakabili vijana katika harakati zao za kuleta mabadiliko

katika jamii. Baadhi ya changamoto alizobaini ni kama chuki na vitina, utengano wa vijana na ukosefu wa ari ya kuleta mabadiliko. Utafiti huu ulikuwa na manufaa kwetu kwa sababu uliangazia baadhi ya maudhui kama vile ukabila, chuki na vitina miongoni mwa masuala mengine. Utafiti wetu ulitofautiana  na wao kwani sisi tulisawiri waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Wao wametumia nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii kuchanganua na kuwasilisha utafiti huu kwa njia ya maelezo ilhali sisi tulitumia nadharia ya uhalisia katika uhakiki wetu.

Kwa upande wake, Aming'a (2018), amechunguza usawiri wa wahusika vijana katika riwaya za*Nyota ya Rehema*, *Kufa Kuzikana*  na *Kidagaa kimemwozea*. Ametambua kwamba wahusika vijana kama mawakala muhimu wa kuleta mabadiliko ambayo yatafaidi jamii. Pamoja na hayo, ameonyesha kuwa vijana wanakumbwa na matatizo mengi ambayo ni sharti yachukuliwe hatua zinazofaa ili kuokoa kizazi hiki muhimu cha vijana. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu unaangazia baadhi ya masuala ambayo yamejitokeza katika uhakiki wetu kama vile dhuluma za kisiasa na ukosefu wa haki kwa vijana.Aidha, utafiti huu ulituongezea maarifa na mbinu ambazo zilitufaa katika kutafiti kuhusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii.

Usawiri wa mhusika mwanamke umechunguzwa na Hemed, (2018) katika riwaya ya *Mfadhili*. Ametambua taswira mbalimbali za mhusika wa jinsia ya kike katika riwaya. Aidha mtafiti amefafanua sifa mbalimbali za mhusika mwanamke zinazomfanya asawiriwe kama alivyosawiriwa.Utafiti wake ulitumia mbinu ya utafiti maktabani na kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika

iliongoza utafiti huu. Uhakiki huu ulikuwa wa manufaa kwetu kwani ulitusaidia katika kudhihirisha usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii na changamoto walizokabiliana nazo. Utafiti huu ulituongezea maarifa ya kutafiti pamoja na kuwa nyongeza muhimu ya marejeleo ya kitaaluma kwa utafiti wetu.

Mbinu za kusawiri wahusika katika utanzu wa riwaya teule za Kiswahili umetathminiwa na Ali (2018). Mhakiki huyu amebaini mbinu mbalimbali zinazotumiwa kuwasawiri wahusika katika riwaya. Ili kufanikisha kazi yake, mhakiki alitumia mihimili ya nadharia za fasihi linganishi na mwitiko wa msomaji kuendeleza utafiti wake. Uchanganuzi huu ulifanywa maktabani na kuwasilishwa kwa mkabala wa kimaelezo. Uchunguzi huu ulituongezea tajriba na maarifa yaliyotusaidia katika utafiti wetu uliohusu usawiri wa wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule.

Wanjiku (2018), ameshughulikia mhusika mwanamume kwa kuonyesha jinsi alivyosawiriwa kama mhusika aliyekengeuka kimtazamo katika riwaya teule za Kiswahili. Katika uhakiki huu, mtafiti amebaini  kwamba mhusika mwanamume amebadilika katika riwaya za kisasa akilinganishwa na riwaya za awali za Kiswahili. Ameonyesha kuwa mhusika mwanamume aliyekuwa mtafuta riziki, mtunga sheria, mtafuta suluhu na mfanya kazi amekengeuka katika riwaya za kisasa. Anaeleza kwamba mabadiliko haya yamesababishwa na mabadiliko ya kimazingira, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ili kufanikisha utafiti wake, mhakiki alitumia nadharia ya uhalisia kuchanganua data yake. Utafiti huu uliwasilishwa kwa mbinu ya maelezo. Uhakiki huu ulitufaa kwa sababu amesawiri wahusika katika riwaya za Kiswahili kazi ambayo pia tuliishughulikia.  Pia,

alitupa mbinu na maarifa muhimu yaliyotusaidia katika kusawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

Simiyu, (2019), amechunguza siasa za vurugu na mapendeleo katika tamthilia ya *Pango* na riwaya ya *Kufa Kuzikana*. Alionyesha namna viongozi hupigania mamlaka ili kujinufaisha na uongozi. Manufaa haya ni kama vile mamlaka na utawala, kusimamia raslimali zote za serikali, kujigawia raslimali pamoja na manufaa mengine. Makala haya yalikuwa muhimu kwetu kwa sababu yalibaini baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika utafiti wetu. Makala haya yanatofautiana na uhakiki wetu ambapo tulichunguza waathiriwa wa ghasia za kijamii na kisiasa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Chozi la Heri* huku wao wakichunguza siasa za vurugu na mapendeleo katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* na tamthilia ya *Pango*.

Tafiti na tahakiki hizi zimeshughulikia usawiri na uchunguzi wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili kwa vigezo mbalimbali. Baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa ni kama usawiri wa wahusika watoto, usawiri wa mhusika padri, usawiri wa wahusika vijana na usawiri wa wahusika wanasiasa na wahusika makahaba. Aidha usawiri wa wahusika wanawake na jinsia ya kike umesawiriwa pamoja na usawiri wa wahusika wanaume. Kuna pia tahakiki ambazo zimechunguza ghasia za uchaguzi na suala la ukabila nchini Kenya na Tanzania. Hata hivyo, hamna uchunguzi wowote uliofanywa kuhusu usawiri wa wahusika waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Kufa Kuzikana*. Kwa misingi hii basi, utafiti wetu ulijaza pengo hilo kwa kuchunguza

waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)*na *Kufa Kuzikana (2003).*

## 1.8 Misingi ya Kinadharia

Uhakiki huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa na wasomi na waandishi wa Kifaransa. Wanauhalisia hawa ni pamoja na Flaubert (1880), Stendhal (1839) na Balzac (1850). George Eliot (1859) aliongoza maenezi ya nadharia hii nchini Uingereza huku William Howells (1891) akiisambaza nchini Marekani. Kulizuka baadaye wanauhalisia wengine ambao waliendeleza mafunzo ya nadharia hii. Wataalam hawa ni pamoja na Gorky Maxim (1934), Mann Thomas (1939), Rolland Romain (1914) na Lukacs George (1938). Baadaye kulitokea aina tofauti za uhalisia. Mathalani, uhalisia wa kijamaa, uhalisia hakiki na uhalisia wa kibepari. Aina hizi za uhalisia zilijishughulisha na majukumu tofauti. Mathalani, katika miaka ya 1930, uhalisia wa kijamaa ulishughulikia michoro iliyosawiri ubaguzi wa rangi na mbaguano wa kijamii nchini Marekani. Wanauhalisia wachoraji walioitumia nadharia hii walikinzana kimaoni na Wamaksi.

Uhakiki huu uliongozwa na mihimili iliyopendekezwa na George Lukacs (1963). Mwanauhalisia huyu anadai kwamba sababu za kuzuka kwa uhalisia ni wakati binadamu alipogundua kuwa matatizo yanayomkumba husababishwa na binadamu mwenzake. Nadharia hii ilinuiwa kutambua uhusiano wa watu na jamii na nguvu za jamii, kisiasa na kitamaduni kwa watu na mazingira yao. Hegel (1830), anafafanua kuwa wahusika wa kazi za kihalisia wanaumbwa na kuwasilishwa kutegemea mazingira waliyomo. Asili ya Uhalisia ni Ulaya kulipozuka uvumbuzi wa viwanda. Uvumbuzi huu ulileta mabadiliko

makubwa katika jamii ya wakati huo. Kulikuwa na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyoletwa na uvumbuzi mpya wa sayansi. Uvumbuzi wa teknolojia na viwanda, uliibua miji na majiji ambapo maisha ya watu yaliimarika. Aidha, kulitokea na matatizo kama vile umaskini na utabaka miongoni mwa wanajamii. Kufuatia mabadiliko haya, wasanii wengi wakanuia kutunga kazi za kisanaa wakichochewa na hali halisi waliyokumbana nayo na kususia kutunga kazi za kijonzi ambazo hazikuwasilisha hali halisi ya maisha.

Mwanauhalisia humthamini mno mtunzi wa kazi ya sanaa anavyojitahidi kuwasilisha ukweli wa maisha ya jamii. Wahakiki wa uhalisia wanafafanua kuwa mtunzi wa kazi ya sanaa anastahili kuchora taswira ya wanadamu kwa kutoa ukweli halisi bila kutia chumvi wala kuitweza kazi yao. Kigezo muhimu katika uhalisia ni kusisitiza kwamba kazi yoyote ya sanaa sharti iwakilishe maisha kutegemea ukweli unaopatikana katika jamii. Mandhari, maudhui na wahusika katika kazi ya sanaa za kihalisia wawakilishe hali yakinifu ya binadamu kutegemea mazingira waliyomo. George Lukacs (1963) alipendekeza mihimili ya uhalisia ifuatayo:

(i) Sanaa lazima iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku

(ii) Sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake.

(iii) Mtunzi anapaswa afanye utafiti juu ya yale anayotaka kuandika ili aweze kuandika ukweli unaokubalika kifasihi.

(iv) Mtunzi anapoandika azingatie mambo madogo madogo ambayo hujenga wazo kubwa.

(v) Wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii.

(vi) Mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake.

(vii) Fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe.

(viii) Mwandishi adumishe uhalisia katika ubunifu wake katika kazi ya sanaa.

Utafiti huu uliongozwa na mihimili mitano ya George Lucas (1963) ambayo ni pamoja na wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake. Mhimili mwingine tuliotumia ni ule wa sanaa kuwa ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku. Aidha tulitumia mhimili unaosema kuwa sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake. Mhimili wa mwisho uliotumika ni ule unaodai kuwa fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe.

Mhimili unaoeleza kuwa mtunzi atumie mandhari asili na kuyaendeleza katika hali ya ukawaida wake, ulitumika kutathmini kama mandhari yaliyotumiwa na watunzi wa riwaya teule yanalingana na maelezo na majukumu ya wahusika katika riwaya husika. Mhimili huu ulisaidia kubaini wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule na pia kutathmini maudhui waliyokuza na kuyaendeleza waathiriwa.

Mhimili wa mtunzi kuwasawiri wahusika jinsi walivyo kwa jamii, ulitumika kuchunguza kama wahusika wamepewa hulka za mwanadamu wa kawaida kutegemea na jinsi watunzi

walikuwa wamewachora. Mhimili huu ulitumika kuwabaini na kuwasawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule.

Mhimili unaodai kuwa sanaa lazima iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku ulitumika kuonyesha hali zote za maisha ya wahusika na kuonyesha jinsi wanavyoonekana na wala sio vile wanavyofikiriwa kuwa na wanasanii. Mhimili huu ulisaidia katika kuchunguza mchango wa wahusika katika kukuza maudhui mbalimbali katika riwaya teule.

Mhimili mwingine uliotumika ni ule unaodai kuwa kazi ya sanaa inapaswa kumulika maisha halisi jinsi yalivyo katika mandhari yake. Nguzo hii ilitumika kusawiri wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii  na kutathmini maudhui yaliyokuzwana waathiriwa hawa. Mhimili  unaofafanua kuwa sanaa inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na wala sio vile msanii anataka yawe, ulitumika kubaini ikiwa wahusika waliotumika ni wa kweli au ni wa kubuni tu. Aidha mhimili huu ulitusaidia kutathmini kama maudhui yaliyoendelezwa na wahusika ni maudhui yanayoibuka katika jamii halisi.

**1.9.0 Mbinu za Utafiti**

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2008), kuna mbinu mbili kuu za utafiti. Mbinu hizi ni mbinu ya kithamano na mbinu ya kiwingi-idadi. Utafiti wetu ulitumia mbinu ya kithamano kwa sababu ni utafiti wa kifasihi ambapo data ilikusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Kasomo (2006), anasema kuwa katika mbinu ya Kithamano, data haiwezi kuandikwa kiidadi ila maelezo ndiyo huzingatiwa.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Kothari (1990), uchanganuzi matini ni mbinu ambayo mhakiki hutoa maelezo kwa data ya utafiti kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kusoma riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003) kisha maneno, vifungu na aya zinazotaja au kueleza kuhusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kikabila zikadondelewa. Aidha, data nyingine ilitokana na mazungumzo baina ya wahusika walioathirika na ghasia, matendo yao na wanayoyasema na wahusika wengine. Data hii ilikusanywa, ikachanganuliwa na kuwasilishwa kwa muundo wa maelezo.

### 1.9.2 Eneo la Utafiti

Enon (1998) anafafanua kwamba mahali pa utafiti ni sehemu ambapo utafiti unatarajiwa kufanywa au mahali ambapo utafanywa. Utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo data kuhusu waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kikabila ilidondolewa kutoka riwaya za *Chozi la Heri* na *Kufa Kuzikana*. Data hii ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya uhakiki huu iliteuliwa kwa mbinu ya usampulishaji kinasibu. Walibora na Matei wameandika vitabu kadhaa kama vile tamthilia, riwaya na hadithi fupi. Walibora ametunga kazi kama vile *Siku Njema* (1996), *Kufa Kuzikana* (2003), *Ndoto ya Alimasi* (2012), *Ndoto ya Amerika* (2001), *Nasikia Sauti ya Mama* (2014), *Kidagaa Kimemwozea* (2012), *Damu Nyeusi* (2013), *Kiti cha Moyoni* (2007), *Innocence Long Lost* (2005), *Waja Leo* (2012), *Chapu Chapu* (2012), *Mtu wa Mvua* (2012), *Hazina Bora* (2012) na *Narrating the Prison experience* (2013). Matei ameandika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), *Uteuzi wa Chale* (2022) na *Mji wa Matarajio* (2022).

Tulifanya utafiti wa awali kwa kusoma kazi za waandishi wengine wa kazi za Kiswahili zinazohusiana na mada ya utafiti huu na kazi zote za Ken Walibora na Assumpta Matei. Tukiongozwa na malengo ya utafiti huu; kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii, kuchunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya teule na kutathmini maudhui yaliyokuzwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule, tuliteua riwaya za Waliaula na Matei. Riwaya tulizoteua ni *Chozi la Heri* (2014) ya Matei na *Kufa Kuzikana* (2003) ya Walibora. Riwaya hizi zilikuwa na data ya kutosha ambayo ilihusu waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Kukusanya data ni kufanya utafiti wa awali ili kumwezesha mtafiti kupata taarifa au takwimu zitakazotumika katika utafiti, (Kothari, 2004). Data yetu ilikusanywa kwa usomaji wa kina wa riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Tulisoma riwaya hizi na kutenga maneno na vifungu vinavyohusu usawiri wa wahusika wa ghasia za kisiasa na kikabila na yanayoafikiana na malengo na mihimili ya nadharia ya uhalisia.Tulikusanya maelezo kuhusu kile wanachosema waathiriwa wa ghasia za kisiasa na yale yanayosemwa na wahusika wengine kuhusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii. Aidha, tulikusanya maelezo yote ya waandishi kuhusu wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii. Tulikusanya data ambayo ilituwezesha kuwabaini waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Aidha tuliteua data ambayo ilitusaidia kuchunguza namna wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika

riwaya teule. Vilevile tulitenga data ambayo ilitusaidia kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na waathiriwa katika riwaya teule za Kiswahili.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Kuchanganua data ni kupanga data kwa njia mahsusi ili iweze kutumika katika kuwasilisha matokeo ya utafiti, (Kothari, 2004). Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kuainisha na kutenga data iliyohusu waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003).* Katika kuchanganua data, tulitenga na kuainisha data kuhusu kubaini waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Aidha tulitenga na kuainisha data kuhusu usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Vilevile tulitenga na kuainisha data iliyohusu namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyokuza na kuendeleza maudhui katika riwaya teule za Kiswahili. Data hii ilikusanywa kwa kuinakili katika shajara maalum kulingana na malengo na nguzo za nadharia ya Uhalisia na kisha ikachanganuliwa kwa njia ya maelezo.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya uhakiki huu yaliwasilishwa kupitia kwa mtindo wa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa katika sura ya pili, sura ya tatu na sura ya nne. Ili kuwasilisha matokeo haya, tuliongozwa na nadharia ya uhalisia na malengo ya utafiti. Sura ya pili ilihusu kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Tuliwatambua wahusika hawa kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile umri, jinsia, kiwango cha elimu, utabaka, wanandoa miongoni mwa vigezo vingine ambavyo vimejadiliwa katika sura ya pili.

Sura ya tatu iliwasilisha matokeo yaliyohusu namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili. Wahusika hawa walisawiriwa kwa njia mbalimbali kama vile wahusika waliotamauka, wachochezi, wakimbizi, wajane miongoni mwa taswira zingine. Matokeo ya sura ya nne yalitatmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili. Maudhui yaliyotambuliwa ni pamoja na nafasi ya vijana katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, siasa, elimu miongoni mwa maudhui mengine.

### 1.9.7 Maadili ya Utafiti

Mligo (2012), anaeleza kwamba kukopa matini ya mtaalamu mwingine bila kumtambua kwa njia yoyote ni kinyume na maadili ya uandishi.Utafiti huu ulizingatia maadili ya utafiti ili kuwasilisha matokeo ya kweli na ya uhakika. Mosi, tumewatambua wataalamu wengine ambao kazi zao zilitufaidi kwa njia moja au nyingine kwa kuzinukuu  na vilevile kuwatambua katika sehemu ya marejeleo. Aidha, tuliomba vibali vyote vilivyohitajika katika hatua mbalimbali kikiwemo kibali kutoka kwa tume ya  NACOSTI.

# SURA YA PILI

## KUBAINISHA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LA HERI* (2014) NA *KUFA KUZIKANA* (2003)

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu kuwabainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003)*. Katika kuwabaini wahusika, tuliongozwa na lengo la kwanza la utafiti ambalo lilikuwa kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Woloch (2003) anasema kuwa, aina zote za wahusika katika fasihi ni wa maana. Hata hivyo, kuna wahusika wasaidizi ambao kazi zao huingiliana katika tungo za fasihi na tunapowachanganua wachache wanawakilisha wengine.

Riwaya za *Chozi la Heri* na *Kufa Kuzikana* zina wahusika wengi lakini tulishughulikia wale walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), wahusika tulioshughulikia ni pamoja na Akida Sululu, Tim Mapisi, Tamari Mapisi, Tom Mangala, Jenelle Tom, Johnstone Mabende, Mzee Sululu, Mwalimu Alex, Zablon Mapisi, Tito Tembo na Mzee Uledi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), tuliwatambua wahusika Kama Ridhaa, Mwangeka, Lily Nyamvula, Lunga Kangata, Umulkheri, Kairu, Mwanaheri, Subira, Dickson, Terry, Anatila na Kaizari.

### 2.1 Kuainisha Waathiriwa kwa Misingi ya Kitabaka

Kwa mujibu wa Karl Marx (1883), jamii ina matabaka mawili makuu; tabaka la juu ambalo humiliki nyenzo za uzalishaji mali na tabaka la chini ambalo hujumuisha

wafanyakazi. Wanachomiliki wafanyakazi ni uwezo na ujuzi wa kufanya kazi tu ilhali mapepari (wamiliki wa kazi) ndio wenye uwezo wa kuamua mishahara ya wafanyakazi. Marx anaamini kuwa ukosefu wa uwezo kwa wafanyakazi ndicho chanzo cha migogoro ya kitabaka. Alitambua tabaka la kati lililojumuisha wafanyabiashara wadogo. Kwake, ilikuwa vigumu kuainisha tabaka la kati kwa sababu wakati mwingine lilijinasibisha na tabaka la juu na wakati mwingine likajinasibisha na tabaka la chini.

### 2.1.1 Wahusika wa Tabaka la Juu

Marx (1983), anasema kuwa kila tabaka lina sifa zake zinazolibaini na hutambulika kulingana na hadhi yake katika jamii. Mtu huwekwa katika tabaka fulani kutegemea kigezo cha elimu, vipawa, utajiri na utambulisho wake. Tabaka la juu linahusu wahusika walio na nafasi katika jamii. Wahusika hawa wana mali na uwezo kwa sababu ya wao kuwa aidha viongozi wa kiserikali au kidini.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, Ridhaa ni mwathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii ambaye alikuwa katika tabaka la juu. Utabaka wake ulitokana na kiwango cha juu cha elimu alichokuwa nacho. Alikuwa amesomea taaluma ya upasuaji hadi kiwango cha uzamili. Baada ya masomo, Ridhaa alipata ajira katika mashirika mbalimbali yaliyohusiana na taaluma ya afya kabla ya kuzuka kwa ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina.

Kulingana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema kuwa; mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, ilibainika kuwa makazi ya Ridhaa

yalikuwa ya mhusika wa tabaka la juu. Ridhaa alimiliki majumba ya kibiashara kama lile lililokuwa katika mtaa wa Zari ambalo lilibomolewa kwa kilichosemekana kuwa lilijengwa katika sehemu iliyotengewa ujenzi wa *bypass*. Jumba lingine liliteketea kufuatia hitilafu za nguvu za umeme. Daktari Ridhaa alikuwa amefanya kazi katika serikali kwa muda mrefu hata kuwa mkurugenzi wa shirika mojawapo la serikali. Vita vilipokwisha katika nchi ya Wahafidhina, alijenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya kilichotoa huduma za afya kwa umma. Alimwajiri Kaizari kama afisa wa matibabu na Selume kama muuguzi mkuu. Ridhaa akawa mkurugenzi wa kituo hiki na akahamia mtaa wa Afueni walikoishi watu wa tabaka la juu. Mwandishi anasema;

> Kwa kweli huu ni mwezi wa tatu tangu Ridhaa kuhamia kwenye mtaa wa Afueni. Afueni ni mtaa wa raia wenye kima cha juu kiuchumi. Mtu anapoutazama mtaa huu husalimiwa na majengo ya kifahari ya ghorofa, yale ambayo yanaitwa katika janibu hizi ‘town houses.’ (Matei, 2014: 137)

Kulingana na nadharia ya Uhalisia, wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, Bell (1977), anasema kuwa tabaka la juu ni lile linalojumuisha viongozi wanaofisidi raslimali za umma kwa maslahi yao. Kutokana na umiliki wa mali, kufanya kazi za kifahari na kuishi katika mtaa wa watu wenye kiwango cha juu kiuchumi, Ridhaa anatambuliwa kuwa mwathiriwa wa tabaka la juu. Ridhaa aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo mkewe, Terry; mkaza mwanawe, Lily; bintiye, Anatila na mjukuu wake; Becky, waliangamia katika moto ulioliteketeza jumba lake la kifahari. Nyumba hii ikateketezwa motoni na waandamanaji na baadaye Ridhaa akasombwa kwenda kambi za wakimbizi.

Lunga Kangata ni mhusika mwingine aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamii aliyekuwa katika tabaka la juu. Lunga Kangata alikuwa ameajiriwa kazi katika shirika la nafaka la Fanaka kama mkurugenzi mkuu katika kitengo cha kuhakikisha ubora wa bidhaa. Shirika hili lilipoagiza mahindi yaliyokuwa yameharibika, Lunga alikataa kuidhinisha matumizi ya mahindi hayo yaliyokuwa hatari kwa matumizi ya binadamu. Msimamo wake ulimfanya kukorofishana na wakuu wa shirika hili na hivyo akapigwa kalamu kazini. Akahamia katika Msitu wa Mamba ambapo alijishughulisha na kilimo. Kutokana na bidii yake katika kilimo, alipanda ngazi hadi tabaka la juu. Lunga akamiliki nyumba kadhaa, mashamba na mazao. Mwandishi anasema;

> Sasa anamiliki, si nyumba tu, bali pia mashamba makubwa makubwa. Anafuga kuku, bata, mbuzi na ng'ombe. Anaweza kuwaajiri watu kufanya kazi katika mashamba yake. Sasa Lunga ni Lunga Kiriri kweli…Marafiki zake wamempa jina la Msimbo Mkulima Namba Wani. Ametononoka si haba katika msitu huu… (Matei, 2014: 70-73)

Wahusika waliotumiwa katika riwaya teule ni halisi na lugha wanayoitumia inaeleweka jinsi inavyofafanua nadharia ya uhalisia. Masuala yanayoelezwa ni ya kweli kama yalivyotukia katika mandhari halisi. Mathalani, utafiti wa Brady (2018), unaeleza kwamba umaskini huchangiwa na mabadiliko ya kisiasa pamoja na vita vya kisiasa na kikabila. Katika Msitu wa Mamba, kulitokea mizozo ya kitabaka na kikabila miongoni mwa wakazi wa eneo hilo. Migogoro ya kitabaka na kimbari ilipokithiri, serikali ikawahamisha wakazi hawa kutoka Msitu wa Mamba hadi Mlima wa Simba huku mali waliochuma yakiharibiwa na serikali. Lunga aliathirika ambapo mali yake yaliharibiwa, nyumba zake zikabomolewa.

Mwangeka, mwanawe Ridhaa, alisomea taaluma ya uhandisi na kuhitimu chuoni kisha akajiunga na kikosi cha usalama kudumisha usalama. Alipandishwa vyeo kimoja baada ya kingine hadi alipoenda ughaibuni kushughulikia maswala ya usalama. Kupanda ngazi katika kazi kulimweka Mwangeka katika tabaka la juu akilinganishwa na wahusika wengine katika jamii. Akiwa huko ughaibuni, vita vilitokea nchini mwao Wahafidhina. Mkewe, Lily Nyamvula na mwanawe, Becky, waliteketezwa motoni. Aliporejea kutoka ng'ambo alinunua kiwanja na kujenga jumba la kifahari na akamwoa mke mwingine kwa jina Rachael Apondi. Rachael Apondi, mjane wa Mandu, alikuwa akifanya kazi katika serikali. Familia ya Mwangeka ilikuwa ya watu wa tabaka la juu kama anavyofafanua mwandishi;

> Sisemi kwamba wangeweza kutiwa katika lile kumbo la wazazi ambao hukerwa na vinywa vya kulisha. La! Hasha! Mwangeka na Apondi walikuwa mkono wazi. Maskani yao yalimiminika wahitaji kutoka kila pembe ya eneogatuzi lao, nao hawakurudi kwao mikono mitupu. (Matei, 2014: 116)

Rachael Apondi na Mwangeka walimchukua Umulkheri kama mtoto wa kupanga na kumlea na kumsomesha mpaka akahitimu kuingia chuo kikuu kusomea taaluma ya uhandisi katika maswala ya kilimo.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, wahusika kadhaa wameainishwa kuwa wa tabaka la juu. Wanauhalisia wanaamini kuwa, sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake. Osango (2015), anasema kuwa utabaka hutokea wakati watu wachache

wanapohodhi nyenzo za uzalishaji na kuacha wanajamii wengi kuwa maskini. Maskini hubaki wakiuza nguvu zao kwa matajiri, wakipewa ujira duni.

Tom Mangala, mtoto wa Mzee Mangala, aliyekwenda Marekani kusoma alikuwa mhusika wa tabaka la juu. Tom alipohitimu masomo yake alirejea nchini Kiwachema na mke wa kizungu; Jenelle. Tom aliajiriwa katika shirika la Anken na akamjengea babake jumba la kifahari kijijini Baraki. Aidha, Tom mwenyewe alijijengea jumba la kifahari kijijini kwani aliamini itikadi za kwao kuwa mtu ni sharti ajijengee nyumba kwao. Mwandishi anaonyesha kuwa mhusika huyu alikuwa anaishi katika mtaa wa kifahari wa Milimani jijini Tandika alipokuwa amejenga jumba la kifahari. Akida anasema;

> Macho yangu yalituama kwenye kasri tuliyoelekeana nayo. Sampuli ile ile ya kiambo cha mjomba wake Tim. Si maasumini, si Zumaradi. Palikuwa na gari aina ya Benz katika banda la maegesho. (Walibora, 2003: 81)

Mtaa wa Milimani ulikuwa wa kifahari kwani ulikuwa na mandhari ya kupendeza ya miasumini, mawaridhi na zamaradi. Aidha Tom alikuwa na gari zuri aina ya Benz katika banda la maegesho. Taswira ya makaazi ya Tom yanadhihirisha kuwa alikuwa katika tabaka la juu. Tom aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho ambapo babake Mzee Mangala aliuawa na genge la wapiganaji. Tom alikodisha kikosi cha polisi pamoja na marafiki wachache kwenda kumzika babake, Mzee Mangala wilayani Korosho. Baada ya kumzika babake, Tom alishambuliwa na genge la wapiganaji akaachwa yu mahtuti.

Kama anavyodai Marx (1983), kila tabaka lina sifa zake zinazolibaini. Kila tabaka hutambulika kwa hadhi yake katika jamii. Mtu huwekwa katika tabaka fulani kutegemea

kigezo cha elimu, vipawa, utajiri na utambulisho wake. Kila tabaka huonyesha tabia fulani za maisha, ufanisi na mielekeo fulani ya maisha. Viongozi mbalimbali wa kiserikali na kidini katika riwaya hii walibainishwa katika tabaka la juu. Viongozi hawa ni pamoja na Johnson Mabende na  muhubiri James Sanya ambao pia waliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii.

Viongozi hawa walikuwa na mamlaka ya kushawishi vita nchini humo.Wanauhalisia wanaamini kuwa sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake. Kwa mfano, nchini Kenya, mwaka wa 2007/2008, viongozi mbalimbali walishukiwa kuchochea vita vya kijamii ambapo baadhi yao walishtakiwa katika mahakama ya kimataifa ya ICC nchini Uholansi. Masango (2002) anasema kuwa kiongozi ni mtu anayewaathiri watu binafsi au vikundi vya watu miongoni  mwa wanajamii. Johnstone Mabende aliyekuwa mbunge wa eneobunge la Korosho alifadhili mapigano wilayani Korosho. Johnstone Mabende aliteuliwa kama waziri wa usalama wa ndani wa nchi ya Kiwachema. Uteuzi huu uliwasononesha wananchi wengi kwani walifahamu kwamba yeye pamoja na viongozi wengine Wakorosho walichochea vita wilayani Korosho.  Jarida moja liliripoti ifuatavyo;

> Mbunge mheshimiwa Johnstone Mabende, wakereketwa wake na viongozi wa kidini Wakorosho na wasio Wakorosho walikuwa watuhumiwa wakubwa katika mauaji hayo ya halaiki. (Walibora, 2003: 160)

Mheshimiwa Johnstone Mabende aliyekuwa waziri wa usalama wa ndani aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii kwa  kushambuliwa kwa risasi na mtu asiyejulikana na akafa. Baadaye uchunguzi ulibaini kuwa waziri huyo alipigwa risasi na Johnson Muyaka

aliyekuwa afkani ambaye alitorokea nchi jirani. Johnson alimshambulia Mheshimiwa Johnson Mabende kwa sababu kiongozi huyu alichochea ghasia baina ya Wakanju na Wakorosho wilayani Korosho.

### 2.1.2 Wahusika Waliokuwa wa Tabaka la Chini

Gastil (1973), tabaka la chini linajumuisha wafanyakazi, waajiriwa wa mashambani na watu ambao hawana ajira wanaokumbwa na umaskini. Wahusika kadhaa walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii walibainishwa katika tabaka la chini.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, wahusika mbalimbali waliojumuishwa katika tabaka la chini. Wahusika hawa ni Tim, Akida na Tamari. Kulingana na mhimili wa nadharia ya Uhalisia unaosema; mtunzi atumie mazingira halisi na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, mandhari ya mtaa wa Falkland yalikikuwa ya kudunisha mno. Tim alikuwa amepangisha chumba uchwara katika mtaa huu. Alipomaliza kidato cha nane, Tim aliajiriwa kazi ya ukarani katika kiwanda cha kusindika mafuta jijini Tandika na mjomba wake, Samson Tungu. Rafiki yake, Akida, alimtembelea jijini Tandika kuzawadiwa. Baada ya kuzawadiwa na waziri wa elimu, Bwana Kato, kulitokea habari kuwa vita vya kisiasa na kijamii vimezuka wilayani Korosho. Akida aliamua kukaa pamoja na Tim hapo jijini.

Mwandishi anaonyesha kwamba vita hivi viliathiri Wakorosho na Wakanju. Tim aliathirika na vita hivi ambapo, Tamari (dadake Tim), alinusurika kubakwa na kuuawa na genge la wapiganaji. Alilala vichakani na kushuhudia mauaji ya watu hadi alipookolewa na wahisani waliomsafirisha kwenda jijini Tandika na kumwacha mlangoni mwa Tim.

Aidha Tim aliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii kwa kuachishwa kazi. Mwajiri wake, Samson Tungu, alipogundua kwamba Tim anamhifadhi Mkanju chumbani mwake alimfuta kazi. Kuachishwa kazi kwa Tim kuliwaletea matatizo vijana hawa. Tim alitafuta chumba uchwara katika mtaa wa Falkland. Mtaa huu ulikuwa wa watu wachochole. Mwandishi anasema;

> Mtaa wa Falkland, maarufu kwa jina la Kambichafu ulikaa kina Pangu Pakavu. Mabanda yaliyopachanapachana yenye kuta zilizokandikwa kwa udongo na kuezekwa mabati yenye vishimo na kutu ndiyo vilivyokuwa baina ya mabanda hayo yaliyoinamiana. Fondogoo ya marundo ya taka, maji ya mvua na mikojo ya watu, ilichangamana na harufu ya vinyezi vya watoto na watu wazima vikaunda mseto wa mnuko mbaya sana. (Walibora, 2003: 110)

Kwa mujibu wa wanauhalisia, wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii. Maslow (1987), anaeleza kuwa binadamu anahitaji mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, usalama, upendo na kujithamini kabla ya kusonga katika daraja lingine la utabaka. Tunaelezwa kwamba, Akida, Tim na Tamari walikosa mahitaji ya kimsingi. Chumbani walimokaa, hamkuwa na viti, walikalia kitanda kimoja alicholalia Tamari. Hawakuwa na chakula cha kutosha, Tim alikuwa akiwatengenezea chai ya mkandaa isiyokuwa na sukari ila majani chai na maji tu. Mwandishi ananukuu;

> Tim aliinuka akatia majani ya chai kwenye maji yaliyokuwa yanachemka chemchem sufuriani. Akaepua sufuria na kuimimina birikani chai hiyo ya mkandaa.

> Tukainywa kavu, haina sukari wala haiandamani na kipande cha mkate wala chochote. (Walibora, 2003: 114-115).

Hali hii ya ufukara inawabaini Tim, Akida na Tamari kama wahusika wa tabaka la chini waliopitia changamoto tele. Akida aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo babake, Mzee Sululu, aliuawa katika ghasia hizo. Tofauti za kijamii na kisiasa zilichangia Akida kudhulumiwa, kutukanwa na kudharauliwa na Samson Tungu pamoja na Tamari. Tungu na Tim wanasema;

> "Eti Mkanju?" alitikisa kichwa na kuangua kicheko kikavu nilichokiona cha kishetani.
>
> "Kwani mjomba kuna nini?" aliuliza Tim.
>
> "Wakanju?" aliendelea yule mzee huku amenikazia macho."Hakuna watu wajinga kama Wakanju…" (Walibora 2003: 25)

Tamari aliathirika katika vita hivi ambapo alinusurika kubakwa na genge la wapiganaji. Alitembea mwendo mrefu akijificha vichakani mpaka alipopata mhisani aliyembeba kwa gari lake hadi jijini Tandika alipokuwa akiishi nduguye, Tim.

Wahusika wengine waliobainishwa katika tabaka la chini ni Mzee Sululu, Zablon Mapisi, Tito Tembo na Mzee Uledi. Mzee Sululu alikuwa babake Akida na alikuwa mkulima wa kiwango cha chini. Hakuweza kuyamudu masomo ya mwanawe. Sululu alikuwa na masomo ya ngumbaru na alipanda mazao machache ya mahindi, majani chai na kahawa. Mzee Sululu aliandika kitabu cha mashairi kilichoitwa *Kero za Mkiwa*. Diwani hii ilichapishwa na shirika la uchapishaji la Hatubaguani Publishers. Mzee Zablon Mapisi

alikuwa mhusika wa tabaka la chini wilayani Korosho. Mzee Zablon na Sululu walikuwa majirani ambao walitegemea kilimo cha chini kwa mahitaji yao ya kila siku. Tim anasema;

> "Ni kweli shemeji," alishikilia Tim. "Kila mwaka nyie mwapata mazao bora kuliko wazee wangu. Si mahindi, si majani chai, si kahawa. Hata ng'ombe wenu wanatoa maziwa mengi zaidi. Mambo yenu yanatengenea kila mara…" (Walibora, 2003: 13)
>
> Mzee Sululu aliathirika na vita vya kisiasa na kijamii wilayani Korosho kwa kuuawa na jirani yake wa karibu, Mzee Zablon Mapisi. Zablon Mapisi alikuwa Mkorosho huku Mzee Sululu akiwa Mkanju. Akida anaomboleza;
>
> "Mama alikufa ajalini," nilisema baina ya kwikwi za kilio. "Ndugu zangu walionitangulia hata sikuwahi kuwaona. Sasa baba, mboni ya jicho langu jamani…sina wazazi sina ndugu…" (Walibora 2003: 198)

Tito Tembo na Mzee Uledi ni wahusika wengine waliokuwa katika tabaka la chini. Tito Tembo alikuwa mlevi katika mtaa wa Falkland ambaye alijisifu mbele ya walevi wengine kwamba aliwaua Wakanju wengi katika vita vya kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Mwandishi anaonyesha kwamba Akida aliyekuwa anapita karibu na mangweni hayo, aliudhika mno na usemi wa Tembo kwamba aliwaua Wakanju wengi. Akida alichukua gogo la mti na kumfuata Tito hadi msalani na kumtwanga nalo hadi akazirai. Akida akatorokea wilayani Sangura kujificha.

Naye Mzee Uledi alikuwa jirani wa Mzee Sululu aliyekuwa mhusika wa tabaka la chini. Mzee Uledi alikuwa mlevi na aliweza kushambuliwa wilayani Korosho na akalazwa katika hospitali ya Rufaa ya Tandika. Mzee Uledi aliweza kutoka hospitalini, na baada ya vita kwisha wilayani Korosho, aliingia mtaani akawa ombaomba. Mwandishi anasema kwamba familia yake ilikuwa imeangamia katika vita vya kikabila na waliosalia kama Regina, walitorokea jijini pasiwe na wa kumuauni.  Akida anasema;

> Siku moja nilipokuwa napita barabarani nilikumbana na Mzee Uledi. Alikuwa amekaa mbele ya duka la mhindi na mkongojo kauweka pembeni anaomba fedha. Kikandiko kilikuwa ki bado mguuni. Alikuwa katoka mabebe na kuzeeka si haba. Nilimwonea imani maskini. Nikamsalimu na kutumbukiza shilingi mbili nilizokuwa nazo kwenye bakuli lake. (Walibora, 2003: 219)

Kwa mujibu wa nadharia uhalisia katika mhimili usemao; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, Mwalimu Alex ametambuliwa kuwa katika tabaka la chini. Mhusika huyu alikuwa na matatizo ya akili na aliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Mwalimu Alex aliuawa na Wakorosho wenzake. Mauaji haya yalifanywa ili Wakorosho waweze kuhalalisha mashambulizi yao dhidi ya Wakanju. Mwalimu Alex alionekana akimkashfu Mbunge wa Korosho, Johnstone Mabende, kwa kuwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju. Mwalimu Alex anasema;

> "Mheshimiwa sasa unaanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. Wakanju ni ndugu zetu ati. Watu wa fikra kama zako ndio maharabu wa nchi," (Walibora, 2003: 2)

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya waathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii wamebainishwa kuwa katika tabaka la chini. Wahusika hawa ni Lunga, Kairu, Mwanaheri, Kaizari na Subira. Wanauhalisia wanaeleza kwamba sanaa inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe. Marx na Engels (1959), wanasema kwamba matabaka huibuka kwa sababu ya tofauti za kiuchumi. Tabaka la watawala huhodhi mbinu za kuzalisha mali na kubaki kumiliki mali na uwezo wa kifedha. Tabaka la chini lililo na watu wengi linasalia maskini wasio na chochote ijapokuwa nguvu zao wanazoziuza ili kukidhi mahitaji ya kimsingi.

Mwandishi anaonyesha kwamba, Lunga Kangata alihamia Msitu wa Mamba na kupanda mazao baada ya kuachishwa kazi kutoka shirika la nafaka la Fanaka. Yeye pamoja na wakaazi wengine walipata utajiri kutokana na kilimo. Kutokana na tofauti za kitabaka, mizozo ilianza kujitokeza miongoni mwa wakazi wa Msitu wa Mamba. Msitu wa Mamba ulibeba watu wa asili mbalimbali. Serikali ilipoona kwamba uhasama wa kitabaka umezidi, chama tawala kiliamua kuwatafutia wakazi hao mahali kwingine. Lunga na aila yake wakarudishwa Mlima wa Simba ambapo iliaminika kuwa ndipo wazee wake walikotoka, Kaloleni, siku za biashara ya utumwa. Mali aliyokuwa nayo, majumba makubwa, wanyama wa kufugwa vyote vikateketezwa.
Maisha yakambadilikia Lunga Kangata na umaskini ukamkumba. Wanawe waliokuwa wakisomea shule za kifahari, wakarejea kusomea shule za kutwa. Lunga akawapoteza marafiki zake. Fidia ya serikali aliyopewa haikutosha kukidhi mahitaji yake. Mwandishi ananukuu ifuatavyo;

> Alikumbuka mali yake ambayo aliichuma kwa viganja vyake katika msitu wa Mamba. Sasa ameipoteza. Ameyapoteza maisha yake, amewapoteza ndugu na marafiki zake. Wanawe waliosoma katika shule za kifahari, sasa fidia aliyopewa na serikali haitoshi hata kuwapeleka katika shule za watu wa kima wastani. (Matei, 2014: 79)

Mkewe Lunga,Naomi, alipoona mambo yamewaendea kombo, akaamua kumtoroka mumewe na kuhamia mji wa Karaha. Lunga akashindwa kustahimili matatizo haya, akashikwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na mwaka mmoja baadaye, Lunga akafariki na kuwaacha wanawe. Mwandishi anasema;

> Katika hali hii Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki. (Matei, 2014: 81-82)

Kutokana na mhimili wa nadharia ya uhalisia, sanaa inapaswa ieleze ukweli wa Maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe. M'ngaruthi (2015), anasema kwamba,wanasiasa na viongozi wanahodhi na bado wanahodhi nyenzo za kuzalisha mali na kujiweka katika tabaka la kwanza. Wananchinao husalia katika tabaka la chini la watu maskini. Kairu alikuwa mmojawapo wa wanafunzi katika shule ya Tangamano aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Walipokuwa wakitoroka ghasia za kisiassa na kijamii kutoka maeneo yao, ndugu yake mdogo alipatwana ugonjwa wa udhaifu wa mapafu na akaaga dunia. Mamake alimzika kichakani na baadaye wakapelekwa katika kambi za wakimbizi. Kairu anawaeleza wanafunzi wenzake kuwa mamake alikuwa mzazi

wa pekee aliyekuwa maskini. Mamake alikuwa muuza samaki na kwamba baada ya mzozo kutokea kuhusu umiliki ziwa kuu, biashara ya samaki iliathirika. Wavuvi waliambiwa kuwa ardhi ni yao lakini maji si yao na hivyo hawakuwa na kibali cha kuvua samaki. Kairu anaeleza;

> Samaki wamekuwa adimu sokoni na bila shaka bei yake inaweza kutabirika. Kwa mtu maskini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzisha biashara nyingine, maisha yamekuwa magumu zaidi. (Matei, 2014:93)

Kufuatia mizozo ya umiliki wa ardhi na maji ya ziwa, biasharailiathirika na familia ya Kairu na mamake ikakumbwa na matatizo. Anasema kwamba maisha yaliwawia magumu hata karo ya kuwalipia wanawe shuleni ikawa ngumu ambapo ilibidi mamake alipe kiasa anachoweza kwa muda.

Kaizari na aila yake ni wahusika wengine walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa katika tabaka la chini. Mwandishi anaeleza kwamba Kaizari alishambuliwa na vijana waliongozwa na Mzee Kedi ambao pia waliwabaka mabinti wake wawili, Lime na Mwanaheri. Mkewe, Bi. Subira alikatwa kwa sime akazirai huku Kaizari akishuhudia kubakwa kwa mabinti wake asiwe na uwezo wa kuwasaidia. Baadaye Kaizari na aila yake walipelekwa katika kambi za wakimbizi, walikokaa kwa muda kabla ya kuhamishwa tena kwenda katika Mlima wa Simba. Walijijengea nyumba katika mlima wa Simba na kuselelea hapa pamoja na wakimbizi wengine kwa muda kabla mizozo ya tofauti za kiusuli kutokea. Mzozo katika Mlima wa Simba ulipozidi, chama tawala kiliwahamisha hadi Msitu wa Mamba kulipoaminiwa kuwa kwao. Kaizari, mkewe Subira, na wana wao, Lime na

Mwanaheri walijenga nyumba kufu yao na mabinti hawa wakarudishwa shule za vijijini kuendelea na masomo. Mwanaheri anasema;

> "Baada ya kurudishwa nyumbani kutoka Msitu wa Mamba, baba yangu, Mzee Kaizari, aliweza kuyajenga maisha yetu upya. Alijenga nyumba kufu yetu pale pale penye lile ganjo,"alihadithia Mwanaheri baada ya Kairu kumaliza kisa chake. (Matei, 2014: 93)

Mzee Kaizari aliendelea kuishi maisha ya tabaka la chini huku mkewe Subira akiendelea kutengwa kwa misingi ya tofauti za kimbari na mamamkwe wake pamoja na watu wa jamaa ya bwanake. Subira aliposhindwa kustahimili kero hizo, aliamua kutorokea mji wa Kisuka.

## 2.2 Kuainisha Waathiriwa Kijinsia

Steady (1981), anafafanua kuwa jinsia ni uhusiano wa kijamii na kitamaduni unaozingatia kugawanya majukumu kwa kigezo cha jinsia. Jinsia inasababisha kutokea kwa tofauti kati ya mwanamke na mwanaume kutegemea tofauti majukumu kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

### 2.2.1 Wahusika wa Kiume

Riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, inambaini Akida Sululu kama mhusika wa jinsia ya kiume aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Akida alikuwa amemaliza masomo ya shule ya msingi kutoka shule ya Baraki na akawa mmojawapo wa wanafunzi watatu bora katika taifa la Kiwachema. Babake, Mzee Sululu, alimruhusu

kwenda jijini Tandika katika makao makuu ya wizara ya elimu kuzawadiwa na waziri wa elimu. Baada ya kuzawadiwa hakuweza kurejea nyumbani kwao Korosho kwa sababu vita vilizuka wilayani humo. Akida na babake, Mzee Sululu, walikuwa Wakanju walioishi wilayani Korosho. Wakanju na Wakorosho walizozana mara kwa mara . Mzee Uledi anasema;

> "Wewe ni mtoto wa Sululu ul'okuja Tandika kuzawadiwa na waziri wa elimu?
>
> "Naam," nikajibu.
>
> "Tulifurahi kusikia ukitajwa redioni. Mtoto wa Mkanju mwenzetu, masomoni amewabwaga wote
>
> Kiwachema nzima."
>
> "Niliacha nyumbani kukiwa salama, kumbe mambo yatalipuka nyuma yangu." (Walibora, 2003: 76)

Mzee Sululu aliuawa na jirani yake, Mzee Zablon Mapisi, ambaye alikuwa mhusika wa jinsia ya kiume.Tim Mapisi ni mhusika mwingine ambaye ni kijana wa kiume wa Mzee Zablon aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Tim alikuwa amemaliza masomo ya shule ya msingi na alikuwa ameajiriwa katika kiwanda cha kusindika mafuta jijini Tandika. Aliathirika na vita vya kijamii ambapo babake, Mzee Zablon, alijitia kitanzi baada ya jamaa zake kuuawa katika vita hivyo vya kisiasa na kijamii. Tim anaeleza;

> "Vita vilikuwa vimekwisha. Tulikwenda na babangu. Sitayasahau mambo tuliyoyaona. Marundo na marundo ya maiti. Haidhuru tuliwatambua watu wa aila yetu. Tingatinga ilitumika kuchimba shimo kubwa na kuzifukia maiti hizo pamoja. Nilishindwa kula kwa siku nyingi." (Walibora, 2003: 197)

Kupitia nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; sanaa iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku ilibainika kuwa, mzee Zablon alishiriki katika mauaji ya Wakanju. Baadaye naye Zablon alijitia kitanzi na kumwachia Tim jukumu la kumtunza ndugu yake wa kike, Tamari. Tamari alikuwa ameathirika na vita baada ya kujinusuru kutokana na jaribio la kubakwa na vijana waliokuwa wakiandamana. Alitoroka, akalala vichakani na kushuhudia mauaji ya watu wengi wilayani Korosho. Alisaidiwa na wahisani waliomsafirisha hadi mlangoni mwa Tim jijini Tandika.

Tom Mangala na babake, Mzee Mangala, ni wahusika wengine wa jinsia ya kiume walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Tom alikuwa mtoto wa pekee wa kiume wa Mzee Mangala. Alikuwa ameenda Marekani kusomea shahada ya uzamili na akarejea nyumbani na mke wa asili ya kizungu. Mwandishi ananukuu;

> Tim alisisitiza sana tumpitie Tom, mtoto wa pekee wa Mzee Mangala wa kijijini kwetu. Tom alikuwa msomi. Alikwenda Marekani kusoma akahitimu na shahada ya uzamili. Mkewe Mzungu aliyempata huko ndiye shahada ya ziada aliyorejea nayo Kiwachema. (Walibora, 2003: 80)

Vita vilipotokea wilayani Korosho, Mzee Mangala aliuawa. Tom, Akida na Tim waliuhamisha mwili wa Mzee Mangala hadi hospitali ya Rufaa ya Tandika. Tom alikodisha maafisa wa polisi pamoja na marafiki wachache wakausafirisha mwili huo hadi nyumbani kwao Baraki kuuzika. Tom alipomaliza kumzika babake, genge la wapiganaji lilimshambulia Tom kwa kuja kumzika Mkanju wilayani Korosho. Maafisa wa polisi aliowakomboa Tom hawangeweza kumuokoa kwa sababu wale waliomshambulia Tom

walikuwa maafisa wa polisi na wapiganaji wengine ambao waliongozwa na mkubwa wao. Baada ya kushambuliwa, Tom aliachwa huko huku maofisa wa polisi aliowakomboa pamoja na Tim wakitoroka kwa gari walilokuja nalo. Akida alimbeba Tom kwa toroli hadi barabara iendayo jijini Tandika alikopata wahisani wakamsaidia kumpeleka Tom katika hospitali ya Rufaa ya Tandika.

Mheshimiwa Johnstone Mabende alikuwa mhusika wa kiume aliyekuwa na mamlaka katika uongozi wa Kiwachema. Kama wanavyoeleza wanauhalisia kwamba wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, tuligundua kuwa viongozi wa serikali walichochea ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Matara (2014), anasema kuwa lugha waitumiayo wanasiasa na viongozi wengine huathiri wananchi kwa njia hasi au chanya. Wanachochea maamuzi ya raia kutegemea na kile wasemacho kwa raia.

Masango (2002), kiongozi ni mtu anayewaathiri watu binafsi au vikundi vya watu katika jamii. Johnstone Mabende aliwachochea Wakorosho na Wakanju kupigana. Anawarejelea Wakanju kama 'madoadoa' ambao walistahili kuondolewe wilayani Korosho. Aidha, Mabende pamoja na wakereketwa wengine walifadhili mapigano wilayani Korosho. Jarida moja liliripoti ifuatavyo;

> Mbunge Mheshimiwa Johnstone Mabende, wakereketwa wake na viongozi wa kidini Wakorosho na wasiokuwa Wakorosho walikuwa watuhumiwa wakubwa katika mauaji hayo ya halaiki: Kioja kilioje kubaini kwamba makasisi waliokuwa wakikaa mbali mijini na majijini kama John Njalala wakifadhili kisiri mapigano hayo. (Walibora, 2003: 160)

Kulingana na wanauhalisia, sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, mwalimu Alex ametambuliwa kama mhusika wa jinsia ya kiume aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamii. Mhusika huyu alikuwa na matatizo ya kiakili lakini alielewa yaliyoendelea nchini mwao. Mwalimu Alex alimkashfu Mheshimiwa Johnstone Mabende kwa kuwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju. Mwalimu Alex alisema;

> "Mheshimiwa sasa unaanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. Wakanju ni ndugu zetu ati. Watu wa fikra kama zako ndio maharubu wa nchi." (Walibora, 2003:2)

Mwalimu Alex aliuawa na Wakorosho wenzake ili isemekane kuwa Wakanju ndio walimuua ili wapate kuhalalisha mashambulizi yao dhidi ya Wakanju.

Tito Tembo na Mzee Uledi ni wahusika wengine wa jinsia ya kiume walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Tito Tembo ni mwanamume aliyekuwa mlevi ambaye alimfanana Zablon kwa sura na kimo. Aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo Akida alimtwanga kwa gogo la mti na kumwangusha mchangani. Hii ni baada ya Akida kumfananisha na Mzee Zablon. Tito Tembo alikuwa akijisifu kwa walevi wenzake kwamba alikuwa amewaua Wakanju wengi katika vita wilayani Korosho. Tembo anasema;

> "Mwenyewe mimi usinione hivi nimeua Wakanju wengi sana," alijipigapiga kifua. "Usione wembamba wa reli, garimoshi hupita." (Walibora, 2003: 13)

Mzee Uledi naye alikuwa babake Regina na alikuwa ameshambuliwa na genge la wapiganaji wa jamii ya Wakorosho. Alilazwa katika hospitali ya Rufaa ya Tandika kwa sababu ya majeraha. Mzee Uledi anasema;

> "Palikuwa hapana budi ila kila mtu kuiokoa nafsi yake mwenyewe. Nilimwonea imani mwenzangu, ila ningefanya nini? Nilitazama ng'ambo kule n'kaona wingu la moshi na miale ya moto, nyumba zinateketea. Nikaiambia nafsi yangu 'niponye.' Hata watoto wangu na wake zangu sikuwafikiria. Nilipasua weu, nilikata mbuga. Tembo ilinitoka kichwani. Almuradi mahambe wale hawakunipata." (Walibora, 2003: 78)

Mzee Uledi alikuwa Mkanju aliyekuwa jirani na rafiki wa Mzee Sululu. Kupitia utafiti huu, tuligundua kwamba Mzee Uledi alikuwa mlevi chakari.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014) wahusika kadhaa wa jinsia ya kiume waliathiriwa na ghasia za kisiasa katika nchi ya Wahafidhina. Daktari Ridhaa na Mwanawe wa kiume, Mwangeka, ni baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii. Familia ya Ridhaa iliangamia kwa kuteketezwa motoni na waandamanaji waliokuwa wakipinga uteuzi wa Bi. Mwekevu kama kiongozi wa taifa la Wahafidhina. Mkewe Bi. Terry, bintiye Anatila, na mjukuu wake Becky waliteketezwa na genge la wapiganaji na kumuathiri Daktari Ridhaa. Mwandishi anasema;

> Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake, Becky. Anawaona wote mbele ya macho yake yaliyojaa mavune. (Matei, 2014: 5)

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; Sanaa lazima iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku ilibainika kuwa Ridhaa iyapoteza mali yake. Jumba lake la kifahari alilokuwa akiishi liliteketezwa na vijana wakiongozwa na Mzee

Kedi ambapo aila yake iliangamia. Majumba mengine mawili aliyokuwa amepangisha yaliteketea ambapo moja lilibomolewa na serikali kwa kile kilichosemekana lilikuwa limejengwa kwenye ardhi iliyotengewa ujenzi wa *bypass*. Jumba lingine liliteketea kwa moto kwa kile kilichosemekana kuwa hitilafu za nguvu za umeme. Mwangeka naye aliathirika kwa ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Mwangeka alikuwa amesafiri kwenda ng'ambo kudumisha usalama huku nchini mwao kukitokea vita vya kisiasa na kijamii ambapo mkewe, Lily Nyamvula, na mwanawe, Becky, wkiangamia. Ridhaa anawaza;

> "Maskini mwanangu, hata maisha ya unyumba hakuwa ameyakinai. Amekuwa mjane." aliwaza Ridhaa baada ya kukamilisha usimulizi wake. (Matei, 2014: 57)

Lunga Kiriri Kangata ni mhusika mwingine wa jinsia ya kiume aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Lunga alipofutwa kazi kutoka shirika la nafaka la Fanaka, alihamia Msitu wa Mamba ambapo alishiriki shughuli za kilimo. Hata hivyo, jamii ya Msitu wa Mamba iliyojumuisha watu kutoka makabila mbalimbali ilikumbwa na uhasama kutokana na tofauti za kitabaka na uhasama wa kiusuli. Mizozo hii ilipozidi, serikali iliwahamisha kina Lunga Kangata na wakazi wengine hadi Mlima wa Simba. Mwandishi anasema;

> Wengine kama Lunga, ambaye tangu hapo hakujua kitovu chake hasa, walitimuliwa pamoja na familia zao. Hawakujua walikokuwa wakipelekwa hadi baada ya miezi mitatu, Lunga alipogundua kuwa amerudishwa kwenye Mlima wa Simba ambako inaaminiwa mababu zake walikuwa wamehamia kutoka Kaloleni, (Matei, 2014: 76)

Kuhamishwa kwa Lunga na aila yake kulimwathiri Lunga. Alikumbwa na ufukara pamoja na upweke kwani mali yake yalikuwa yameharibiwa na pia aliwapoteza marafiki zake. Mkewe, Naomi, na wanawe, Umulkheri, Dickson na Mwaliko, wakaathirika pakubwa. Naomi aliamua kumtoroka Lunga na kumwachia ulezi wa watoto. Lunga alishindwa kustahimili, akashikwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na baada ya mwaka mmoja akaaga dunia.

Kaizari ni mhusika wa jinsia ya kiume aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa ambapo mabinti wake, Mwanaheri na Lime, walibakwa na vijana watano chumbani mwake. Mkewe, Subira, alishambuliwa na kukatwa kwa sime akazirai. Kaizari hakuweza kuwasaidia kwani genge hilo la vijana lilimzidi nguvu. Baada ya unyama huu, Kaizari na aila yake walipelekwa katika kambi za wakimbizi.Vita vilipokwisha, walirudishwa katika Msitu wa Mamba. Kaizari anasema;

> "Baadaye genge hili la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti wangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa. Nilijaribu kwa jino na ukucha kuwaokoa lakini likawa suala la mume nguvuze! Mahasimu hawa walitekeleza unyama wao na kuniacha bila kunigusa, niuguzie majeraha moyoni." (Matei, 2014: 25)

Mizozo ilipokithiri katika Msitu wa Mamba, Kaizari na familia yake walirudishwa katika Mlima wa Simba.

### 2.2.2 Wahusika wa Kike

Kohrs (2003), anadai kwamba matatizo kati ya mwanamume na mwanamke hayatasuluhishwa kwa kuliondoa tatizo la upande mmoja tu. Hata kukiwepo na usawa kati ya mwanamume na mwanamke, maslahi kama ya kikoloni na ubaguzi bado yatakuwepo.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003),* Tamari ni mhusika wa jinsia ya kike aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Tamari alikuwa bintiye Mzee Zablon Mapisi kutoka kabila la Wakorosho aliyesomea shule ya msingi ya Baraki. Vita vilipotokea wilayani Korosho, Tamari alitorokea vichakani na kushuhudia maafa ya Wakorosho na Wakanju waliopigana. Mwandishi anasema kwamba Tamari alinusurika kubakwa na magenge ya wapiganaji. Binti huyu aliokolewa na wahisani waliomsafirisha hadi jijini Tandika alipokuwa akiishi nduguye Tim. Pam anasema;

> "Msichana wa watu mzuri kaponea tundu la sindano: Walijaribu kumnajisi akajinasua na kukwepa. Ametembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa. Ameona maiti ngapi sijui? Ameona watu wakiuawa, mtoto mdogo pale alipo. Anasema alipata lifti ya lori la wafadhili wengine waliomleta mpaka hapa kwenye geti…" (Walibora, 2003: 67-68)

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014),* wahusika wengi wa jinsia ya kike waliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Terry, mkewe Ridhaa na Anatila, bintiye aliyekuwa mwanafunzi wa shule moja ya upili ni baadhi ya wahusika wa jinsia ya kike walioteketezwa na moto chumbani mwao. Naye Lily Nyamvula na mwanawe, Becky, waliathirika kwa kuangamia katika moto huo. Mwandishi anasema;

> Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake, Becky. Anawaona wote mbele ya macho yake yaliyojaa mavune. (Matei, 2014: 5)

Kama wanavyoeleza wanauhalisia, fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe, ilibainika kuwa baadhi ya wahusika wa kike waliathirika kwa kubakwa. Wood (2018), anafafanua kuwa ubakaji ni mojawapo ya madhara ya vita vya kisiasa na kijamii. Katika riwaya hii, Lime na Mwanaheri, mabinti wa Mzee Kaizari, walivamiwa chumbani mwao na vijana watano waliowabaka huku wazazi wao wakishuhudia. Kaizari na mkewe, Subira, hawakuweza kuwanusuru kwani genge hili liliwazidi nguvu. Bi. Subira alikatwa kwa sime na kubakia hali mahututi. Mzee Kaizari naye alizirai na alipopata fahamu, walisombwa kwenda kambi za wakimbizi ili kunusuriwa kutoka kwa uvamizi zaidi. Kaizari anasema;

> Mahasimu hawa walitekeleza unyama wao na kuniacha bila kunigusa, niuguze majeraha ya moyo. (Matei, 2014: 25)

Mbali na Subira kushambuliwa na vijana waandamanaji, alifanyigwa ubaguzi na wakwe zake. Ubaguzi huu ulimsononesha mno Subira akaamua kutorokea mji wa Kisuka alipojihusisha na unywaji wa pombe haramu. Unywaji huu wa pombe ulimfisha huko jijini Kisuka. Mwanaheri anasema;

> “Nasikia mama yangu ametoka kwenye jamii ya Bamwezi, baba mnajua jamii yake bila shaka. Daima mama alichukuliwa kama mgeni, si katika boma letu tu, bali pia katika kijiji kizima. Haikuwa ibra kumsikia nyanya akimrejelea kama Muki, yaani

> ‘huyo wa kuja’, na kusema kwamba msichana wa Bamwezi, hata akiwa na umri wa miaka tisini ni msichana wa Bamwezi tu…” (Matei, 2014: 94)

Umulkheri ni mhusika mwinginre wa kike aliyeathirika kufuatia ghasia za kisiasa na kijamii zilizozuka katika nchi ya Wahafidhina. Babake, Mzee Lunga Kangata, alifariki kutokana na athari za migogoro ya kisiasa na kijamii. Lunga Kangata alipatwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na baadaye akaaga dunia. Aliwaacha wanawe, Dick, Mwaliko na Umu chini ya uangalizi wa kijakazi wao. Mwandishi anasema;

> Mwaka wa kwanza ulikuwa mgumu mno. Japo majirani walimsaidia kama ndugu, Lunga alilazimika kuwa baba na mama wa watoto wake, na hilo usilione kuwa jepesi. Katika hali hii, Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo, Lunga alifariki. (Matei, 2014: 81-82)

Naomi, mkewe Lunga, alikuwa ametoroka na kumwachia majukumu ya kuwalea watoto wake. Baada ya siku chache, kijakazi Sauna, aliwatorosha ndugu za Umulheri, Dick na Mwaliko na kuwauza katika madanguro ya kuuza mihadarati. Umulkheri aliwasaka na pia kuripoti katika kituo cha askari lakini hakuwapata. Alipowakosa, akaamua kutorokea jiji la Karaha alikokutana na rafiki yake wa utotoni, Hazina, ambaye alimpa hifadhi. Hazina alimpeleka katika shule ya Tangamano ambapo aliendelea na masomo. Umulkheri anasema;

> “Nani katika umri mdogo kama huu wangu aliyewahi kushuhudia mawi kama niliyoyashuhudia? Binadamu kumhusudu mwenzake hadi kumfutisha kazi. Mtu

> unamtazama jirani yako anachinjwa bila mwombezi, majizi yakivamia mali ya watu, nyingine ikikatalia migongoni mwao!Mama mzima akiwaacha wana…" (Matei, 2014: 90)

### 2.3 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Elimu

Kwa mujibu wa Mandela (1994), elimu ndiyo injini ya maendeleo ya kibinafsi. Ni kupitia kwa elimu ambapo binti wa maskini atakuwa daktari, mwana wa mchimba madini atakuwa msimamizi wa machimbo; mtoto wa mfanya kazi wa shamba atakuwa rais wa taifa kubwa. Wahusika walioathirika walikuwa na viwango mbalimbali vya elimu. Baadhi walikuwa na elimu ya vyuo, huku wengine wakiwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi.

#### 2.3.1 Wahusika Waliokuwa na Elimu ya Chuoni

Kama anavyosema Millet (1969), elimu humpa mtu nguvu ya kujiendeleza. Elimu huwawezesha vijana kutambua uhalisia wa maisha na hujenga uhuru wa ndani, huwapa mwanga na kuwakuza kimaadili. Baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii walikuwa na elimu ya kiwango cha chuoni.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, tuliwatambua wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa na elimu ya vyuo. Tom Mangala na mkewe Jenelle ni wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kikabila waliokuwa na elimu ya chuo kikuu. Tom alikuwa mtoto wa kiume wa Mzee Mangala kutoka wilaya ya Korosho aliyeenda nchini Marekani kusomea shahada ya uzamili. Alipohitimu, alirejea nyumbani na mke wa asili ya kizungu aliyeitwa Jenelle. Mwandishi anasema;

> Tom alikuwa msomi. Alikwenda Marekani kusoma akahitimu shahada ya uzamili. Mkewe mzungu aliyempata huko ndiye shahada ya ziada aliyorejea nayo Kiwachema. Mradi Tom alikuwa simulizi kwetu kijjiini. La kwenda ng'ambo kusoma ni jambo la namna yake kwa watu wa kwetu, kaifa ya kumwoa mzungu. (Walibora, 2003: 80)

Kupitia nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe, ilibainika kuwa, Tom alitumia elimu aliyopata kuboresha maisha ya jamii yake. Tom aliboresha makazi yao kwa kumjengea babake jumba la kifahari kijijini mwao Baraki. Vilevile akajenga majumba mawili mazuri ya kifahari. Jumba moja alilijenga jijini Tandika katika mtaa wa Milimani alipoishi na mkewe Jenelle. Tom aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Alipoenda kumzika babake, Mangala, alivamiwa na kushambuliwa na genge la wapiganaji walioongozwa na Zablon. Aliachwa katika hali mahtuti ambapo Akida alimnusuru kwa kumsafirisha hadi hospitali ya rufaa ya Tandika.

Kulingana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, Alex ni msomi aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Mwalimu huyu alikuwa akifundisha katika shule ya msingi ya Baraki walikosomea Tim, Akida na Tamari. Mwalimu Alex alikumbwa na changamoto za kiakili akawa mwehu. Hata hivyo tulibaini kuwa, Mwalimu Alex alikuwa jasiri ambapo aliweza kumkashfu mbunge wa eneo la Korosho, Mheshimiwa Johnstone Mabende. Mbunge huyu alikuwa akiwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju wilayani Korosho. Akida anasema;

> "Nikamvua koti lake na shati na kumpepea upepo. Nikayatumia mafunzo ya hayati mwalimu wangu Alex ya utoaji wa msaada wa kwanza. Mwajiri wangu alianza kupata fahamu pole pole" (Walibora, 2003: 167)

Mwalimu Alex aliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii kwa kuuawa na Wakorosho ili wapate halali ya kuwashambulia Wakanju walioishi Wilayani Korosho. Mwili wake ulipatikana umekatwakatwa na kutupwa kando ya mto Kibisi. Baadaye, kulisambaswa vijikaratasi vilivyosema kwamba Wakanju sharti wahame kutoka wilaya ya Korosho.

Riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, inaonyesha waathiriwa kadhaa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuwa na viwango mbalimbali vya elimu. Daktari Ridhaa, Mwangeka, Lily Nyamvula na Mzee Kaizari ni baadhi ya wahusika waliokuwa na viwango mbalimbali vya elimu ambao waliathirika. Ridhaa alikuwa na kiwango cha juu cha elimu. Kupitia elimu yake, aliweza kuwahudumia wagonjwa katika mashirika mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya nchini Kiwachema. Ridhaa anasema;

> "Katika maisha yangu kama mwanafunzi wa udaktari na baadaye masomo ya uzamili katika taaluma ya upasuaji, sikuwahi kujihisi kama asiyeweza kuyahimili maisha yake jinsi nilivyohisi siku hii." (Matei, 2014: 55-56)

Daktari Ridhaa aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Katika ghasia hizo, aila yake iliangamia motoni huku mali yake yakiteketezwa. Vita vilipokwisha, Ridhaa alijenga kituo cha kibinafsi cha utoaji huduma za afya. Katika kituo hiki, aliwaajiri Kaizari na Selume huku yeye akiwa mkurugenzi.

Mwangeka alikuwa msomi aliyesomea taaluma ya uhandisi katika chuo kikuu. Mwangeka alikutana na mkewe, Lily Nyamvula, chuoni ambaye pia alikuwa akisomea taaluma ya uanasheria. Licha ya Mwangeka kusomea taaluma ya uhandisi, alighairi nia ya kuwa mhandisi, akajiunga na kikosi cha ulinzi ambapo aliajiriwa na kupanda ngazi za uongozi hadi alipoenda ughaibuni kudumisha usalama. Akiwa huko ughaibuni, ndipo ghasia za kisiasa na kijamii zilipozuka nchini mwao ambapo mkewe na mtoto wake pamoja na mamake na dadake waliuawa. Mwandishi anasema;

> Aliinamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambapo alisomea uhandisi. Hapo ndipo alipokutana na mkewe Lily Nyamvula. Siku hizo Nyamvula alikuwa akisomea shahada ya uanasheria. Mwangeka alihitimu masomo yake akajiunga na kikosi cha wanamaji. (Matei, 2014: 61)

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema, wahusika wasawiriwe kama walivyo, tulibaini kuwa Lunga alikuwa mchapa kazi kutokana na elimu yake. Kupitia kwa elimu aliyopata, aliajiriwa katika shirika la maghala ya Fanaka ambako alikuwa mkurugenzi katika kitengo kilichoshughulikia viwango vya ubora wa bidhaa. Hata hivyo kutokana na msimamo wake thabiti kuhusu ubora wa bidhaa katika shirika hilo aliachishwa kazi. Shirika hilo lilikuwa limeagiza mahindi yaliyokuwa yameharibika yakiwa na sumu ambayo ilikuwa hatari hata kwa panya. Lunga aliwakabili wakubwa wake na kupinga uagizaji wa mahindi hayo. Mwandishi anaeleza;

> Mwezi mmoja baadaye, akiwa ofisini mwake, akili yake kaizamisha kwenye shughuli ya kuibua mikakati ya kukabiliana na janga la njaa nchini, Lunga alipokea barua ya kumfuta kazi. (Matei, 2014: 71)

Lunga alirudi katika Msitu wa Mamba kufanya shughuli za kilimo. Aliathirika na ghasia za kijamii ambapo katika msitu wa Mamba kulikuwa na mizozo ya kijamii na kitabaka. Walioishi katika msitu huo walikuwa maskwota waliotoka kambi za wakimbizi. Mizozo katika msitu huo ilipokithiri, serikali iliwahamisha wakazi hawa kwenda Mlima wa Simba. Mali na mazao yao yakateketezwa na serikali kuu.

Hali kadhalika, Kaizari ni mwathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii aliyekuwa na kiwango cha juu cha elimu ya chuo. Tunaelezwa kwamba Daktari Ridhaa alipojenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya, alimuajiri Kaizari kama afisa wa matibabu pamoja na wahudumu wengine. Kutokana na ajira hii, Kaizari aliweza kuikimu familia yake. Mwandishi anasema;

> Wakati Selume akiwazia kustaafu mapema, naye Ridhaa ndipo anapomalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Nafasi za kazi zilipotangazwa, Selume na Kaizari waliomba kazi, Selume akaajiriwa kama Muuguzi mkuu, naye Kaizari kama afisa wa matibabu. (Matei, 2014: 141)

Kaizari alikuwa ameathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina ambapo aila yake ilishambuliwa na genge la wapiganaji. Vijana watano mabarobaro walivamia familia ya Kaizari, wakamkata mkewe kwa sime kisha wakawabaka mabinti wake, Lime na Mwanaheri. Baadaye Kaizari na aila yake walisombwa kwenda katika kambi za wakimbizi. Katika kambi hizi, kulikuwa na matatizo mengi kama vile magonjwa, njaa, ukosefu wa maji, uhaba wa huduma za kimsingi na upotovu wa maadili. Taswira hii ya kambi za wakimbizi inaingiliana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; msanii

atumie mandhari asili na ayaendeleze kwa kuonyesha hali ya ukawaida wake. Wakimbizi wengi walifariki kufuatia magonjwa yaliyoletwa na ukosefu wa maji safi na huduma nyingine za kimsingi.

### 2.3.2 Wahusika Wanafunzi wa Shule za Msingi na Upili

Waandishi wa riwaya teule za Kiswahili wametambua wanafunzi wa shule za msingi na upili ambao waliathirika. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, wahusika hawa ni pamoja na Akida Sululu na Tamari Mapisi. Akida alikuwa ameupasi vyema mtihani wa darasa la nane na kuwa mwanafunzi bora zaidi nchini Kiwachema. Akida alielekea mjini Tandika katika makao makuu ya wizara ya elimu kuzawadiwa. Babake, Mzee Sululu, alimfanyia mpango kwenda jijini Tandika kufuatia matokeo yake pamoja na bima ya marehemu mamake na pia kufuatia machapisho ya kitabu cha babake katika shirika la uchapishaji la Hatubaguani Publishers.  Alipofika jijini, Akida alizawadiwa na waziri wa elimu Bwana Kato. Akida anasema;

> Waziri Bwana Kato alitupongeza sisi 'wanafunzi watatu bora' kwa kushinda mtihani vyema zaidi. Akaahidi kuwa serikali imetenga fedha kugharamia masomo yetu hadi kiwango chochote tuwezacho kukifikia…Nilikuwa nambari tatu taifa zima kwenye mtihani, lakini mimi ndiye niliyekuwa wa kwanza kuzawadiwa. (Walibora, 2003: 50)

Kama unavyosema mhimili wa nadharia ya uhalisia; sanaa imulike maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, eneo la Korosho lilikumbwa na vita vya kisiasa na kijamii. Siku chache tu baada ya Akida kuzawadiwa kama mwanafunzi bora, vita vya kisiasa na kijamii

vilizuka wilayani Korosho. Makabila ya Wakorosho na Wakanju yalivamiana kufuatia uchochezi uliofanywa na viongozi wa kisiasa na kidini. Mzee Sululu, aliuawa katika vita hivyo na ikawa vigumu kwa Akida kuendelea na masomo ya shule ya sekondari. Akida akastakimu na rafikiye jijini Tandika kwa muda kisha baadaye akatorokea wilayani Sangura baada ya kumshambulia Tito Tembo. Alikaa wailayani Sangura kwa miaka mitatu, tena akarejea jijini Tandika.

Tamari ni mwanafunzi mwingine wa shule ya msingi aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamiii. Masomo yake ya msingi yalikatishwa kwa muda baada ya vita kuzuka wilayani Korosho. Mwandishi anasema;

> Tim alikuwa shemeji wa kupanga, sikuwa nimeoa kwao wala yeye kuoa kwetu. Alikuwa na dada yake msichana mrembo, mwingi wa ndaro na mikogo, jinale Tamari. Imepita miezi michache tangu nilipofanya mtihani wa taifa wa darasa la saba na Tamari, kwenye shule ya msingi ya Baraki. (Walibora, 2003: 7-8)

Masomo ya Tamari ya shule ya msingi yalikatishwa vita vya kijamii na kisiasa vilipozuka wilayani Korosho ambapo Wakanju na Wakorosho walipigana baada ya kuchochewa. Alitorokea jijini Tandika alikoishi nduguye, Tim, ili aweza kujinusuru kutoka kwa mashambulizi. Vita vilipoishi, Tim alimrudisha Tamari shuleni. Alianza kusomea darasa la sita katika shule ya Mumbaimbai jijini Tandika.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina walikuwa wanafunzi. Kwa mfano, Mabinti wa Kaizari, Lime na Mwanaheri, walikuwa wanafunzi wa shule ya msingi. Mabinti hawa

walinajisiwa na vijana watano nyumbani mwao. Baada ya unyama huu, wasichana hawa walipelekwa katika kambi za wakimbizi. Mwanaheri anasema;

> "Mimi na ndugu yangu, Lime, tulirudi shuleni mle mle kijijini mwetu tu. Haikuwa vigumu kuyazoea maisha tena kwani wanafunzi wenzetu walitupenda mno." (Matei, 2014: 93)

Baadaye Mwanaheri alisajiliwa katika shule ya upili ya Tangamano alikosoma na wanafunzi wengine ambao waliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina.

Wahusika wengine walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa wanafunzi ni Umulkheri, Dickson na Mwaliko. Hawa walikuwa watoto wa Mzee Lunga Kiriri Kangata na Bi Naomi. Lunga Kangata alipofutwa kazi kutoka shirika la nafaka la Fanaka, alihamia Msitu wa Mamba. Msitu wa Mamba ulibeba watu kutoka makabila mbalimbali waliokuwa wamefurushwa kutoka maeneo yao asilia. Serikali ilijaribu kusimamisha mizozo hii lakini iliposhindwa, ikaamua kuwahamisha wakaazi hawa hadi Mlima wa Simba. Mali ya Lunga Kiriri Kangata yakaharibiwa pamoja na nyumba zake kubomolewa. Uhalifu huu wa mali pamoja na kuhamishwa kwa Lunga, mkewe na watoto wake waliathirika mno. Mwandishi ananukuu;

> Ameyapoteza maisha yake, amewapoteza ndugu na marafiki zake. Wanawe waliosomea katika shule za kifahari, sasa fidia aliyopewa na serikali haitoshi kuwapeleka katika shule za watu wa kima wastani. (Matei, 2014: 79)

Kutokana na matokeo haya, Bi. Naomi, alimtoroka mmewe na kumsababishia huzuni na hatimaye ugonjwa wa mshtuko wa moyo. Baada ya miaka miwili, Lunga akaaga dunia na

kuwaacha wanawe chini ya ulezi wa kijakazi, Sauna. Kijakazi huyu aliwatorosha Mwaliko na Dick na kuwauza kwa bwana Buda na Bi. Kangara watumiwe katika ulanguzi wa mihadarati. Umulkheri alipowatafuta asiwapate nduguze, aliamua kutorokea jijini ambapo alimpata rafiki yake wa utotoni, Hazina. Rafiki huyu alimpa uhifadhi na kumtafutia mhisani aliyempekeleka kwa mmiliki wa shule ya Upili ya Tangamano. Baadaye tunaelezwa kuwa, Umu alichukuliwa kama mtoto wa kupanga na Mwangeka na mkewe Rachael Apondi.

Aidha, Anatila na Kairu ni wahusika wengine waliokuwa wanafunzi walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Anatila alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili na tunaelezwa kwamba, alikuwa anapenda somo la fasihi, siasa na sheria. Kila mara Anatila na babake  walikuwa na mijadala mirefu mirefu kuhusu masuala yaliyoathiri nchi ya Wahafidhina. Ridhaa anawaza ifuatavyo;

> Uyabisi aliouhisi wakati alipokuwa akifikiria haya sebuleni pake siku ile hausemeki. Alitazama gofu hili kana kwamba analitazama miezi sita iliyopita. Uyabisi huu ndio unaomkumbatia sasa, hata anapojua fika kuwa anamngojea mmoja wa wanawe... Anamwona mwanawe, Tila, akitoka shuleni na kuuweka mkoba wake juu ya meza. (Matei, 2014: 37-38)

Anatila aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo yeye, mamake, Terry, wifi wake, Nyamvula, na Becky waliuawa kwa moto ulioteketeza jumba la babake. Moto huo uliwashwa na vijana waliopinga uteuzi wa Bi. Mwekevu kama kiongozi wakiongozwa na Mzee Kedi.

Kairu pia alikuwa mwanafunzi aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Vita vilipotokea katika nchi ya Wahafidhina, Kairu, mamake na ndugu yake mdogo walitoroka kutoka maeneo yao ili kujinusuru kutoka kwa ghasia zilizokuwa zikikumba maeneo hayo. Wakiwa njiani kuelekea sehemu isiyojulikana, ndugu yake mdogo alishikwa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu. Mtoto huyu alifia mgongoni mwa mamake. Kairu anasema;

> "Wewe hujapitia tuliyopitia. Tulitendwa ya kutendwa. Siku hiyo tulipofurushwa kwetu kama taka tulitanga na njia bila kujua twendako, mama mbele, sisi nyuma, mama amebeba kitindamimba ambaye baadaye alishindwa kukamilisha safari, roho yake changa ikakatikia hapo hapo mgongoni mwa mama, amemezwa na njaa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu…" (Matei, 2014: 91)

Mamake Kairu alitafuta kiserema, akachimba kaburi lenye urefu wa kina kichakani na kukizika kitoto hicho. Baadaye Kairu na mamake waliendelea na safari hadi walipopata wahisani wakawasomba kwa gari kwenda katika kambi za wakimbizi. Vita vilipokwisha, mamake aliyekuwa muuza samaki aliendelea kuathirika kwa ufukara kwa sababu ya mizozo ya umiliki wa maji ya ziwa kuu. Mama huyu alishindwa kumlipia Kairu karo ya shule. Ilibidi azungumze na mwalimu mkuu ili amruhusu kulipa karo kadiri anapopata.

### 2.4 Kuainisha Waathiriwa Kiumri

Erik Erikson (1930), anasema kwamba maisha ya binadamu hupitia hatua mbalimbali katika ukuaji wake. Alitambua hatua saba za ukuaji wa binadamu na akafafanua kuwa kila moja ya hatua hizo huonyeshwa kwa mzozo maalum kwake, azimio zuri ambalo

linasababisha mabadiliko ya hatua mpya. Kila umri wa mwanadamu huwa na changamoto zake, mitazamo yake na hata mielekeo yake kuhusu masuala yanayoiathiri jamii.

### 2.4.1 Wahusika Wazee

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, wahusika wazee walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kikabila ni mzee Uledi, mzee Mangala, mzee Sululu na mzee Zablon. mzee Mangala aliuawa na wapiganaji waliokuwa Wakorosho wilayani Korosho. Mangala alikuwa babake Tom Mangala.  Mwandishi anasema;

> Mwili wa hayati mzee Mangala ulikuwa katika nyumba ya maiti ya Hospitali ya Nduchi. Tom alikuwa amearifiwa akiwa kazini habari za kifo cha babake. Alikuwa mwathiriwa wa mshale uchungu katika vita vya kikabila wilayani Korosho. (Walibora, 2003: 86)

Mwili huo ulihamishwa hadi jiji la Tandika na kisha baadaye ukachukuliwa kijijini mwao Baraki kuzikwa. Mwanaye, Tom, alipomaliza kuuzikwa mwili wa mzee Mangala, naye alishambuliwa na wapiganaji wa kabila la Wakorosho. Mzee Mangala alikuwa Mkanju na kitendo cha Tom kuja kumzika wilayani Korosho kiliwaudhi magenge ya wapiganaji. Wakanju walichukuliwa kama wageni wilayani Korosho kwani walikuwa masetla. Mpiganaji mmoja anasema;

> “Naam. Ati aje amzike babake kwetu Baraki? Wakanju wana haki gani kumzika mtu Baraki. Wao ni magugu sharti wang’olewe, zao linawiri,” (Walibora, 2003: 106)

Kutokana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; fasihi inaposwa ionyeshe ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe, mzee Uledi na mzee Sululu walikuwa marafiki. Uledi aliyekuwa jirani ya Mzee Sululu kijijini Baraki na alikuwa mmoja wa watu walioshambuliwa wilayani Korosho. Siku hiyo ya mashambulizi, Mzee Uledi alikuwa amemtembelea Mzee Sululu kumjulia hali na pia kusikiliza muziki aliokuwa akiuimba kwa gitaa. Uledi aliposhambuliwa, aliokolewa na wahisani, akachukuliwa katika hospitali ya Korosho kupata matibabu. Mzee Uledi anasema;

> "Kipaji changu nacho kikaumia kidogo kwa mshindo wa anguko langu. Ulikuwa usiku wenye kiza totoro. Basi nilijiburura kwa taabu kama kondoo. Kulipoanuka nilikuwa nimefika kando ya barabara. Walipita wahisani walionichukua kwa gari lao na kunileta hapa." (Walibora, 2003. 78)

Tim na Akida walipoenda katika hospitali ya Korosho, walikutana na Uledi akiwa na majeraha. Hata hivyo Mzee Uledi akiwa hospitalini alikuwa amelazwa akiwa mlevi.

Wahusika wengine ambao ni wazee walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kikabila katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003) ni Mzee Sululu na Mzee Zablon. Mzee Sululu aliuawa na Mzee Zablon ambaye alikuwa Mkorosho. Zablon naye baadaye akajitia kitanzi kwa kujutia vitendo vyake na pia kwa kuangamia kwa familia yake katika vita vya kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Haya yanadhihirika katika barua ambayo Mzee Zablon aliiandika na kuiacha nyuma akielezea vitendo vyake.

### 2.4.2 Wahusika wa Umri wa Makamo

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)* baadhi ya wahusika walioathiriwa walikuwa wa umri wa makamo. Wahusika hawa ni Tom Mangala, Mwalimu Alex na Jenelle. Tom Mangala alikuwa mtoto wa kiume wa mzee Mangala na alikuwa mume wa Jenelle. Tom aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kikabila wilayani Korosho. Alipoenda kumzika babake, Mzee Mangala, aliyeuawa katika vita vya kikabila, naye pia alishambuliwa na genge la wapiganaji. Tom alijeruhiwa na genge hili la wapiganaji lilitoka katika jamii ya Wakorosho wakamwacha hali mahututi. Akida anaeleza;

> "Nikapiga moyo konde kuuchomoa mshale uliomkita kidarini. Nikauchomoa taratibu tena kwa makini. Damu ikatiririka tiriri kutoka kwenye kidonda kilichofanyizwa kifuani na mshale ule. Nikamwimua Tom pole pole na kumbeba mgongoni. Katika maisha yangu yote sijawahi kuubeba uzito kama huo. Nilikwenda nikipepesuka, husemi mlevi. Damu ya Tom ikanilowesha shati. Nikamtua karibu na ua. Nikajaribu kila mbinu kuizuia damu yake kuendelea kuvuja." (Walibora, 2003: 107)

Akida alimnusuru Tom kwa kumbeba kwa toroli hadi barabara kuu iendayo jiji kuu la Tandika. Alipata wahisani waliomsafirisha Tom hadi hospitali ya Rufaa ya Tandika. Baadaye Tom Mangala alisafirishwa na mkewe Jenelle kutoka hospitali ya Tandika kwenda nchini Canada kupata matibabu zaidi.

Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, amebaini wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii ambao walikuwa wa umri wa makamo. Wahusika hawa ni pamoja na Ridhaa, Kaizari, Lunga Kangata, Terry, Naomi, Subira, Mwangeka na Lily Nyamvula.

Daktari Ridhaa na aila yake waliathirika mno kutokana na ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Ridhaa aliwapoteza watu wa aila yake akabakia mwanawe wa kiume, Mwangeka, aliyekuwa akidumisha usalama katika mataifa ya ughaibuni. Mkewe, Terry, bintiye, Anatila, mkaza mwanawe, Nyamvula, na mjukuu wake, Becky, waliangamizwa na moto uliowateketeza.

Kaizari na mkewe, Naomi, waliathirika katika ghasia za kisiasa na kijamii. Hii ni baada ya vijana watano mabarobaro kumkata Naomi kwa sime akazirai. Baadaye vijana hawa walifululliza hadi chumbani walimokuwa mabinti wake; Lime na Mwanaheri na kuwabaka. Mkewe alizirai na alipopata fahamu, walisombwa kwenda katika kambi za wakimbizi ambapo mazingira yalikuwa duni. Naye Lunga Kangata ni mhusika wa umri wa makamo ambaye aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Lunga alikuwa mkaazi wa Msitu wa Simba alipokuwa amewekeza katika shughuli za kilimo baada ya kupigwa kalamu kutoka shirika la nafaka alikokuwa akifanya kazi. Mwandishi anasema;

> Kundi la kwanza la 'wakimbizi' lilipofika hapa-lile la akina Ridhaa, Kaizari na Kangata-hamkuwa na tofauti kubwa. Jamaa hawa walikuwa wamelazimika kuja hapa. Walikuwa wahitaji, wakapigania vyakula vya misaada, wakala majani mwitu na vingine pamoja. (Matei, 2014: 74-75)

Hata hivyo uhasama ulienea katika msitu wa Mamba na Lunga akahamishwa hadi mlima wa Simba. Katika harakati za kuhamishwa, Lunga aliyapoteza mali yake yakiwemo majumba, mazao shambani na mivugo. Hali hii ilimsababishia kihoro kilichomsababishia ugonjwa wa moyo ambao ulimwangamiza.

### 2.4.3 Wahusika Waliokuwa Vijana

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, Akida, Tim na Tamari ni wahusika vijana walioathirika kufuatia ghasia za kisiasa na kijamii. Akida Sululu aliathiriwa na ubaguzi wa kimbari ambapo babake Mzee Sululu aliuawa katika vita hivyo. Aidha, Akida alifanyiwa madharau kwa misingi ya kabila lake na Samson Tungu aliyekuwa Mkorosho.Vilevile, kufuatia vita vya kisiasa na kijamii nchini Kiwachema, Akida hakuweza kuendelea na masomo yake ya shule upili. Baada ya kuchelewa kuingia shuleni, ufadhili wake ulibatilishwa na kupewa mwanafunzi mwingine. Akida akaanza kufanya kazi za sulubu. Tamari anamtukana Akida kwa misingi ya kikabila. Tamari anasema;

> " Nenda huko bwege wewe," alinitupia tusi.
>
> "Mwanzo unafanya nini katika nyumba ya kakaangu?" (Walibora, 2003: 63)

Tim Mapisi na Tamari Mapisi ni wahusika wengine vijana walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Tamari aliathirika kwa kunusurika kubakwa na genge la wapiganaji. Alitorokea vichakani akashuhudia mauaji mengi ya watu. Alitembea mwendo mrefu njiani na kulala vichakani kabla ya kupata mhisani ambaye alimsafirisha kwa gari hadi jijini Tandika alikoishi nduguye. Tim Mapisi naye aliathirika na vita hivi pale ambapo alimhifadhi rafiki yake wa asili ya Kikanju. Tim alikuwa Mkorosho na Wakorosho na Wakanju walikuwa wanazozana na kupigana wilayani Korosho. Mjombake Tim, Samson Tungu alipogundua kwamba Tim anamhifadhi Mkanju chumbani mwake, alimfuta kazi mara moja. Tim anaeleza;

> "Basi ameniuliza jana nilikuwa wapi. Nikamwambia nilienda kwa sherehe ya kuzawadiwa kwa rafiki yangu. Akaniuliza, 'rafiki yako kabila gani?' N'kamjibu Mkanju. Basi wacha zimpande za kwao. Eeh! Unafanya urafiki na Wakanju huku, unaelewa wanatuua sisi Wakorosho. Unasaliti kabila lako? Unamweka Mkanju nyumbani kwako Shauri Moyo!'…Hebu toka hapa. Nimekufuta kazi!" (Walibora, 2003: 65)

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014),* wahusika walioathirika ambao ni vijana ni pamoja na Anatila, Umulkheri, Kairu, Dickson, Mwaliko, Lime na Mwanaheri. Anatila alikuwa kijana wa kike wa Daktari Ridhaa aliyeathirika kwa kuuawa na waandamanaji pamoja na mamake na wifi wake. Familia ya Daktari Ridhaa iliangamizwa na Mzee Kedi aliyeongoza mapigano hayo. Wapiganaji hawa walikuwa wanapinga uteuzi wa Bi. Mwekevu Tendakazi. Lime na Mwanaheri nao waliathirika kwa kubakwa na mabarobaro watano ambao walishambulia aila ya Mzee Kaizari na Subira. Baadaye walipelekwa katika kambi za wakimbizi. Kaizari anasema;

> Sijui ilikuwaje, lakini baada ya dakika chache nilijipata nje ya nyumba yangu, wanangu wawili wamezirai ubavuni mwangu, mke wangu anatoka damu; mchirizi baada ya mwingine. (Matei, 2014: 25-26)

Kaizari anaeleza kwamba mabinti wake walibakwa na vijana hawa na kuwaathiri mno kisaokolojia. Walipopelekwa katika kambi za wakimbizi, walikumbana na matatizo tele. Kulikuwa na ukosefu wa chakula, maji safi, huduma za kimsingi kama vile misala na mogonjwa yaliwaathiri vilevile. Baadhi ya wakimbizi waliaga dunia kwa magonjwa.

Umulkheri, Dickson na Mwaliko walikuwa wahusika vijana wa Mzee Lunga Kangata na Naomi. Baba yao Lunga Kangata, aliathiriwa na ghasia za kisiasa ambapo mashamba yake yaliyokuwa yakimletea utajiri mwingi katika Msitu wa Mamba yalinyakuliwa na serikali. Hii ni baada ya uhasama wa kijamii kuzuka miongoni mwa wakaazi wa Msitu wa Simba. Mizozo ilipozidi, uongozi uliwahamisha Lunga na wakazi wengine kwenda Mlima wa Simba. Mali aliyokuwa ameyachuma Lunga yaliharibiwa huku nyumba zikibomolewa. Lunga alikumbwa na ufukara katika mazingira haya mageni. Kutokana na upweke aliopata, Lunga alishikwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na baadaye akafariki.

Kairu ni mhusika mwingine kijana ambaye aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Yeye pamoja na mamake na ndugu zake walifurushwa kutoka sehemu walikoishi, wakapelekwa katika kambi za wakimbizi. Walipokuwa wakitoroka, nduguye mdogo alishikwa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu akafia mgongoni mwa mamake. Mamake alitafuta kiserema, akachimba kaburi kichakani, akamzika kisha wakaendelea na safari ya kutoroka. Vita vilipotamatika, walirejeshwa kwao ambapo kulitokea na mizozo ya umiliki wa maji na ardhi ya ziwa kuu. Kairu anasema;

> Kwa mtu maskini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzishia biashara nyingine, maisha yamekuwa magumu zaidi. Hata karo yangu imebidi amlilie mwalimu mkuu amruhusu alipe kidogokidogo… (Matei, 2014: 93)

### 2.4.4 Wahusika Waliokuwa Watoto

Ondieki (2015), anafafanua kwamba watoto hukabiliwa na matatizo mengi kama vile kunyimwa uhuru wa kujieleza, kutusiwa, kutosomeshwa, kupokonywa urithi,

kudhulumiwa kimapenzi na kadhalika. Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, mjukuu wa Daktari Ridhaa, Becky, aliteketezwa motoni pamoja na mamake na nyanyake na wapiganaji wa kivita. Becky alikuwa mtoto wa Lily Nyamvula na Mwangeka ambaye alichomwa pamoja na mamake katika kasri la babake. Kutokana na moto huo uliowashwa na genge la wapiganaji, Becky aliaga dunia. Mwandishi anaeleza;

> Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake, Becky. Anawaona wote mbele ya macho yake yaliyojaa mavune. (Matei 2014:5)

Aidha, Ridhaa akiwa mtoto, alifanyiwa ubaguzi wa kimbari na wanafunzi wenzake shuleni. Babake, Mzee Mwimo Msubili, alikuwa amemhamisha mamake Ridhaa kuja kwa Msitu wa Heri kwa kuwa aila yake ilikuwa imebanuka na ardhi haingetosheleza mahitaji yao. Ridhaa akiwa shuleni katika eneo hilo, wanafunzi wenzake walimfanyia ubaguzi wa kimbari. Mwanafunzi mmoja alimwambia;

> “Wewe ni mfuata mvua,” Mwanafunzi Yule akamwambia, “Hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda mitihani. ” (Matei, 2014: 10)

Kutokana na usemi huu wa mwanafunzi mwenzake, Ridhaa alikimbia nyumbani na kumwambia mamake. Mamake Ridhaa alienda shuleni siku iliyofuata na kuzungumza na mwalimu na hatimaye Ridhaa akaendelea na masomo yake mpaka akahitimu.

Nduguye Kairu naye aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Kairu na mamake walikuwa wakitoroka mashambulizi yaliyotokea nchini mwao. Wakiwa katika hali hii, mtoto huyo alifariki akiwa mgongoni mwa mamake kutokana na ugonjwa wa mabafu. Kairu anasema;

> “Siku hiyo tulipofurushwa kwetu kama taka tulitanga na njia bila kujua tuendako, mama mbele, sisi nyuma, mama amebeba kitindamimba ambaye baadaye alishindwa kukamilisha safari; roho yake changa ikakatika hapo hapo mgongoni mwa mama, amemezwa na njaa na ugonjwa wa udhaifu wa mapafu.” (Matei, 2014: 91)

Mamake Kairu alitafuta kiserema, akachimba kaburi na kumzika mtoto huyo. Baadaye waliendelea na safari ya kutoroka kwenda mahali salama. Walichukuliwa na wahisani kwenda katika kambi za wakimbizi kupata hifadhi dhidi ya mashambulizi.

## 2.5 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo chaUongozi

Masango (2002), anasema kwamba kiongozi ni mtu anayewaathiri watu binafsi au vikundi vya watu katika jamii. Baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kikabila walikuwa viongozi.

### 2.5.1 Viongozi wa Kisiasa

Kisurulia (2020) anaeleza kwamba viongozi huchangia pakubwa ghasia za kisiasa na kijamii barani Afrika. Baadhi ya viongozi hueneza uchochezi wa kijamii na kisiasa huzua uhasama, ghasia, vita na mauaji miongoni mwa makabila. Naye Masango (2002), anasema kuwa Viongozi huwa na mchango mkubwa kunapotokea ghasia za kisiasa na kijamii katika jamii.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)* baadhi ya wahusika walichochea ghasia za kisiasa ambapo wengine wao waliathirika na ghasia hizo. Mmojawapo wa viongozi aliyechochea ghasia za kisiasa na kijamii na baadaye akaathirika ni Johnstone Mabende. Kiongozi huyu alikuwa mbunge wa eneo la Korosho aliyewachochea Wakorosho kuwashambulia Wakanju wilayani Korosho. Mabende anawachochea wakorosho katika soko la Baraki. Mabende anasema;

> "Hatutaki 'madoadoa' hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju." (Walibora, 2003: 2)

Wanauhalisia wanaamini kuwa, sanaa inafaa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe. Hii inadhihirika riwayani ambapo viongozi wa kisiasa wanajihusisha katika kuchochea ghasia za kisiasa waliyani Korosho. Hali hii ni sawia kama anavyosema Gachukia (2003), kuwa vyama vya kisiasa nchini kenya, huteuaa viongozi wa vyama na nyadhifa zingine za uongozi kwa misingi ya kikabila. Uongozi wa aina hii hujaa dhuluma na ukatili kwa watawaliwa.

Ilisemekana kuwa Johnstone Mabende pamoja na wakereketwa wengine walifadhili mapigano wilayani Korosho. Baadaye, serikali ya Kiwachema ilimteua Mabende kama waziri wa usalama wa ndani. Uteuzi huu uliwafanya watu wengi kuhuzunika. Johnson Muyaka alilalamika kwamba muuaji amepewa wadhfa wa kulinda raia. Baadaye iliripotiwa kuwa Johnstone Mabende amepigwa risasi na kuuawa na Johnson Muyaka aliyekuwa afukani.

### 2.5.2 Viongozi wa Kidini

Njenga (2021), anasema kwamba viongozi waovu hubagua watawaliwa wao kwa misingi ya kabila, dini na jinsia. Hii ni ishara mojawapo ya uongozi ulio katili. Katika riwaya ya *Kufa kuzikana (2003),*mhubiri James Sanya aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kikabila wilayani Korosho. Makabila ya Wakanju na Wakorosho yalikuwa na mizozo ya kisiasa ambapo watu wengi waliathirika kwa kuuawa au kufurushwa kutoka maeneo yao na mali kuharibiwa. Athari za ghasia zilienea hadi kanisani na kuwaathiri waumini, viongozi wao wakiathirika vilevile. Mhubiri, James Sanya alifurushwa kanisani alipokuwa akihubiri kwa misingi ya kisiasa na kijamii. Mwandishi anaeleza kuwa, maafisa wapolisi walitumwa katika baadhi ya makanisa kudumisha usalama. Kasisi John anasema;

> "Kwa nini mnaruhusu ukabila kuingia kanisani. Kisa cha kumkataa mhubiri James Sanya kwa sababu ya ukabila kimetia doa kanisa. Eeh! Fikiria askari kuja kanisani kuzima ghasia miongoni mwa waumini! Si jambo la aibu hilo?..." (Walibora 2003: 121)

## 2.6 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Ajira na Taaluma

Wanjiru (2021) anasema kwamba, haitoshi tu kushiriki uchaguzi lakini ni muhimu pia wananchi kufuatilia vitendo vya viongozi wanaowachagua na utendakazi wao. Baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii walikuwa waajiriwa na wataalamu.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, mwalimu Alex alikuwa mmoja wa wataalamu aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Mwalimu Alex alikuwa Mkorosho aliyekuwa akifundisha katika shule ya msingi ya Baraki. Yeye ndiye

aliyewafundisha Tim, Akida na Tamari katika masomo ya msingi. Mwalimu Alex alipinga hulka ya viongozi kuchochea makabila wilayani Korosho. Utafiti huu ulibaini kuwa Mwalimu Alex aliuawa na Wakorosho ili kuwe na kisingizio cha kuwashambulia Wakanju walioishi wilayani Korosho. Mwili wake ulipatikana karibu na Mto Kibisi kijijini Baraki. Akida anaeleza;

> Wanawake hao walituelekeza hadi kwenye kichaka kilichokuwa katika kingo za Mto Kibisi. Hapo ndipo nilipoiona maiti ya mwalimu wangu mpendwa Alex. Ilikuwa imekatwakatwa vibaya. (Walibora, 2003: 4-5)

Tom naye alikuwa msomi aliyesomea shahada ya uzamili nchini Marekani. Alipomaliza masomo yake alirejea nchini Kiwachema na mke wa kizungu kwa jina Jenelle. Alipata kazi katika shirika moja lisilo la kiserikali liitwalo Anken. Tom aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo babake, Mzee Mangala, aliyekuwa Mkanju aliuawa na Wakorosho wilayani Korosho. Alipoenda kumzika babake, Mzee Mangala, wilayani Korosho, Tom alishambuliwa na genge la wapiganaji. Mwandishi anasema;

> Tom alikuwa msomi. Alikwenda Marekani kusoma akahitimu shahada ya uzamili…Tom alikuwa anafanya kazi na shirika moja lisilo la serikali liitwalo Anken. (Walibora, 2003: 80-81)

Tom alipoenda kumzika kijijini Baraki, alishambuliwa na Wakorosho akabaki hali mahututi. Aliokolewa na rafikiye, Akida, ambaye alimsafirisha katika gari la mhisani mmoja hadi hospitali ya Rufaa ya Tandika. Baadaye mkewe, Jenelle, akamsafirisha Tom kwenda nchini Canada kupata matibabu spesheli. Akida anasema;

> Nilimkuta Tom kalala chini ya mwembe. Hafurukuti. Hasemi ana tofauti na magogo ya mkalitusi yaliyolala karibu naye. Kanyooka pale chini, hatikisiki licha ya matone ya mvua yaliyomrowanisha. Nikamkaribia karibu. Nikashtuka hadi ya kushtuka. Mshale ulikuwa umemkita kifuani, chembe kizima kimezama zi ndani yake. (Walibora, 2003: 105)

Tom aliokolewa na Akida ambaye alimbeba kwa torori hadi barabara kuu na kupelekwa hospitali ya Tandika na baadaye mkewe akamhamisha kwenda nchini Canada kupata matibabu zaidi.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya wahusika waliokuwa wanataaluma na waajiriwa waliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Ridhaa ni mhusika mwanataaluma aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Ridhaa alikuwa amepaa katika anga ya elimu kupitia vyuo mbalimbali hadi akahitimu kama daktari baada ya kumaliza masomo yake ya uzamivu. Alisomea taaluma ya matibabu katika kitengo cha upasuaji. Alifanya kazi na hata kuwa mkurugenzi aliyesimamia mashirika ya huduma za afya. Mwandishi ananukuu;

> Ridhaa alipea kwenye anga ya elimu, akabisha milango ya vyuo, akafikia kilelecha cha ufanisi alipohitimu kama daktari. Utendakazi wa Ridhaa ulimletea mbivu, akawa mkurugenzi wa mashirika mbalimbali yanayohusiana na huduma za kiafya. (Matei, 2014: 11)

Ridhaa aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii wakati mkewe Bi. Terry, bintiye Anatila na mjukuu wake, Becky, waliuawa katika ghasia hizo. Baadaye Ridhaa alijenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya ambapo aliwahudumia wagonjwa. Aliwaajiri Bwana Kaizari kama afisa wa matibabu na Selume kama muuguzi mkuu huku naye Ridhaa akawa mkurugenzi wa kituo hicho.

Mwangeka na Kaizari nao walikuwa wanataaluma walioathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*. Mwangeka alikuwa amesomea taaluma ya uhandisi. Baada ya kuhitimu shahada, alijiunga na kikosi cha usalama cha wanamaji ambapo alipandishwa vyeo hadi alipohamia nchi za ughaibuni kudumisha hali ya usalama. Mwandishi ananukuu;

> Baada ya kipigo hiki cha babake, Mwangeka aliapa kuwajibika zaidi. Aliinamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. (Matei, 2014: 61)

Mwangeka aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo mkewe Lily Nyamvula na mwanawe, Becky, waliteketezwa motoni katika kasri la babake, wakaaga dunia.

Bwana Kaizari ni mwajiriwa na mtaalamu aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamii. Kaizari alikuwa amesomea taaluma ya matibabu. Kaizari aliathirika ambapo yeye pamoja na mkewe Bi. Subira walipigwa kwa sime na waandamanaji. Baadaye, mabinti wake; Mwanaheri na Lime, walibakwa na vijana walioandama ambao waliingia katika chumba chao. Mzee Kaizari na mkewe, Subira, hawakuweza kuwasaidia.Baadaye, aila ya Kaizari ilisombwa kwenda kambi za wakimbizi. Vita vilipokwisha, walirudishwa katika Msitu wa Mamba. Hata hivyo sehemu hii nayo ilikumbwa na misukosuko ya kikabila na uongozi

mpya ukaamua kuwahamisha kwenda Mlima wa Simba. Ridhaa alipojenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya, alimuajiri Kaizari kama afisa wa matibabu. Mwandishi anasema;

> Nafasi za kazi zilipotangazwa, Selume na Kaizari waliomba kazi, Selume akaajiriwa kama muuguzi mkuu, naye Kaizari kama afisa wa matibabu. (Matei, 2014: 141)

## 2.7 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Ndoa

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, baadhi ya wahusika walioathirika katika nchi ya Kiwachema walikuwa wanandoa. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia, wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii. Ndoa ndiyo kiungo asilia cha ujenzi wa jamii. Nock (2009), anasema kuwa ndoa ni muhimu kwani ndiyo chanzo cha familia, umoja na ukamilivu. Anadai kuwa, ndoa husaidia uzazi na huleta upendo miongoni mwa wanadamu.

Wahusika wanandoa tuliowabaini ni pamoja na Mzee Sululu, Mzee Zablon, Terry na Mzee Uledi ambao waliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii.

Kutokana na nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe, ilibainika kuwa kulikuwa na ndoa kati ya mzee Sululu na mkewe Johani. Johan alikuwa amefariki katika ajali ya barabara katika vilima vya Tungule wilayani Korosho. Johan alipofariki, Mzee Sululu alisalia na mwanawe wa kipekee ambaye ni Akida Sululu. Akida anawaza;

> Tungule! Niliwaza. Halikuwa jina geni kwangu. Tungule ni jina linalonitonesha kidonda. Takribani miaka kumi iliyopita mamangu mzazi aliangamia katika ajali ya barabarani katika vilima hivi. (Walibora, 2003:1)

Mzee Sululu alikuwa Mkanju aliyeishi wilayani Korosho na aliathirika na ghasia za kisiasa na kijamii kwa kuuawa na Mzee Zablon Mapisi aliyekuwa Mkorosho.

Mzee Zablon na mkewe walijaliwa na watoto ambao ni Tim na Tamari na ndugu wengine. Mwandishi anasema kuwa Mzee Zablon alijutia kitendo cha mkewe kuuawa pamoja na watoto wake wengine. Zablon alikuwa mmoja wa genge lililovamia na kuwaua Wakanju yakiwemo mauaji ya Mzee Sululu. Zablon alikumbwa na majuto kutokana na mauaji ya aila yake na pia mauaji ya Mzee Sululu; akajitia kitanzi. Kabla ya kujitia kitanzi, Zablon aliandika waraka akauacha chumbani. Barua hiyo inasema;

> Kuuwawa kikatili kwa muke na wadodo wango wasio wa hattia kumeniattua mooyo. Mie nimewaua Wakanju wengi vittani. Nilikuwa mstari wa mbele katika kikosi cha Wakorosho. Ila sasa nashindwa kuhimili majutto ya kumuuwa ndugu Sululu, mutu asie hattia. Samaani Sululu. (Walibora, 2003: 198)

Mzee Zablon anakiri kuwa alikuwa muuaji wa Wakanju kutokana na waraka aliouacha nyuma kabla hajajitia kitanzi.

Tom Mangala naye alikuwa mwanandoa aliyeathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Tom alikuwa amemwoa mke kwa jina Jenelle. Tom na Jenelle walikutana katika chuo kikuu nchini Marekani walipokuwa wakisoma, wakachumbiana na baadaye wakaoana. Waliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii nchini Kiwachema. Akida anasema;

> Nilitamani ningalikuwa yeye , mwingi wa mali na elimu pamoja na mke mzungu. (Walibora, 2003: 84)

Mzee Uledi naye alikuwa mwaathiriwa wa gasia za kisiasa na kijamii aliyekuwa mwanandoa. Uledi alikuwa jirani ya Sululu katika kijiji cha Baraki aliyeshambuliwa na wapiganaji wa kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Mzee Uledi alilazwa katika hospitali ya Rufaa ya Tandika. Uledi alikuwa na wake watatu na watoto wanane ambapo baadhi waliangamia katika ghasia za kisiasa na kijamii huku wengine wakitorokea jijini Tandika akiwemo Regina. Mzee Uledi anasema;

> "Kwangu marehemu wanane, wake watatu na watoto watano. Wengine wako jijini wanahangaika tu. Wengine wametawanyika sijui waliko. Na Regine afadhali nisingejua aliko na afanyalo…" (Walibora, 2003: 220)

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014),* wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa wanandoa ni Ridhaa, Lunga Kangata, Kaizari, Mwangeka, Naomi, Subira, Lily Nyamvula na Terry.

Ridhaa na Terry walikuwa wanandoa na ni wazazi wa Anatila, Mwangeka na Dede. Familia hii iliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii zilizozuka katika nchi ya Wahafidhina. Ghasia zilizuka baada ya Mwekevu Tendakazi kuteuliwa kama kiongozi wa nchi ya Wahafidhina.Terry, Anatila na Becky waliangamizwa na moto ulioteketeza nyumba yake Ridhaa. Mwandishi anasema;

> Laiti Ridhaa angalijua kwamba hii ndiyo iliyokuwa mara yake ya mwisho kuzungumza na mkewe. (Matei, 2014: 2)

Mzee Kedi ndiye aliyeteketeza jamaa hii kwa sababu ya tofauti za kisiasa na kijamii. Kedi alikuwa jirani wa Daktari Ridhaa katika Msitu wa Heri.

Wanandoa wengine walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ni Mwangeka na mkewe Lily Nyamvula waliokuwa wazazi wa Becky. Familia hii iliathirika ambapo Lily Nyamvula aliteketezwa motoni pamoja na mwanawe, Becky, mama mkwe wake, Terry, na wifi wake Anatila. Mwangeka alikuwa ughaibuni akidumisha usalama haya yakitokea. Mwangeka anasema;

> "Kama ningeusikiliza ushauri wa tausi wangu labda ningeweza kuiokoa aila hii…labda mke wangu angekufa kifo cha faraja…labda ningemwona maskini mwanangu ambaye nimewahi kumwona kwenye picha ambazo tausi wangu alinitumia." Aliwaza Mwangeka. (Matei, 2014: 62)

Kaizari na mkewe Subira ni wahusika wengine walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa wanandoa. Aila hii iliathirika wakati vijana mabarobaro watano walipoivamia na kuwashambulia. Walimchapa Subira kwa sime akazirai kisha wakawavamia mabinti wao, Mwanaheri na Lime, na kuwabaka machoni mwa wazazi wao. Kaizari anasema;

> "…matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri… Sina hata tambara duni la kuwafunika….Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu, Subira. (Matei, 2003: 15-16)

Lunga Kangata na mkewe Naomi alihamia Msitu wa Mamba baada ya kufutwa kazi kutoka shirika la nafaka la Fanaka. Katika Msitu huu kulitokea mizozo ya kitabaka na kijamii baina ya watu walioselelea humo. Watu hawa walikuwa wa asili mbalimbali. Serikali

ilihofia hali hii ikaanza kampeni za kuwahamasisha wananchi umuhimu wa kuishi kwa maelewano licha ya tofauti za kimbari. Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya awamu ya kwanza vilianza. Maafisa wa kulinda usalama walitumwa kukabiliana na mgogoro huo. Hali ilipokuwa mbaya zaidi, serikali iliwafurusha wakaazi hawa hadi Mlima wa Mamba. Familia ya Lunga Kangata ikasambaratika. Mwandishi anasema;

> Mkewe Lunga, Naomi, naye ni miongoni mwa wale wake ambao hata wanapoolewa hawasahau uhusiano wao na nasaba zao. Hawatulii kuyapalilia maisha ya unyumba. (Matei, 2014: 79)

## 2.8 Kuainisha Waathiriwa kwa Kigezo cha Matatizo ya Kiafya.

Mutugu (2019), akiwanukuu Mackenzie (2014), Felman (2003) na Prendergast (2001), anaeleza kuwa watu wenye matatizo ya kiakili hutofautiana na wanajamii wengine kwa mtazamo wa kimawazo. Watu hawa huonyesha mielekeo na hulka zisizozingatia matarajio, mila, desturi na mitazamo ya jamii.

Kutokana na nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, baadhi ya waathiriwa walikuwa na matatizo ya kiakili. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), mwalimu Alex ni mwathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii aliyekuwa na matatizo ya kiafya. Licha ya kuwa na matatizo ya kiakili, mwalimu huyu alitambua kwamba kulikuwa na ghasia za kijamii nchini Kiwachema. Alikuwa na uelewa kuhusu wachochezi wa chuki za kijamii kati ya Wakorosho na Wakanju. Kila mara mwalimu Alex alimkashfu mbunge wa Korosho, Mheshimiwa Mabende, aliyekuwa akiwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju. Mhusika huyu alipatwa na matatizo kiakili. Akida anasema;

> Nilihuzunika Mwalimu Alex aliporukwa na akili. Nilimwona akihutubia vichaka na kuvikumbusha umuhimu wa kusoma. (Walibora, 2003: 2)

Mwalimu Alex alimkabili Mbunge wa Korosho na kukashfu vitendo vyake vya uchochezi baina ya Wakanju na Wakorosho. Mheshimiwa Mabende alitoa hotuba katika mkutano wa hadhara katika soko la Baraki na kuwaita Wakanju 'madoadoa' ambao walihitajika kuondolewa wilayani Korosho. Mwalimu Alex aliyekuwa katika hadhara hiyo alimkemea mheshimiwa Mabende. Mwalimu Alex alisema;

> "Mheshimiwa sasa unaanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. Wakanju ni ndugu zetu ati. Watu wa fikra kama wewe ndio maharabu wa nchi." (Walibora 2003:2)

Mwalimu Alex alikuwa Mkorosho lakini aliwatetea Wakanju ambao hawakuwa wa kabila lake. Baadaye Mwalimu Alex aliuawa na Wakorosho wenzake ili kuhalalisha kitendo cha Wakorosho kuwashambulia Wakanju. Aliuawa na mwili wake ukatupwa kando ya Mto Kibisi.

## 2.9 Hitimisho

Sura hii iliwabainisha wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003)*. Tuliwaainisha wahusika hawa kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile kitabaka, kijinsia, kielimu na kiumri. Aidha, kuna wale waliotambuliwa kwa kigezo cha taaluma zao, uongozi, hadhi ya ndoa na wenye matatizo ya kiafya. Sura inayofuata inashughulikia usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule.

# SURA YA TATU

## USAWIRI WA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LA HERI* (2014) NA *KUFA KUZIKANA* (2003)

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Hill (1977), anasema kwamba usawiri mwafaka wa wahusika unahitaji ubunifu mkubwa ili kuwawezesha wahusika hao kuonyesha hali halisi zinazojitokeza katika mazingira ya jamii. Ingawa riwaya hizi zina wahusika wengi, tuliangazia wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii ili kutosheleza madhumuni ya utafiti wetu. Kusawiri wahusika ni kutoa picha halisi ya wahusika hao; sifa zao, hali yao ya maisha, namna walivyoathirika na ghasia za kisiasa na kijamii. Katika kusawiri wahusika, tulichunguza wanachosema kujihusu, wahusika wengine wanavyosema kuwahusu, maelezo ya mwandishi kuwahusu, hisia zao na uzungumzi nafsi wao na pia matendo yao.

### 3.1 Wahusika Waliosawiriwa Kama Watu Waliokata Tamaa

Soren Kierkgaard (1843), anasema kwamba kukata tamaa ni kuwa na fadhaa, mashaka, pekecho na uchovu na jinsi hali hizi zinavyoathiri maisha ya mtu. Hali hizi hutokana na mateso, matatizo, machungu na vifo vya wapendwa.

Waandishi wa riwaya teule, wamewasawiri baadhi ya wahusika wa ghasia za kisiasa na kijamii kama watu waliokata tamaa kutokana na ghasia za kisiasa na kijamii zilizoyakumba

mataifa ya Kiwachema na Wahafidhina. Hali hii inatokana na madhila waliyopitia wakiwa katika hali ya migongano ya kisiasa na kijamii.

Kutokana nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, mwandishi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003),* ametambua baadhi ya wahusika ambao wamekata tamaa. Makabila ya Wakorosho na Wakanju yalipigana na kusababisha maafa ya watu na uharibifu wa mali pamoja na kufurushwa kwa watu kutoka maeneo yao. Akida Sululu, alipopata habari kwamba babake alikuwa ameuawa katika ghasia za kisiasa, alihuzunika mno. Akida alikuwa amemwacha babake, mzee Sululu, nyumbani kwao Baraki na kuzuru jiji la Tandika kwenda kuzawadiwa na waziri wa elimu. Alikuwa ameupasi vyema mtihani wake na akawa miongoni mwa wanafunzi watatu bora nchini Kiwachema. Alipokuwa jijini, vita vilizuka wilayani Korosho na akafahamishwa kwamba babake alikuwa miongoni mwa watu waliouawa. Akida alipashwa habari za kifo cha babake na rafikiye, Tim. Habari hizi zilimtamausha Akida. Akida anasema;

> Nilisimama tulii, nimeghumiwa, ungedhani nimegeuka nguzo ya chumvi kama mke wa Loti. Wazo la kumwona baba kanyooka, maiti kwenye nyumba ya maiti halikuniingia. Haiwezekani. Haiyamkiniki. Afe kwa nini na sasa ndio wakati wa kutafahari kwa kuchapishwa diwani yake? Afeje na ndoto yake ndio mwanzo inatimia? Baba hajafa. Nilipiga usiahi ghafla na kugaragara sakafuni… (Walibora, 2003: 69)

Akida alijawa na majonzi kwa sababu mamake vilevile alikuwa ameaga dunia katika ajali ya barabara huku ndugu zake nao wakifariki kutokana na magonjwa.

Tom Mangala ni mwathiriwa mwingine wa ghasia za kisiasa na kijamii aliyesawiriwa kama mtu aliyekata tamaa. Kukata tamaa kwake kulitokana na kuuawa kwa babake, Mzee Mangala, na genge la wapiganaji wa kisiasa na kikabila. Tom Mangala alikuwa akiishi jijini Tandika na mkewe, Jenelle. Mzee Mangala aliuawa katika ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea wilayani Korosho. Inasemekana kuwa Mzee Mangala alikuwa Mkanju na walishambuliwa na wakorosho.

Tom alipata habari za kifo cha babake, Mzee Mangala. Mwili wake ulikuwa umehifadhiwa katika nyumba ya maiti katika hospitali ya wilaya ya Nduchi. Tom alisaidiwa na Akida na Tim kuuhamisha mwili huo kutoka Nduchi hadi hospitali ya Tandika. Alipokuwa akiuzika mwili wa babake alionekana kuwa na huzuni. Kaburi lilipochimbwa, Tom alisimama kimya kitambo, akiwa ametabaradi na kuinamisha uso wake kulitazama jeneza lililobeba mwili wa babake, Mzee Mangala. Tom alitoa taabini ndefu ya kumwomboleza babake kisha akaelekea kwenye gari akitiririkwa machozi kwa huzuni.Tom anaomboleza;

> “Ulikuwa baba mcheshi mwenye usafi wa nia. Ulijisabilia kwangu, ukajipa umaskini ili nipate elimu na umekufa kabla sijakulipa fadhila zako. Wema wako usio na mfano pengine utatupwa kwenye jaa la sahau na kizazi hiki maaluni…nimekuja kukuzika! Buriani. (Walibora, 2003: 99)

Maelezo haya ya Tom Mangala juu ya kaburi la babake yanadhihirisha kwamba kifo hiki cha babake kilimfanya akakata tamaa. Walipokuwa wakipanga kurejea jijini baada ya mazishi hayo, genge la wapiganaji wakiongozwa na askari lilimshambulia Tom na kumwacha hali mahututi. Walimshambulia kwa kuja kumzika babake, Mzee Mangala,

wilayani Korosho. Akida ndiye aliyemwauni Tom kwa kumburura kwa toroli hadi kichakani na baadaye kumchukua jijini Tandika.

Kutokana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; msanii atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, mazingira aliyojipata Mzee Zablon yalimfanya kukata tamaa. Mzee Zablon alikuwa ameshiriki mauaji ya Wakanju katika ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Familia yake nayo iliathiriwa na ghasia hizi za kijamii na kisiasa. Mkewe na baadhi ya wanawe waliuawa katika vita hivyo wakabakia Tim na Tamari waliokuwa wakiishi jijini Tandika. Kutokana na maafa haya pamoja na kushiriki kwake katika mauaji ya halaiki ya watu, Zablon alishikwa na msongo wa mawazo. Aliposhindwa kuvumilia hali hii ya maisha, Zablon alijitia kitanzi. Tim anasema;

> “Baba aliporudi kwa mjomba akawa anajifungia ndanindani hatangamani na yeyote. Ipo siku hakutoka kabisa. Wajua tena aila ya mjomba wanavyomvalia mtu miwani na kujipurukusha. Hawakushughulika. Ndipo mjomba mwenyewe alipokwenda chumbani. Akamkuta baba ananing’inia darini kwa kamba ya katani shingoni."  (Walibora, 2003: 197)

Wanauhalisia wanaamini kuwa, wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii. Kulipotokea mauaji ya Wagala mwaka wa 1984 nchini Kenya, watu wengi waliuawa huku wengine wakabaki wametamauka. Panagloti, Gooding na Tarrier (2012), wanasema kuwa mtu anapokata tamaa hupungukiwa na matumaini maishani na huathirika namna anavyojichukulia yeye binafsi na anavyouchukulia ulimwengu. Katika Riwaya ya *Chozi la Heri (2014)* kuna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kikabila waliosawiriwa kama wakata tamaa. Ridhaa ni mmojawapo wa wahusika aliyekata tamaa kutokana na ghasia za kisiasa

na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Ridhaa alikumbwa na misiba kadhaa ambapo wa kwanza ni ule wa aila yake kuangamizwa na vijana waliokuwa wakipigana wakipinga matokeo ya uchaguzi katika taifa la Wahafidhina. Katika vita hivyo, mkewe, Bi. Terry, mkaza mwanawe, Lily Nyamvula, bintiye, Anatila na mjukuu wake, Becky, waliangamizwa motoni wakati jumba lake lilipoteketezwa kwa moto na genge la wapiganaji. Ridhaa alikuwa hospitalini akimhudumia mgonjwa aliyekuwa ameathiriwa na vita vya kisiasa na kikabila. Ridhaa aliporejea kwake, alizirahi kutokana na kihoro kilichomshika, akatamauka. Mwandishi anaeleza;

> Ridhaa alisimama kwa maumivu makali, mikono kairudisha nyuma ya mgongo wake uliopinda kwa uchungu. Macho yake yaliyotanda ukungu alikuwa kayatunga juu angani.. (Matei, 2014: 1)

Baada ya familia ya Ridhaa kuangamia, alibaki kukosa mapenzi na akaishi maisha ya ujane akiwa na mwanawe wa pekee, Mwangeka. Majanga mengine yaliyomkata tamaa Daktari Ridhaa ni uharibifu wa mali yake. Jumba lake la kwanza lililokuwa katika mtaa wa Zari lilibomolewa kwa kile kilichosemekana kwamba lilikuwa limejengwa katika sehemu iliyotengewa ujenzi wa Bypass. Aidha, jumba lingine alilopangisha watu lilichomeka kwa kile kilichosemekana kuwa hitilafu za nguvu za umeme. Ridhaa anasema;

> “Mwanangu,” alisema Ridhaa, “Maisha yalitubadilikia mara tu baada ya kuondoka kwako. Tuliandamwa na msiba baada ya mwingine. Kwanza nilipoteza majumba mengine mawili. La kwanza ni lile lililokuwa katika mtaa wa Zari…” (Matei, 2014:53)

Wanauhalisia wanaeleza kuwa, fasihi inafaa kueleza ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe. Mathalani, Winerman (2005) anasema kuwa, wanaume wanapokumbwa na matatizo, hawaonyeshi hisia zao kwani hawataki waonekane wadhaifu. Hili linadhihirika kupitia kwa Lunga Kiriri Kangata aliyethiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Mizozo hii inamfanya Lunga kukata tamaa. Hali hii ilichangiwa na uharibifu wa mali na mazao aliyokuwa ameyachuma kwa muda mrefu baada ya kufutwa kazi kutoka katika shirika la Fanaka. Mali haya yaliharibiwa kwa kile kilichosemekana kwamba Lunga Kangata alikuwa akikaa katika ardhi ya wenyewe. Lunga Kangata na wenzake walihamishwa kutoka Msitu wa Mamba hadi Mlima wa Simba. Jambo lingine lililomtamausha Lunga Kangata ni kutoroka kwa mkewe Bi. Naomi. Lunga Kangata alikumbwa na kihoro na baadaye akashikwa na ugonjwa wa shinikizo la damu, mwishowe akafariki. Mwandishi anasema;

> Katika hali hii, Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki." (Matei, 2014: 81-82)

Vita vilipozuka katika nchi ya Wahafidhina, Kaizari na mkewe, Bi. Subira walishambuliwa kwa sime na genge la vijana waliokuwa wakiandamana wakipinga matokeo ya uchaguzi. Mabinti wake, Lime na Mwanaheri, walibakwa machoni mwake asiwe na uwezo wa kuwaauni. Vita vilipokwisha walirudishwa nyumbani kutoka Msitu wa Mamba, wakaanza maisha yao upya. Naye Subira alionekana kukata tamaa kutokana na matendo ya mama mkwe wake. Mama mkwe wake alimfanyia chuki kwa sababu alikuwa ametoka katika ukoo tofauti na familia ya bwanake. Alikuwa ametoka jamii ya Bamwezi na mama mkwe

wake alimrejelea kama Muki, yaani 'huyo wa kuja.'Kufuatia ubaguzi huu, Subira alitorokea mjini Kisuka alipojihusisha katika unywaji wa pombe haramu. Kaizari alipoenda kumtafuta huko, alipata Subira amejifia chumbani mwake huku chupa ya mvinyo ikiwa ubavuni mwake.  Mwanaheri anasema;

> "...Baba alifululiza mjini kumfuata mama, majuto yamemjaa kifuani.Miezi miwili, mitatu, minne, mitano, sita…Hata alipompata alikuwa amejifia chumbani mwake wiki mbili zilizopita, tayari mafunza yanafanya kazi yao…" (Matei, 2014: 96-97)

Aidha, Naomi, mkewe Lunga Kiriri ni mwathiriwa mwingine wa ghasia za kisiasa na kijamii aliyesawiriwa kukata tamaa. Naomi aliitoroka familia yake kwa sababu ya ufukara uliowakumba baada ya wao kuhamishwa kutoka msitu wa Mamba hadi mlima wa Simba. Alimwandikia mmewe ujumbe wa rununu na kumwambia kuwa ameenda kutafuta cha kuwasaidia. Ujumbe ulisema;

> Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao. (Matei, 2014: 81)

Alipofika katika jiji la Karaha alijaribu kutafuta kazi akitumia stashahada yake ya uhazigi bila mafanikio.  Mwishowe alipata kazi ya kuuza nguo kuukuu kwa bwana Kimbaumbau. Kazi hii ya Kimbaumbau haikumwendea vyema kwani Bwana huyu alikuwa na tabia ya ukware. Maji yalipozidi unga, Naomi aliacha kazi na kurudi nyumbani katika Mlima wa Simba. Alipofika huko alipata mmewe, Lunga Kangata, amefariki.

### 3.2 Wahusika Waliosawiriwa kama Wachochezi

Kwa mujibu wa Hogan (2007), watu huchochewa kuzua vurugu na ghasia za kisiasa baada ya kutoridhika na uongozi ulio mamlakani. Uongozi mbaya hudhihirika kupitia kwa maisha duni wanayoishi watawaliwa. Katika riwaya teule za Kiswahili, baadhi ya wahusika wamesawiriwa kama watu waliokuwa wachochezi na wazua ghasia. Miongoni mwa wachochezi hao kulikuwepo na viongozi wa kisiasa na wa kidini.

Aidha kulikuwepo na vijana pamoja na waandamanaji walioshiriki uchochezi pamoja na mauaji ya watu. Stewart  (2001), anafafanua kuwa kiini hasa kinachowachochea watu kushiriki vita vya kisiasa na kijamii ni tofauti za kiuchumi na kisiasa, ukosefu wa usawa katika jamii, umaskini, uchumi usiokua, huduma mbovu za kiserikali, ukosefu wa kazi na ari ya kibinafsi ya watu kutaka kupigana. Anasema kwamba mataifa manane kati ya mataifa kumi yaliyo maskini zaidi ulimwenguni yamewahi kukumbwa na ghasia za kisiasa.

Kwa mujibu wa nadharia nadharia ya Uhalisia, sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, baadhi ya viongozi wa kisiasa na kidini wanatuhumiwa kuchochea ghasia. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, kuna wahusika waliokuwa viongozi wa kidini na wa serikali waliosawiriwa kama wachochezi wa ghasia za kisiasa na kijamii. Aidha, kulikuwa na wananchi wa kawaida waliochochea na kushiriki ghasia za kisiasa na kijamii. Mbunge wa eneo la Korosho, mheshimiwa Mabende ni mmojawapo wa viongozi wa kisiasa waliochochea na kufadhili ghasia za kisiasa na kijamiis wilayani Korosho. Mheshimiwa Mabende alihutubia mkutano wa hadhara katika uwanja wa soko la Baraki na kusema kwamba Wakanju ni 'madoadoa' ambao walistahili kurudishwa kwao Kanju.

Alishangiliwa na Wakorosho huku Wakanju wakisononeka mioyoni kwa sababu ya matamshi haya. Mabende anasema;

> "Hatutaki 'madoadoa' hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju." (Walibora, 2003:2)

Bwana Mabende aliwachukia Wakanju kwa madai kwamba Wakanju hawakumpigia kura na pia walipinga serikali ya Kiwachema. Mwalimu Alex aliyekuwa Mkorosho, aliuawa ili ionekane kwamba ameuawa na Wakanju ndiposa wapate sababu za kuwashambulia Wakanju. Bwana Mabende alipoteuliwa kama waziri wa usalama wa ndani wa nchi ya Kiwachema, wananchi waliudhika kwa muuaji kapewa nafasi ya kulinda wananchi. Johnson Muyaka alisononeka sana kuhusu uteuzi wa Mabende kama waziri wa usalama wa ndani. Alikataa kula chakula wala kukoga kwa siku kadhaa kama ishara ya kuomboleza uteuzi wa Mabende kama waziri wa usalama. Mwandishi ananukuu ifuatavyo;

> Nikamuuliza; "Kuna nini?"
>
> "Mwuaji kapewa kazi ya kulinda uhai wa watu," alisema.
>
> "Unamaanisha nini?"
>
> "We' hujasikia mbunge wa Korosho Mabende kapewa wadhfa wa waziri wa usalama wa ndani."
>
> Nilikuwa sina mwao na hilo.
>
> "Mabende!" Nilimaka.(Walibora, 2003: 163)

Kutokana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; msanii atumie mandhari na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, mandhari ya kivita yanamsawiri Zablon kama

mchochezi. Zablon Mapisi alikuwa mmojawapo wa wanamgambo wa kivita waliokuwa katika genge lililoshiriki mauaji ya watu na kuzua vujo wilayani Korosho. Mzee Mangala alipouawa katika vita vya kisiasa na kikabila, Toma liuchukua mwili wake kijijini Baraki, kuuzika. Punde tu baada ya mazishi, Tom alishambuliwa na genge la wapiganaji. Akida akiwa kichakani amejificha, genge lingine la wapiganaji lilirudi tena likiongozwa na Zablon Mapisi likiwa limebeba zana za kivita. Kundi hili lilitaka kumkata Tom kichwa licha ya kwamba alikuwa mahututi na kudhaniwa kuwa amekufa. Hata hivyo walighairi nia ya kumkata kichwa na wakaenda zao. Akida anasema;

> Nilimwona mtu mmoja miongoni mwao, mfupi wa kimo. Uso wake ulionyesha mtu aliyekuwa sugu wa kuua; anaweza kumwua binadamu kama anayemuua mbu au nzi. Na uso huo si mgeni kwangu. Aaah! Mbona akili yangu inaingia taahira? Huyu si Mzee Zablon, babake rafiki yangu wa kufa kuzikana Tim? (Walibora, 2003: 107).

Mhusika mwingine aliyesawiriwa kama mchochezi na mzua vujo katika riwaya ya Kufa *Kuzikana (2003)* ni Tito Tembo.Tembo alikuwa mlevi katika mtaa wa Falkland aliyejigamba kwa walevi wengine kwamba alikuwa amewaua Wakanju wengi katika ghasia za kisiasa na kijamii zilizozuka wilayani Korosho. Tembo anasema;

> "Mwenyewe mimi usinione hivi nimeua Wakanju wengi sana." Alijipigapiga kifua.
> "Usione wembamba wa reli, gari moshi hupita." (Walibora, 2003: 13)

Maneno haya ya Tito Tembo yalimuudhi Akida ambaye baadaye alichukua gongo na kumtwanga Tembo alipokuwa msalani na kumbwaga chini. Vitendo na semi za Tembo zilimsawiri kama mtu aliyezua vujo na aliyechochea ghasia za kisiasa na kijamii.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014),* baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii wamesawiriwa kama watu waliochochea ghasia, uharibifu wa mali pamoja na mauaji ya watu katika nchi ya Wahafidhina. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, ilibainika kuwa vijana walikuwa katika mstari wa mbele katika kuchochea na kuzua ghasia za kisiasa na kikabila. Vijana walipewa ahadi za uongo kwamba wangepata ajira baada ya viongozi kushindi katika uchaguzi. Pia waliahidiwa mikopo ya kufanyia biashara. Viongozi waliwashirikisha vijana katika njama za kifisadi na wizi wa kura. Hata hivyo baada ya uchaguzi, vijana hawa walisahauliwa jinsi walivyokuwa hapo awali hawana ajira, hawana pesa za kuanzisha biashara, wanahangaika na maisha ya ufukara. Hali hii iliwafanya vijana kushiriki katika ghasia za uchaguzi kwa kuwachochea wenzao na hata kutekeleza mauaji na uharibifu wa mali. Kijana mmoja analalama;

> "Wengine tulikuwa tumeahidiwa makubwa wakati wa vuguvugu la kuwania nafasi za uongozi. Mara, 'Ubalozi wa Emirates unahitaji kijana aliyesomea shahada ya uzamifu katika mahusiano ya kimataifa kama wewe"(Matei, 2014: 23)

Makundi mawili yalizozana kuhusiana na uteuzi wa Mwekevu Tendakazi. Kundi lililopinga uteuzi wake lilidai kuwa jamii ya Wahafidhina haijawahi kuongozwa na mwanamke tangu enzi za kiistiimari. Walisema kwamba serikali iliyokuwepo ilikuwa ikiwapendelea wanawake kwa njia zozote zile na kuacha jinsia ya kiume kuteseka. Aidha, walidai kuwa Mwekevu Tendakazi aliiba kura. Mwandishi ananukuu;

> "Tangu lini mwanamke akashinda katika uchaguzi? Kama mama taifa hakuyashinda majabali miaka kumi na mitano iliyopita itakuwa huyu mwanagenzi ambaye hata kushika mgwisho sisi ndio tulimfunza? Lazima ameiba kura! Lazima

> wafuasi wake waliwanunua akina mama ambao ndio wapiga kura wengi," Sauti zikalalama. (Matei, 2014: 18-19)

Kundi lililomuunga mkono Mwekevu Tendakazi lilidai kwamba ushindi wake ulitokana na utendakazi wake katika nyadhfa mbalimbali za uongozi alizoshikilia. Mwekevu Tendakazi aliwahi kuwa mkurugenzi wa shirika la Chemichemi ambapo alitenda kazi kwa juhudi kubwa hadi utendakazi wake ukadhihirika. Aidha aliweza kushikilia nyadhfa kama waziri ambapo alidhihirisha bidii yake katika utendakazi wake kwa wananchi aliowahudumia. Ni uwajibikaji huu kikazi uliomwezesha kuteuliwa kama kiongozi wa nchi ya Wahafidhina. Bi Shali anasema;

> "…Ushindi wake ni zao la bidii na kujisabilia kwake kuwainua raia alipokuwa mkurugenzi wa shirika la Chemichemi. Nashangazwa sana na jinsi binadamu walivyo wepesi wa kusahau! Je, ule mradi wake wa kuchimba visima haujawafaidi raia kwenye maeneo kame?" Bi. Shali alikuli. (Matei, 2014: 18)

### 3. 3 Wahusika Waliosawiriwa kama Watu wenye Matatizo ya Kisaikolojia

Mutugu (2019) akimnukuu Mackenzie (2014), anasema kwamba matatizo ya kiakili ni hali ambapo mwathiriwa hufanya mambo yasiyo ya urazini kama vile ukosefu wa uwajibika, hasira, kukata tamaa na kutokuwa na uwezo wa kujiamlia mambo ipasavyo. Watu wenye matatizo ya kiakili huonyesha mielekeo na hulka ambazo hazilingani na maadili, pamoja na matakwa ya jamii. Mtafiti alitambua kuwa baadhi ya wahusika walisawiriwa kama watu waliokuwa na matatizo ya kisaikolojia. Changamoto hii ilitokana na madhila waliyokumbana nayo kufuatia kuzuka kwa ghasia za kisiasa na kijamii. Wengine wao walifurushwa kwao, wengine wakafiwa na jamaa zao, wengine mali yao kuharibiwa, wengine familia  kutengana miongoni mwa matatizo mengine.

Kutokana na nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; sanaa iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku, wahusika kadhaa wamesawiriwa kuwa na msongo wa mawazo. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003),*wahusika mbalimbali walisawiriwa kama watu wenye matatizo ya kisaikolojia. Tamari Mapisi aliathirika kwa kukumbwa na msongo wa mawazo. Kulipotokea ghasia za kisiasa na kijamii wilayani Korosho, familia yao haikuachwa nyuma licha ya babake, Mzee Zablon, kuwa miongoni mwa washiriki wa mauaji. Mamake na ndugu zake wengine waliuawa akabakia Tim aliyekuwa akifanya kazi jijini Tandika. Tamari alitoroka nyumbani kwao, akatembea kwa muda mrefu usiku na mchana akilala vichakani. Katika mahangaiko haya, alikumbana na hali za kuogofya. Genge la vijana waliokuwa wakipigana walijaribu kumbaka lakini akajinusuru, alishuhudia watu wakiuawa na kukumbana na miili ya wafu vichakani na

barabarani. Hata alipofika katika jiji la Tandika, alikuwa amejawa na fikra nyingi zilizomfanya kusongwa na mawazo tele. Pam na Akida wanasema;

> "Umesikia vile mambo yalivyo?"
>
> "Wacha kusikia, nimeona matokeo yake," alimwashiria Tamari aliyekuwa anaanza kuforota. "Msichana wa watu mzuri kaponea tundu la sindano. Walijaribu kumnajisi akajinasua na kuwakwepa. Anatembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa. Ameona maiti ngapi sijui? Ameona watu wakiuawa, mtoto mdogo pale alipo. Anasema alipata lifti kwa lori ya wafadhili waliomleta mpaka kwenye geti…" (Walibora, 2003: 67-68)

Kutokana na msongo wa mawazo, Tamari alibadilika kitabia akawa anatoa matusi, lugha chafu na hata kupiga kelele ovyoovyo. Alipompata Akida aliyekuwa akistakimu chumbani humo, Tamari alimtolea matusi, akamwonyesha madharau na kumfokea kwa misingi ya kikabila. Akida alikuwa Mkanju ilhali Tim na Tamari walikuwa Wakorosho. Mwandishi ananukuu;

> "Umerukwa na akili?" nikamwuliza.
>
> "Wakanju ni mbwa."
>
> "Eeh! Tamari wacha matusi hapa. Utanizulia zani bure," Tim alimsihi dadake. (Walibora, 2003: 130)

Wanauhalisia wanaamini kuwa, wahusika wasawiriwe kama walivyo katika jamii. Kulipotokea machafuko ya kisiasa nchini Kenya mwaka wa 2007 na 2008, waathiriwa wengi walisongwa na mawazo huku wangine wakishikwa na magonjwa ya kiakili.

Kwa mujibu wa Scott (2020), baadhi ya matatizo ya kisaikolojia huweza kusababishwa na masuala kama vile unyayasaji wa kijinsia, dhuluma kwa raia na umaskini.

Mhusika mwingine aliyesawiriwa kuwa na msongo wa mawazo ni Tom Mangala. Mhusika huyu alikumbwa na tatizo la msongo wa mawazo wakati babake, Mzee Mangala, alipouawa na genge la wapiganaji wilayani Korosho. Baada ya kumzika, Tom aliingia garini akakimya kwa muda akiwaza na kumwomboleza babake, Mzee Mangala. Akida anaeleza;

> Hapo ndipo nilipomwona Tom anatoa kitambaa mfukoni na kufuta machozi machoni. Aliinamisha kichwa, akarejea kwenye basini na kuketi ndani peke yake kitambo. (Walibora, 2003: 99)

Kama unavyosema mhimili wa nadharia ya uhalisia kuwa, wahusika wasawiriwe kama walivyo katika jamii, Akida anachorwa kuwa na msongo wa mawazo. Akida alikuwa amemshambulia Mzee Tito katika mangweni moja ya kuuza pombe haramu. Mzee Tito alikuwa anajigamba mbele ya walevi wengine kuwa alikuwa amewaua Wakanju wengi vitani huko Korosho. Kwa sababu Akida alikuwa Mkanju alipandwa na hamaki kuhusu kuuawa kwa Wakanju wenzake. Mzee Tito alipoelekea msalani, Akida alimfuata huko na kumtwanga kwa gongo na kumtupa chini. Baadaye Akida aligura jiji la Tandika na kutorokea wilayani Sangura katika kijiji cha Binge kuzumbua riziki. Baada ya miaka mitatu, Akida alirudi tena jijini Tandika. Hapo jijini, msongo wa mawazo ulimkumba, akawaza kuhusu kitendo alichokifanya. Akaanza kuzunguka barabara za jiji akiwazia kujiua, akanuia kununua sumu ya panya anywe. Akida anawazo;

> Dhamiri yangu imenishtaki na kunighasi kwa muda huo wote. Hakuna purukushani ambayo inaweza kunisahaulisha hatia yangu. Sikupata nafuu hata baada ya kukimbilia Sangura umbali wa kilomita mia nne kutoka hapa Tandika jijini. Bora nijisalimishe kwa polisi niondokane na kero na usumbufu hata ikibidi nife kwa mkono chakari. Hisia za hatia zimenitafiri kwa siku nyingi. Lo! Kitendo nilichokitenda katika wimbi la hasira…je, maskini babangu hakunionya kuwa hasira yangu itakuja kunihasiri? Hasira ni hasara. Maneno yake yamesibu barabara. (Walibora, 2003: 182)

Kutokana na mawazo haya, Akida anaonekana kama mtu aliyekuwa na matatizo ya kisaikolojia. Matatizo mengine yaliyochangia Akida kuwa na msongo wa mawazo ni kusingiziwa kwamba amemnajisi Tamari, kitendo ambacho hakukifanya. Aidha Akida alikosa kuendelea na masomo katika shule ya upili, ufadhili wake uliposimamishwa na kupewa mwanafunzi mwingine.

Katika riwaya ya *Chozi La Heri (2014)*, baadhi ya wahusika waliathirika kwa kukumbwa na matatizo ya kisaikolojia. Ridhaa ni mmojawapo wa wahusika waliokumbwa na matatizo ya kisaikolojia. Vita vilipozuka katika nchi ya Wahafidhina, Daktari Ridhaa alipatwa na misiba na majanga. Mkewe Ridhaa, Terry, bintiye, Anatila, mkaza mwanawe, Lily Nyamvula na mjukuu wake, Becky, waliangamia kwa kuteketezwa katika jumba la Ridhaa. Msiba huu ulimwachia majonzi yaliyomfanya Ridhaa kukumbwa na matatizo ya kisaikolojia. Mwandishi anasema;

> Ridhaa hakujua alikuwa amesimama pale kwa muda gani. Miguu yake sasa ilianza kulalamika. Polepole parafujo za mwili wake zililegea, akaketi juu ya majivu-la, juu ya miili ya wapenzi wake. Baada ya muda wa mvutano wa hisia na mawazo, usingizi ulimwiba. Katika fikira zake ambazo tangu hapo zilikuwa macho, alikumbuka taarifa ya habari kwenye runinga… (Matei, 2014: 12)

Kutokana na nguzo ya nadharia ya uhalisia inayosema; fasihi iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mandhari yake, Ridhaa alisongwa na mawazo kwa kuharibiwa mali yake. Majumba yake yaliharibiwa; jumba moja likibomolewa na serikali kwa madai kwamba lilikuwa limejengwa katika ardhi ya umma iliyotengewa ujenzi wa Bypass. Vilevile jumba lingine alilopangisha watu liliteketezwa na moto kwa kile kilichosemekana kuwa hitilafu za nguvu za umeme. Nduguye, Bwana Makaa, naye alichomeka motoni alipoenda kuwaokoa watu waliokuwa wakichomeka kutokana na moto wa petroli. Tanki la mafuta ya petroli lilikuwa limeanguka, na watu wakaparamia kuchota mafuta. Makaa alipojaribu kuwaokoa, naye akaangamia. Ridhaa anasema;

> "Maisha yalitubadilikia mara tu baada ya kuondoka kwako. Tuliandamwa na msiba baada ya mwingine. Kwanza nilipoteza majumba mengine mawili…" (Matei, 2014: 53)

Mwangeka ni mhusika mwingine aliyeathiriwa na matatizo ya kisaikolojia. Mkewe, Lily Nyamvula, na mwanawe, Becky, waliteketezwa motoni kufuatia ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Vita vya kisiasa na kisiasa vilikuwa vimezuka nchini humo baada ya Mwekevu Tendakazi kuchaguliwa kama kiongozi wa taifa la Wahafidhina na kumpiku mpinzani wake mwanamme. Mwangeka aliporejea nchini

mwake alielekezwa moja kwa moja hadi nyumbani kwao na babake. Nyumbani kwao alikumbana na ganjo la nyumba ya babake na majivu ya wapendwa wake. Taswira ya uharibifu wa jumba la babake na majivu ya wapendwa wake, Ridhaa alipatwa na mawazo tele. Mandhari haya yanawiana na uamilifu wa nadharia ya uhalisia; mtunzi atumie mazingira asilia na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake. Mwangeka alikumbwa na mawazo tele, akashikwa na kisunzi hata kuzirai kwa muda. Alipopata fahamu alibaki kimya akiwaza kwa muda kuhusu misiba hii aliyoipata pamoja na uharibifu wa mali ya babake, Ridhaa. Mwandishi anasema;

> Hata alipotazama kidimbwi hiki, mawazo yake yako mbali kule-e-e-e alikoanzia maisha. Anakumbuka changamoto za ukuaji wake. Anawakumbuka wanuna wake, Mukeli na Anatila, ambaye wakimwita Tila. Anapokumbuka Annatila mwili unamzizima kidogo, anatabasamu kisha tone moja la chozi linamdondoka. Kumbukumbu ya Annatila inavuta taswira ya mnuna wake mkembe--Dede – ambaye alifariki dunia... (Matei, 2014: 58)

Kutokana na janga hili, Mwangeka anaonekana mwenye matatizo ya kisaikolojia. Baadaye, Mwangeka alimuoa Rachael Apondi aliyekuwa mjane wa Bwana Mandu. Rachael Apondi alikuwa mfanyakazi katika wizara ya usalama na waliweza kupata mtoto wa kiume aliyeitwa Don Ridhaa. Aidha walikuwa na mtoto mwingine aliyeitwa Sophie na pia wakamchukua Umulkheri kama mwana wao wa kupanga.

Lunga Kangata ni mhusika mwingine aliyesawiriwa kuwa na msongo wa mawazo pamoja na matatizo ya kisaikolojia. Msongo wa mawazo ulitokana na kuharibiwa kwa mali yake

katika Msitu wa Mamba. Hapo awali, Lunga alikuwa amefutwa kazi kutoka shirika la nafaka kama mkurugenzi. Baada ya kupanda mazao na kutononoka si haba katika Msitu wa Mamba, walitimuliwa kwa kile kilichosemekana kuwa hawakuwa wakazi asilia wa eneo hilo na wakarudishwa katika Mlima wa Simba ambako inaaminika kuwa mababu zake walitoka katika maeneo ya Kaloleni. Lunga Kangata alikumbwa na ufukara na kuwapoteza marafiki zake huku wanawe wakianza kusomea shule za kutwa kinyume na hapo awali walipokuwa wakisoma katika shule za kifahari. Kufuatia mabadiliko haya ya kiuchumi na kijamii mkewe, Bi. Naomi alimtoroka mmewe. Mwandishi ananukuu;

> ..ameyapoteza maisha yake, amewapoteza ndugu na marafiki zake. wanawe waliosomaea katika shule za kifahari, sasa fidia waliopewa na serikali haitoshi hata kuwapeleka katika shule za watu wa kima wastani. (Matei, 2014: 79)

### 3.4 Wahusika Waliosawiriwa kama Wakimbizi.

Ndindi (1987) anasema kuwa wakimbizi hukumbwa na changamoto kama vile kukosa elimu bora, kubaguliwa kirangi na kikabila, mgongano wa tamaduni, ukosefu wa ajira na mahitaji mengine ya kimsingi. Anaendelea kusema kwamba kuna ubaguzi wa kijinsia, kukosa huduma za kiafya ikiwemo ukosefu wa usaidizi wa matatizo ya kisaikolojia. Wakimbizi hukosa usalama na kutokuwepo kwa uwezo wa kushiriki au kujihusisha katika kutoa maamuzi.

Kwa mujibu wa wanauhalisia; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, riwaya teule za Kiswahili, zimeonyesha wahusika ambao wamesawiriwa kama wakimbizi. Katika nchi ya Kiwachema, Wakorosho na Wakanju waliathiriana pakubwa. Halaiki ya

watu waliuawa huku wengine wakikimbilia usalama katika kambi za wakimbizi. Idhaa ya utangazaji ya BBC ilitangaza kwamba takribani watu themanini walikuwa wameuawa, mia tatu wakijeruhiwa huku wengine wakitorokea kambi za wakimbizi, muda mfupi tu Akida alipotoka kwao kuja jijini Tandika. Idhaa ya BBC iliripoti ifuatavyo;

> "…Habari zinazotufikia hivi punde," alisema mwanamke mtangazaji, "Zasema, mamia ya watu wameonekana wakikimbilia usalama –wengine wao kwa miguu-kwenye miji mbalimbali nchini Kiwachema, baada ya kufumuka vita vya kikabila katika wilaya ya Korosho nchini humo. Mwandishi wa BBC aliyeko Tandika jiji kuu la Kiwachema, amearifu kuwa watu takribani thamanini wameuawa na mia tatu wakajeruhiwa, wengine wao vibaya sana, katika vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju vilivyoanza siku chache zilizopita…" (Walibora, 2003:60-61)

Wakorosho na Wakanju walishambuliana kufuatia uchochezi wa viongozi waliokuwa na ushawishi mkubwa serikalini. Ni katika hamaniko hili ambapo Tamari alitorokea jiji la Tandika alikokuwa akiishi nduguye ili kujinusuru kutoka kwa vurugu hizi. Tamari alikumbwa na matatizo akiwa njiani kuelekea jijini Tandika. Alilala vichakani usiku na kunusurika kubakwa kutoka kwa genge la vijana. Baadaye alipata wahisani wakamsafirisha kwa gari hadi mlangoni kwa Tim jijini Tandika. Hali ya wahusika katika kambi za wakimbizi ilikuwa ngumu mno.  Jarida moja liliripoti ifuatavyo;

> …Matokeo yakawa uharabu mkubwa. Kiwachema ikapata wimbi kubwa la wakimbizi wa ndani kwa ndani ya nchi. Wengi wao wakikimbilia mijini na majijini. Barabara za miji ya Kiwachema sasa zimejaa ombaomba mpaka zikatapika

> wengine. Naam ombaomba waliokatwakatwa na ukata wasioulalia wala kuuamkia. (Walibora, 2003: 160-161)

Kulingana na mhimili wa nadharia ya Uhalisia, msanii atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, mazingira katika kambi za wakimbizi yamesawiriwa kuwa duni na ya kukatisha tamaa. Kama anavyofafanua Otunnu (1992), kunapotokea ghasia za kisiasa na kijamii, mazingira ya kuishi huwa magumu huku baadhi ya watu wakijipata katika kambi za wakimbizi. Waathiriwa katika riwaya teule, walikumbwa na njaa na magonjwa wakiwa katika kambi za wakimbizi. Wengine walishiriki tabia za upotovu wa maadili kama tunavyoambiwa katika jarida moja kuwa baadhi ya wasichana na kina mama walipigania wateja wanaume. Aidha wakimbizi hawa wanasawiriwa kuwa wezi wa mabavu, sinzia na vibaka. Mwandishi ananukuu;

> Kiwachema ikapata wimbi kubwa la 'wakimbizi' wa ndani kwa ndani ya nchi....Baadhi yao wamegeuka sinzia, vibaka, na wezi wa mabavu. Wengine wamegeuka malaya wanachuuza vinofu vyao. (Walibora 2003: 161)

Maisha yalipokuwa magumu chumbani mwa Tim baada ya Tim kufutwa kazi katika shirika la kusindika mafuta, Akida alitaka kutorokea katika kambi za wakimbizi ili aweze kujinisuru. Hata hivyo, Tim alimsihi waendelee kuvumilia maisha hayo magumu. Walianza kufanya kazi za kijungu jiko ili waweze kujikimu.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)* wahusika kadhaa wamesawiriwa kama wakimbizi. Daktari Ridhaa na familia ya Kaizari ni baadhi ya wahusika waliotorokea katika kambi za

wakimbizi. Ridhaa alikuwa ameishi katika Msitu wa Heri kwa miaka mingi tangu babu yake, Mzee Mwimo Msubiri, kuhamia maeneo hayo. Kulipotokea ghasia za kisiasa na kijamii katika taifa la Wahafidhina, aila ya Ridhaa ilishambuliwa na kuangamizwa. Mkewe Bi. Terry, bintiye, Anatila, Mkaza mwanawe, Lily Nyamvula na mjukuu wake, Becky, waliangamia motoni. Walikuwa nyumbani mwao wakati vijana walioongozwa na Mzee Kedi walipovamia nyumba yake na kuiteketeza kwa moto na kuwaangamiza. Wakati haya yakitendeka, Ridhaa alikuwa hospitalini akimshughulikia majeruhi. Aliporudi alipata familia yake imeangamia. Katika hamaniko hili, Ridhaa na waathiriwa wengine walisombwa kwenda katika kambi za wakimbizi. Ridhaa anasema;

> Ni asubuhi. Tumo katika kambi fulani-la, si kambi, mabanda hasa yaliyosongamana na kutazamana kwa jitimai na dhiki, vibanda vya mtomeo hasa. Ni siku ya kumi tangu kuondoka kwetu na kujipata katika mazingira haya mageni. (Matei, 2014: 14)

Kulinganai na nadharia ya uhalisia; msanii atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, mazingira duni ya kambi za wakimbizi yamedhihirishwa na utafiti huu. Kulikuwa na ukosefu wa chakula, maji na malazi. Aidha kulitokea magonjwa ambayo yalisababisha vifo vya watu kadhaa. Baadhi ya wakimbizi walishiriki vitendo vya upotovu wa kimaadili kwa kujihusisha katika uzinifu.

Familia ya mzee Kaizari ilikuwa mojawapo ya familia zilizosawiriwa kama wakimbizi. Kaizari na mkewe walishambuliwa na genge la wapiganaji huku wanao wawili, Lime na Mwanaheri, wakibakwa mbele yao pasiwe na wa kuwasaidia. Baadaye aila hii ilisombwa kwenda katika kambi za wakimbizi. Katika kambi za wakimbizi, hali ya maisha ilikuwa

ya kukata tamaa. Hapo mwanzoni wakimbizi walikula matunda na mizizi ya mwitu. Walilala nje huku baridi na hali ya anga ikiwatatiza.

Kulikuwa na ukosefu wa misala na magonjwa ya utapia mlo pamoja na kipindupindu yalikumba baadhi ya wakimbizi. Wengi wao walikata kamba. Hali hii ya kudunisha inawiana na uamilifu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe. Mashirika mbalimbali ya utoaji wa misaada kama vile 'mothers union', Women's Guild, Ansaar Mwangaza na kadhalika yalileta misaada kama vile chakula na malazi. Chakula kiling'ang'aniwa na wakimbizi huku kingine kikifisidiwa. Bwana Kute aliyekuwa diwani mstaafu aliigawa familia yake ikawa familia mbili zaidi.Ridhaa anasema;

> Kadiri idadi ya wakimbizi ilivyozidi kuongezeka ndivyo hali ya maisha ilivyotuwia ngumu…Vichumba vichache tulivyovijenga havikutosha kuhimili idadi ya watu walioongezeka kila mawio. Huduma za kijamii ziliadimika. Ukosefu wa misala ulipelekea kuzaliwa kwa vyoo vya kupeperushwa. (Matei, 204: 28)

### 3.5 Wahusika Waliosawiriwa kama Wajane na Mayatima

Dombrowski (2005), anasema kuwa ujane na uyatima uliotokana na vita vya kisiasa na kijamii husababisha matatizo mbalimbali. Wajane hukumbwa na mabadiliko ya muundo wa familia ambapo aidha baada ya mzazi mmoja kuaga, yule aliyebaki hubeba mzigo wa kuwa baba na mama wakati uo huo. Kuna matatizo ya kisaikolojia, ukosefu wa usalama, changamoto za kiuchumi na mzigo wa kulea familia kama mzazi mmoja.

Kwa kuongozwa na mhimili unaosema; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)* wamebaki mayatima baada ya ghasia za kisiasa na kikabila. Akida Sululu alikuwa yatima baada ya mamake, Joan Sululu, kufariki. Mama huyu alifariki katika ajali ya barabara katika vilima vya Tungule nyumbani kwao Baraki. Baadaye kulizuka mapigano makali baina ya kabila la Wakorosho na Wakanju wilayani Korosho. Makabila haya yalichochewa na viongozi wa kisiasa na wa kidini kuyashambulia makabila mengine. Wakorosho walichochewa na Mbunge wao Mheshimiwa Johnstone Mabende kuwashambulia Wakanju. Kulikuwa na madai kuwa Wakanju hawakumpigia kura mbunge huyu katika uchaguzi mkuu. Aidha, ilisemekana kwamba Wakanju walipinga serikali ya Kiwachema. Katika machafuko hayo, babake Akida, Mzee Sululu, aliuawa na jirani yake, Mzee Zablon, aliyekuwa Mkorosho. Kifo cha Mzee Sululu kilimfanya Akida kuwa yatima. Akida anasema;

> "Mama alikufa ajalini," nilisema baina ya kwikwi za kilio. "Ndugu zangu walionitangulia hata sikuwahi kuwaona. Sasa baba, mboni ya jicho langu jamani. …Sina wazazi sina ndugu." (Walibora, 2014: 198)

Mzee Zablon alikiri katika waraka kwamba ndiye aliyemuua Mzee Sululu. Kutokana na kifo hiki cha Mzee Sululu, Akida alibaki yatima.

Mhusika mwingine aliyesawiriwa kama yatima ni Tom Mangala. Tom alikuwa mtoto wa pekee wa Mzee Mangala aliyekwenda Marekani kusomea shahada ya uzamili. Alikuwa Mkanju na waliishi wilayani Korosho. Baada ya kufanya kazi kwa muda katika katika shirika la Anken, vita vilizuka nyumbani kwao Korosho. Katika fujo hizo, babake, Mzee Mangala, aliuawa. Mwili wake ulitupwa katika nyumba ya kuhifadhi maiti mjini Nduchi.

Tom alipopashwa habari kuhusu kifo cha babake, alielekea katika mji wa Nduchi na kuuhamisha mwili huo hadi hospitali ya Rufaa ya Tandika. Baadaye, Tom alisaidiwa na marafiki zake na maafisa wawili wa polisi aliowakodisha, kuupeleka mwili wa babake kijijini Baraki kwenda kuuzika huko. Tom Mangala anaomboleza ifuatavyo;

> "Ulijisabilia kwangu, ukajipa umaskini ili nipate elimu na umekufa kabla sijakupa fadhili zako. Wema wako usio na mfano pengine utatupwa kwenye jaa la sahau la kizazi hiki maluuni. Ila kama Antonio nami nasema sikuja kukusifu, nimekuja kukuzika! Buriani baba…" Tom alihitimisha taabini yake. (Walibora, 2003: 99)

Baada ya kuuzika mwili wa Mzee Mangala, genge la wapiganaji liliwavamia na kumshambulia Tom kwa kuja kumzika babake wilayani Korosho. Walimjeruhi na kumwacha katika hali mahututi wakaenda zao. Akida ndiye aliyerejea kumwauni Tom kwa kumbeba kwa toroli hadi barabara iliyoelekea jijini Tandika. Alipata wahisani wakamsaidia kumpeleka katika hospitali ya Nduchi. Baadaye mkewe, Jenelle, alimsafirisha kwenda nchini Canada kwa matibabu zaidi.

Tim Mapisi na Tamari wanasawiriwa kama wahusika mayatima. Katika utafiti huu ilibainika kwamba, babake Tim na Tamari, Mzee Zablon, alikuwa mmojawapo wa genge la Wakorosho waliotekeleza mauaji dhidi ya Wakanju. Vita vilipokwisha, Mzee Zablon alijitia kitanzi katika chumba kimoja cha Samson Tungu. Kabla ya kujiua, Zablon aliandika waraka akieleza sababu za kujitia kitanzi. Alisema kuwa mke wake na watoto wake walikuwa wameuawa vitani. Aidha katika waraka huo, anakiri kuwa yeye ndiye aliyemuua Mzee Sululu. Kujitia kitanzi kwa Mzee Zablon na vile vile kuuawa kwa mkewe, kuliwaacha Tim na Tamari mayatima. Tim anaeleza;

> "Vita vilikuwa vimekwisha. Tulikwenda na babangu. sitayasahau mambo niliyoyaona. marundo na marundo ya maiti. Haidhuru tuliwatambua watu wa aila yetu ." (Walibora, 2003: 197)

Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, ametumia waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa mayatima na wajane. Kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, tuligundua kuwa Ridhaa, Mwangeka, Lunga Kangata, Umulkheri, Dickson na Mwaliko walibaki mayatima na wajane. Hii ni baada ya ghasia za kisiasa na kijamii kuzuka katika nchi ya Wahafidhina. Mwekevu Tendakazi alikuwa amechaguliwa kama kiongozi wa nchi hiyo baada ya kumshinda mpinzani wake wa karibu. Katika fujo hizo, watu wengi waliuawa wakiwemo wazazi, wake na na watoto. Daktari Ridhaa ni mmojawapo wa wanaume ambao wake zao walifariki katika vita na kumuacha akiwa mjane. Aila yake iliangamia motoni isipokuwa mwanawe, Mwangeka, aliyekuwa akidumisha usalama katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Siku hiyo wakiangamia Daktari Ridhaa alikuwa hospitalini akimhudumia majeruhi wa vita vya kijamii na kisiasa. Ridhaa anasema;

> "Familia yangu na mali yangu yote hii kuteketea siku moja? Bila shaka hili ni zao la husuda." (Matei, 2014: 4)

Genge lililoongozwa na Mzee Kedi lilivamia makazi ya Daktari Ridhaa na kuwaua jamaa zake. Mkewe Ridhaa, Terry, bintiye, Anatila, mkaza mwanawe, Lily Nyamvula na mjukuu wake, Becky, waliangamizwa katika moto uliowachomea nyumbani mwao. Kutokana na msiba huu, Daktari Ridhaa akaondokea kuwa mjane.

Mwangeka naye anasawiriwa kama mhusika mjane na vilevile yatima baada ya ghasia za kisiasa na kijamii kuzuka katika nchi ya Wahafidhina. Baada ya kuhitimu masomo ya chuo, Mwangeka alimuoa Lily Nyamvula waliyesoma pamoja nchini Marekani. Alipohitimu, alijiunga na kikosi cha ulinzi cha wanamaji. Baadaye alielekea mashariki ya kati kudumisha usalama. Akiwa huko, mkewe, Lily Nyamvula, na aila ya babake, Mzee Ridhaa, iliangamia kutokana na ghasia za kisiasa na kijamii zilizozukaka nchini mwao. Ridhaa anawaza;

> "Maskini mwanangu, hata maisha ya unyumba hakuwa ameyakinai. Amekuwa mjane hata kabla ya ubwabwa wa shingo kumtoka!"Aliwaza Ridhaa baada ya kukamilisha usimulizi wake. (Matei, 2014: 57)

Kuangamia kwa mkewe na mamake, kulimfanya Mwangeka kubaki mjane na yatima. Aliporudi kutoka ughaibuni babake alimkaribisha katika uwanja wa ndege wa Rubia. Alimwomboleza mkewe kwa miaka miwili, kabla ya kumuoa Rachael Apondi, aliyekuwa mjane wa Mandu. Mwangeka na Apondi walianza familia upya ambapo walibarikiwa na mtoto, Don Ridhaa, na pia walikuwa na mtoto wa kike aliyeitwa Sophie. Mwangeka pia alimpanga Umulkheri kama mtoto wake na kumlea na kumfunza hadi chuo kikuu.

Kaizari amesawiriwa kama mhusika mjane katika riwaya teule ya Kiswahili. Mhusika huyu aliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii ambapo yeye na mkewe Subira walishambuliwa huku mabinti wao, Mwanaheri na Lime, wakibakwa na vijana watano mabarobaro huku wazazi wao wakishudia. Baadaye, aila ya Kaizari ilisombwa kwenda katika kambi za wakimbizi. Vita vilipokwisha, Mzee Kaizari na aila yake walirudishwa nyumbani. Waliporejea nyumbani kwao, mkewe Subira alianza kufanyiwa ubaguzi na mama mkwe

wake. Mama mkwe huyu alimwona Subira kama mgeni katika boma lao na kumrejelea kama Muki yaani ‘huyo wa kuja.’ Subira hakuweza kuvumilia madhila haya, aliitoroka na kwenda mjini Kisuka ambapo alishiriki unywaji wa pombe haramu. Baada ya miezi miwili, Mzee Kaizari alimfuata huko na akakuta Subira amejifia chumbani mwake baada ya kushiriki unywaji wa pombe haramu. Mwanaheri anasimulia;

> “Kaburi limesimama kwa kedi nje ya nyumba yetu kama ukumbusho wa mama yetu Subira ati. Linaloumiza zaidi ni kuamka kila asubuhi kumtazama baba ambaye amebaki gofu tu.” (Matei, 2014: 96-97)

Kifo cha Subira kilimuacha Mzee Kaizari kuwa mjane huku wanawe wawili wakakawa mayatima. Mkasa huu ulimwachia Mzee Kaizari uchungu moyoni kwani aliachiwa ulezi wa wanao wawili. Aliishi maisha ya ujane huku akiwalea wanawe kama mzazi mmoja.

Katika mhimili wa nadharia unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, umulkheri, Dickson na Mwaliko wanasawiriwa kama wahusika mayatima. Wahusika hawa walikuwa watoto wa Lunga Kangata na Bi. Naomi. Katika utafiti huu, tulibaini kuwa, vita vilipokwisha katika taifa la Wahafidhina, Lunga na familia yake walitimuliwa kutoka Msitu wa Mamba hadi Mlima wa Simba kulikoaminika kuwa kwao asilia. Katika eneo hili, maisha yalimbadilikia Lunga. Alikumbwa na uchechevu wa fedha kwa sababu alikuwa amefutwa kazi kutoka shirika la Nafaka na vilevile, mazao na mali yake yalikuwa yameharibiwa. Kufuatia huu ugumu wa maisha, mkewe Naomi aliamua kumtoroka Lunga na kumuachia mzigo wa kulea watoto watatu Umulkheri, Dickson na Mwaliko. Kutoroka kwa Naomi kulimsababishia msongo wa mawazo uliomletea ugonjwa wa shinikizo la damu. Mwaka mmoja baadaye Lunga aliaga dunia.Wanawe walibaki wakilelewa na Sauna. Mwandishi anaeleza;

> Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao. (Matei, 2014: 81-82)

Kufariki kwa Lunga Kangata kuliwaacha wanawe, umulkheri, Dickson na Mwaliko mayatima huku mkewe Naomi akiwa mjane. Dickson na Mwaliko walitoroshwa na kijakazi wao kuenda kulangua dawa za kulevya. Sauna aliwauza kwa bwana Buda ili kushirikishwa katika biashara hii haramu. Dick aliendelea kufanya biashara hii huku Mwaliko akiokolewa na maafisa wa serikali. Umulheri naye alitoroka kutoka nyumbani kwao na kwenda jijini alipopata rafiki yake wa utotoni, Hazina. Hazina alimwelekeza kwa mhisani mmoja aliyemsaidia kwa kumpeleka katika shule ya Tangamano ambapo alichukuliwa na kuanza kusoma na wanafunzi wengine kwa msaada wa wahisani.

### 3.6 Wahusika Waliosawiriwa kama Watu wenye Madharau na Chuki

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalidsia; wahusika wasawiriwe kama walivyo katika jamii, ilibainika kuwa baadhi ya waathiriwa wamesawiriwa kuwa na madharau na chuki. Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003),* mhusika Tamari amesawiriwa kama mtu aliye na madharau, mabezo, chuki na matusi dhidi ya wenzake. Tamari alipotoroka vita vilivyotokea wilayani Korosho, alihamia mjini Tandika alikostakimu nduguye wa kiume, Tim Mapisi. Alipowasili chumbani mwa Tim, alimkuta Akida mwanafunzi waliyesoma pamoja katika shule ya msingi ya Baraki. Tangu utotoni Tamari na Akida walichukiana na kudharauriana kwa misingi ya tofauti za kikabila. Punde tu Tamari alipomuona Akida, alimtolea matusi na kumwonyesha madharau kwa sababu Akida alikuwa Mkanju. Aliwaita Wakanju kama watu wajinga, watu wasiotahiriwa na wenye tabia ya ufuska. Tamari anasema;

"Wakanju ni mbwa tu."

"Ee! Tamari wacha matusi hapa. Usinizulie zani bure," Tim alimsihi dadake. (Walibora, 2003: 130)

Semi hizi zinamsawiri Tamari kama binti mwenye madharau pamoja na chuki dhidi ya watu wa makabila mengine. Tamari alimwambia Akida kwamba Wakanju walikuwa wauaji na akamtaka Akida aondoke chumbani mwa nduguye, Tim. Madharau pamoja na matusi haya yalichochewa kufuatia chuki zilizokuwa baina ya Wakorosho na Wakanju.

**3. 7 Hitimisho**

Sura hii ilishughulikia usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003)*. Katika kusawiri wahusika, tumeangazia sifa za wahusika hao, hali waliyopitia na majukumu yao katika ghasia za kisiasa na kijamii. Tuligundua kuwa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii wameweza kusawiriwa katika njia mbalimbali. Baadhi ya wahusika walisawiriwa kama waliokata tamaa na wenye matatizo ya kisaikolojia huku wengine wakisawiriwa kama wakimbizi. Aidha wahusika wengine wamesawiriwa kama wajane na mayatima huku wengine wakiwa wenye madharau na chuki dhidi ya makabila mengine. Kigezo kingine ambacho wahusika hawa walisawiriwa ni wale wachochezi. Sura inayofuata imetathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za Kiswahili.

# SURA YA NNE

# KUTATHMINI MAUDHUI YALIYOKUZWA NA KUENDELEZWA KUPITIA KWA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIJAMII KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LA HERI* (2014) NA *KUFA KUZIKANA* (2003)

## 4.0 Utangulizi

Sura hii, imeshughulikia maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kikabila katika riwaya teule za Kiswahili. Waandishi wa riwaya hizi wametumia wahusika mbalimbali walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kikabila ambao wamechangia katika kukuza na kuendeleza maudhui.

## 4.1 Ubaguzi wa Kimbari na Kikabila

Justino (2012), anasema kwamba vita vya kikabila huathiri mahitaji ya kimsingi katika jamii.Vita hivi huathiri masuala ya kijamii na maelewano miongoni mwa wanajamii. Kupitia kwa mhimili wa nadharia ya uhalisia; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, tulibaini kwamba kulikuwa na tatizo la ubaguzi wa kimbari na kikabila katika riwaya teule za kiswahili.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, familia ya Ridhaa iliathirika kutokana na tatizo la ubaguzi wa kikabila na kimbari. Ubaguzi wa kikabila na kimbari ulianza kuonekana wakati Ridhaa akiwa mtoto mdogo katika shule ya msingi. Akiwa shuleni alifanyiwa ubaguzi wa kimbari na wanafunzi wenzake ambao walikataa kucheza wala kusoma naye kwa sababu alitoka katika ukoo tofauti. Babake Ridhaa, Mzee Mwimo Msubili, alikuwa amehamia sehemu ya Msitu wa Heri kwa kuwa aila yake ilikuwa kubwa na ardhi ilikuwa ndogo

kuikimu familia yake. Mzee Mwimo alioa wake kumi na wawili na watoto kadhaa. Alihamisha wake wawili hadi Msitu wa Heri ambapo mamake Ridhaa, alihamishwa na watoto wake. Katika maeneo haya, Ridhaa alifanyiwa ubaguzi na wakaazi asilia. Wanafunzi shuleni walimwita ‘Mfuata Mvua’ kwa maana kwamba yeye hakuwa mkazi asilia wa eneo hilo. Mwanafunzi mmoja anasema;

> “Wewe ni mfuata mvua,” Mwanafunzi yule akamwambia. “Hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda katika mitihani yote.” (Matei, 2014: 10)

Mambo wanayoeleza wahusika katika riwaya teule ya Kiswahili ni mambo halisi yanayotokea katika jamii kama wanavyoeleza wanauhalisia kuwa; sanaa lazima iwe ya kuaminika katika kudhihirisha hali halisi, isiwe inatiwa chuku. Kwa mfano, utafiti wa Magnarella (1994), unaonyesha kuwa makabila huweza kupigana kwa sababu za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mathalani, nchini Rwanda, Wahutu na Watutsi walipigana kwa sababu za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kufuatia ubaguzi wa kimbari kutoka kwa wakaazi asilia wa Msitu wa Heri katika riwaya teule, Ridhaa anakuza na kuendeleza maudhui ya tatizo la ubaguzi wa kikabila.

Tatizo la ubaguzi wa kimbari lilipevuka wakati ambapo wenyeji wa Msitu wa Heri walivamia na kuteketeza familia ya Daktari Ridhaa kwa moto ambapo mkewe, Terry, bintiye, Anatila, na mjukuu wake, Becky, waliangamia. Haya yalitokea baada ya uchaguzi katika nchi ya Wahafidhina ambapo Mwekevu aliteuliwa kama kiongozi wa taifa hilo. Mauaji haya yalitokea Ridhaa akiwa hospitalini akimshughulikia majeruhi wa ghasia za kisiasa na kijamii. Mwandishi anasema;

> Wakaanzisha fujo, fujo ambazo zilionekana kuwa cheche moja ya moto, zikapuuzwa! Kumbe zingekuwa jahanamu ya kuangamizia juhudi za miaka hamsini za raia kuijenga jamii yao! Cheche hizi ndizo zilizoichoma aila ya Ridhaa, ndizo zinazomuunguza moyo wake hata sasa. (Matei, 2014:46)

Tatizo la ubaguzi wa kimbari pia linajitokeza kupitia kwa mhusika Subira aliyekuwa mke wa Kaizari. Mwandishi anaonyesha kwamba Subira alitoka katika jamii ya Bamwezi iliyokuwa jamii tofauti na ya mmewe, Kaizari. Kupitia utafiti huu, tulitambua kuwa, Subira alitengwa kwa misingi ya kikabila. Mama mkwe wake alimrejelea Subira kama 'Huyo wa Kuja.' Kulingana nao, hii ilimaanisha kwamba Subira hakuwa na haki yoyote katika jamii ya mumewe. Mamake Kaizari alimwona Subira kama ndiye chanzo cha majirani kuteketeza mali ya Kaizari na kwamba familia hii ilikuwa inamweka mtu aliyekuwa wa ukoo tofauti. Subira alipoona ubaguzi dhidi yake umekithiri, alimwandikia bintiye, Mwanaheri, waraka na kumwambia kwamba ametorokea mji wa Kizuka. Barua ilisema;

> Sikudhamiria hata siku moja kuwaacha wewe, Lime, wala baba yenu. Lakini uvumilivu wangu umeshindwa kuniletea mbivu. Nimemeza shubiri kwa miaka mingi; kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiwa kwa nisiyoyatenda. (Matei,2014: 95)

Subira alipofika katika mji wa Kizuka, alijihusisha na unywaji wa pombe haramu. Kaizari alipomfuatia huko, alimpata Subira akiwa amejifia chumbani mwake, wiki mbili zilizopita, huku chupa ya kinywaji kikali ikiwa ubavuni mwake. Walizoazoa mwili wake na kuuzika nyumbani kwa Mzee Kaizari.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, baadhi ya wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii wamekuza na kuendeleza maudhui ya tatizo la ubaguzi wa kikabila na kimbari. Tim Mapisi na Akida Sululu walipomtembelea Bwana Samson Tungu kumjulia hali, Tungu alimuonyesha Akida ubaguzi wa kikabila na kumdunisha kwa misingi ya kikabila. Bwana Samson Tungu alikuwa mjombake Tim na alikuwa Mkorosho. Akida Sululu alikuwa Mkanju na wote walitoka wilayani Korosho. Hili linadhihirisha uamilifu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia; sanaa inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka. Mfano, mnamo mwaka wa 2007/2008, makabila mbalimbali yalichochewa kupigana nchini Kenya. Makabila ya Wakikuyu, Wakisii, Wakamba na Waluhya yalishambuliwa kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa wa Bonde la Ufa. Katika utafiti huu, tulibaini kuwa Mzee Tungu alipogundua kuwa Akida alikuwa Mkanju, alianza kumtolea matusi ya kumdhalilisha kwa misingi ya kikabila. Tungu anasema;

> "Wakanju?" aliendelea yule mzee huku amenikazia macho. "Hakuna watu wajinga kama Wakanju. Mimi huwa nasema mambo haya kwa jahara, sifichi kitu." (Walibora, 2003:25)

Tungu alipogundua kwamba Tim alikuwa anaishi na Akida chumba kimoja katika mtaa wa Falkland, alimwachisha Tim kazi. Samson Tungu alikuwa amemwajiri Tim kama karani katika kampuni ya kusindika mafuta jijini Tandika.

Wahusika wengine walioendeleza maudhui ya tatizo la ubaguzi wa kimbari na kikabila ni pamoja na Mzee Sululu, Mzee Mapisi, Mzee Uledi, Mzee Mangala na Tom Mangala. Kupitia utafiti huu tulibaini kwamba Wakorosho na Wakanju walishambuliana na

kuangamizana wilayani Korosho kwa sababu ya tofauti za kikabila. Mzee Zablon Mapisa aliyekuwa Mkorosho alimuua jirani yake, Mzee Sululu, aliyekuwa Mkanju. Maafa haya yalisababishwa na uchochezi wa viongozi wa kisiasa kama vile Johnstone Mabende aliyekuwa mbunge wa eneobunge la Korosho. Kiongozi huyu aliwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju ambapo aliwarejelea Wakorosho kama 'madoadoa' ambao walistahili kuondolewa kutoka wilaya ya Korosho. Akida anasema;

Siku moja mbunge wa kwetu Johnstone Mabende alihutubia mkutano wa hadhara katika kituo cha biashara cha Baraki. Nakumbuka mpaka sasa alivyosema;

> "Hatutaki 'madoadoa' hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju." (Walibora, 2003:2)

Mzee Uledi na Mzee Mangala ni wahusika wengine walioendeleza maudhui ya ubaguzi wa kimbari na kikabila katika jamii. Mzee Mangala alikuwa babake Tom, mmewe Jenelle na walikuwa wenye asili ya Kikanju. Waliishi wilayani Korosho na walitengwa kwa misingi ya kikabila na Wakorosho. Vita viliposhuka wilayani Korosho, Mzee Mangala aliuawa na Wakorosho waliokuwa wakiwashambulia Wakanju wilayani Korosho. Tom alipoenda kumzika Mzee Mangala kijijini Baraki, alishambuliwa na genge la wapiganaji la Wakorosho lililoongozwa na Mzee Zablon Mapisi. Tom alishambuliwa akaachwa hali mahututi. Baadaye alipata wahisani ambao walimsafirisha Tom hadi hospitali ya Rufaa ya Tandika alikolazwa kabla ya kusafirishwa kwenda nchini Canada kwa matibabu zaidi. Tom anaomboleza;

> "Baba….Kosa lako lilikuwa nini? Ulifanya kosa kuzaliwa katika kabila la Wakanju, ndio maana mshale mchungu umekupeleka njia ya haki. Kosa lako kabila lako." (Walibora, 2003: 98)

Waliaula (1996:98-99), anasema kuwa, maendeleo bora ni yale ya kutokuwepo adui wala silaha za kujihami, tajiri wala maskini, wala mbaguano wowote wa kikabila, kirangi wala kilugha. Utafiti wetu umetambua kuwa baadhi ya viongozi walichochea ubaguzi wa kimbari na kikabila. Mheshimiwa Johnstone Mabende ni mmojwapo wa viongozi waliochochea na kufadhili mashambulizi ya Wakorosho dhidi ya Wakanju wilayani Korosho. Mwandishi ananukuu jarida moja alilokuwa nalo Jerumani, kwamba ghasia wilayani Korosho zilipangwa na viongozi wa kidini na kisiasa. Viongozi waliotajwa na jaridi hili ni Mheshimiwa Johnstone Mabende na Kasisi John Njalala. Wakorosho walichochewa wakamuua Mwalimu Alex aliyekuwa Mkorosho. Mauaji haya yalifanywa ili Wakorosho wapate kisingizio cha kuwashambulia Wakanju. Jarida hilo lilifafanua kwamba, serikali iliyafahamu mauaji hayo na njama zote zilizofanywa ili kuwashambulia Wakanju walioshi wilayani Korosho. Jarida hilo lilinukuu;

> Serikali iliyafumbia macho mauaji hayo kwa vile maafisa wa ngazi za juu serikalini walihusika. Vita hivyo vilikuwa kwa maslahi yao. Wakanju wakionwa kama wapinzani kwa serikali na kwa hiyo ilikuwa stahili yao. Imebainika wazi kuwa mheshimiwa Mabende alitaka kuwatimua Wakanju kutoka wilayani Korosho kwa madai kuwa hawakumpigia kura katika uchaguzi uliopita. (Walibora, 2003: 160)

Kupitia kwa madai ya jarida hili, tunafahamu kuwa suala la ubaguzi wa kikabila linaonekana kuchochewa na viongozi serikalini ambao walieneza chuki baina ya makabila

haya. Serikali nayo kupuuza kutatua mzozo huu na kuuacha kuendelea, ni dhihirisho kwamba tatizo hili lilikuwa limekita mizizi wilayani Korosho. Tulibaini kuwa baada ya mauaji ya Mwalimu Alex, vijikaratasi vilienezwa nyumbani kwa akina Akida vikiwataka Wakanju wahame sehemu hiyo au wauawe. Akida anasema;

> Siku iliyofuatia kupatikana kwa maiti ya mwalimu Alex, niliokota karatasi katika kiambo chetu. Ilikuwa na maandishi yaliyoandikwa kivoloya kama ya mtoto wa shule ya chekechea: "Wakanju mumechokosa nyuki kwa kumuuwaa mukoroso, Ama muondoke au mufe muzingani." (Walibora, 2003: 5)

**4. 3 Nafasi ya Vijana Katika Jamii**

Becker (2001) anadai kuwa ujana ni kipindi cha mapito kutoka hali ya utoto hadi utu uzima. Katika kipindi hiki mabadiliko mbalimbali hutokea ndipo mtoto awe mtu mzima. Katika utafiti huu, tulibaini kuwa vijana wamepewa nafasi mbalimbali katika riwaya huska. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, sanaa inapaswa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake; utafiti ulibaini kuwa baadhi ya vijana walioathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii walichangia kukuza na kundeleza maudhui ya nafasi ya vijana.

Matukio katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003) ni halisi na yanaingiliana na uhalisia wa maisha namna inavyoeleza mihimili ya nadharia ya uhalisia. Kwa mfano, utafiti ulifanywa na Munyasya (2017), unadhihirisha kwamba vijana ni wadau muhimu katika masuala yanayohusu jamii. Katika masuala ya kisiasa, vijana ndio huathirika mno kunapotatokea matatizo ya kisiasa na kijamii. Vijana huathirika kwa

kutumiwa na wanasiasa visivyo ili kuzua vurugu na ghasia na baadaye wao ndio huumizwa, kuuawa na hata kufurushwa kutoka maeneo wanapoishi.

Utafiti huu ulibaini kwamba vijana wa kike walidunishwa na kunyanyaswa kimapenzi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, familia ya Mzee Kaizari ilivamiwa na vijana watano mabarobaro ambao waliwabaka Lime na Mwanaheri na vilevile kumshambulia Subira kwa sime kabla ya kutoweka. Mzee Kaizari alitazama mabinti wake wakivamiwa na kudhulumiwa asiwe na uwezo wa kuwasaidia. Kaizari anasema;

> Siku ya nne baada ya 'mapinduzi' tulisikia hodi mlangoni. Mke wangu, Subira, ndiye aliyekwenda kufungua. Alisalimiwa kwa kofi kubwa, kisha, "Wapi kile kidume chako kijoga…Baadaye genge hili lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti wangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa. (Matei, 2014: 25)

Kupitia kwa wahusika Lime na Mwanaheri, maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii yanakuzwa na kuendelezwa. Vijana wa kike ni wadhulumiwa kimapenzi ambapo wanabakwa na kukosewa heshima.

Wahusika wengine vijana walioathirika kutokana na ghasia za kisiasa na kikabila wameonyesha ukomavu wa fikira na bidii katika kupambana na changamoto za maisha. Licha ya kukumbwa na changamoto mbalimbali maishani, vijana hawa wanajibidiisha na kufanikiwa maishani. Umulkheri, Dickson na Mwaliko ni baadhi ya vijana waliokumbwa na changamoto mbalimbali. Baba yao, Lunga Kangata, alikuwa amefariki kutokana na ugonjwa wa shinikizo la damu. Ghasia za kisiasa na kijamii zilikuwa zimetokea katika

Msitu wa Mamba ambapo Lunga Kangata alipokonywa mali yake, baadaye akashikwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na kuaga dunia. Vijana wake, Umulkheri, Dickson na Mwaliko walikumbwa na matatizo tele. Dick na Mwaliko walitoroshwa na kijakazi wao, Sauna, ambaye aliwauza kwa Bi. Kangara na Bwana Buda ambao waliwatumia kulangua dawa za kulevya. Mwaliko aliokolewa na polisi, akachakuliwa kama mtoto wa kupanga wa Mwangemi na Rehema huku Dickson akitumikishwa kulangua dawa za kulevya. Baadaye Dickson aling'amua kwamba alikuwa anafanya biashara haramu. Aliacha biashara hiyo, akaanza biashara ya kuuza vifaa vya kutengeneza simu na baadaye akajiunga na taaluma ya TEKNOHAMA alipojifunza ujuzi wa kutengeneza na kuuza bidhaa za simu. Mwandishi anasema;

> Mawazo haya yalimsukuma Dick kufikia uamuzi wa mkataa, akajinasua kutoka kwenye kucha za mwajiri wake huyu. Aliacha biashara hii haramu na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya umeme. Sasa ameanza kujitegemea, hakika amejiajiri…Amekwisha kuhitimu masomo katika chuo cha ufundi ambako alijifunza Teknolojia ya mawasiliano ya simu. (Matei, 2014: 124)

Umulkheri anawakilisha vijana kama watu walio na bidii masomoni licha ya wao kupitia changamoto mbalimbali. Alipowatafuta ndugu zake asiwapate, aliamua kutorokea jiji la Karaha. Huko jijini alikutana na rafiki yake wa utotoni aliyeitwa Hazina. Rafiki huyu alimkaribisha kwake baadaye akamsaidia Umulkheri kupata nafasi katika shule ya mayatima ya Tangamano. Akiwa shuleni, mwalimu Dhahabu alimsaidia kupata wazazi wapya ambao walimchukua Umu kama mwana wao wa kupanga. Umulkheri anasema;

> Usiku nilipotoka Mlima wa Simba nilijua kuwa maisha yangu yameingia katika mkondo wa maangamizi. Nilidhani huo ndio uliokuwa mwisho wa masomo yangu. Sikuotea kukamilisha hata kidato cha pili. Lakini nitazameni hapa nilipo. Nina familia. Nina shahada ambayo nyinyi wenyewe ndio mlioidhamini. Ndugu yangu huyu, Dick, ameweza kujiendeleza kimasomo kwa msaada wenu. Sasa anajitegemea. (Matei, 2014: 172)

Usemi huu unadhihirisha kwamba baadhi ya vijana walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii walikuwa na bidii licha ya kupitia changamoto za maisha. Umulkheri alitia bidii masomoni katika shule ya upili, akafanikiwa kujiunga na chuo kikuu ambapo alisomea taaluma ya uhandisi katika kitengo kinachohusiana na kilimo.

Kutokana na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; fasihi iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, tulibaini kuwa, Kairu ni mwathiriwa mwingine aliyeendeleza maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii. Kairu na familia yake walikumbwa na changamoto zilizotokana na ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Walipokuwa wakitoroka vita kutoka makazi yao, ndugu yake mdogo aliugua ugonjwa wa mabafu na baadaye akafariki. Baada ya kumzika kichakani walipata wahisani wakawachukua kwenda kwa kambi za wakimbizi. Kairu alijiunga na shule ya Tangamano alipokuwa akisoma. Kairu anasema;

> Nilikwenda hapo nikiwa katika darasa la sita. Sasa ni katika kidato cha pili. Tungali tunasubiri kurudishwa nyumbani! Ila sioni kama pana nyumbani zaidi ya mle kambini ambamo tunaishi bila kujali tulikotoka. Vumilia mwenzangu. Zingatia

masomo yako kwani ndiyo yatakayokuvua kutoka kwenye lindi hili la huzuni. (Matei, 2014: 92)

Mamake Kairu alikumbwa na umaskini baada ya vita kuisha nchini mwao. Umaskini huu ulitokana na biashara ya kuuza samaki kuathirika kufuatia mzozo uliohusu nani kamiliki maji na ardhi ya ziwa kuu. Mamake Kairu alikosa pesa za kumlipia karo shuleni na ikabidi azungumze na usimamizi wa shule kumruhusu awe akilipa karo kutegemea na alivyopata mpaka mwisho wa mwaka.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, vijana wanaonekana kupevuka kiakili na kushikilia utangamano na urafiki licha ya wao kutoka katika makabila tofauti tofauti. Mwandishi anabaini kuwa baadhi ya vijana wamepevuka kimawazo na migogoro, migongano, vikwazo na vizingiti vya kikabila havikuwazuia kuendeleza urafiki na uhusiano mwema. Tukiongozwa na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaosema; wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii, tuligundua kwamba Akida, Tim na Tamari ni vijana waliotoka katika makabila tofauti. Hata hivyo, vijana hawa waliweza kusuhubiana na kushirikiana vyema licha ya kwamba makabila hayo yalikuwa yakipigana wilayani Korosho. Akida alikuwa Mkanju ilhali Tim na Tamari walikuwa ndugu waliotoka katika kabila la Wakorosho. Makabila haya yalichukiana baada ya kuchochewa na viongozi, yakaanza kupigana na watu wengi waliuawa huku wengine wakijeruhiwa na kufurushwa kwao. Wakorosho na Wakanju waliokuwa wakiishi wilayani Korosho walikuwa wamechochewa na Mheshimiwa Johnstone Mabende wakapigana kwa misingi ya tofauti za kikabila. Licha ya tofauti zao za kikabila na kisiasa, Akida, Tim na Tamari

waliendelea na urafiki wao wakishirikiana na kuishi pamoja jijini Tandika. Tim na Akida wanasema;

> "Basi muhimu watu wabadilike akilini na moyoni. Mtu ajue wewe ni kabila gani, ila asikuchukie kwa msingi wa kabila lako," alisema Tim.
>
> "Kila kitu hapa Kiwachema hufanywa kwa msukumo wa kikabila," nilisema.
>
> "Eee! Bwana," alidakia maneno Tim. "Watu wa taifa hili husahau kuwa sote ni ndugu, asili yetu shamba la Edeni. Sote njia yetu moja, hakuna tofauti baina ya mtu wa kabila hili wala lile." (Walibora, 2003: 90)

Tofauti zao za kikabila hazikuwatenganisha hata ingawa Tamari alionyesha tabia ya ubaguzi wa ukabila dhidi ya Akida. Hulka hii ilitoweka baadaye na akaacha kumtenga Akida kwa misingi ya kikabila. Baadaye, ilibainika kuwa Mzee Zablon, alimuua babake Akida, Mzee Sululu, kwa sababu ya tofauti za kikabila. Mauaji haya yalimpa simansi kubwa Akida. Hata hivyo Akida na Tim waliendelea kuishi na kushirikiana pamoja. Hatimaye, Akida alifanyiwa mipango na Tom Mangala akaenda nchini Canada kusoma. Kupitia vijana hawa, tulibaini kwamba, vijana wana uwezo wa kuvuka mibaka ya tofauti za kikabila na kuwa na uhusiano na urafiki. Licha ya kubainika kwamba babake Tim, Mzee Zablon, ndiye aliyemuua babake Akida, Mzee Sululu, vijana hawa waliendelea kuishi pamoja na kuwa marafiki. Akida na Tim wanasema;

> "Usilie Akida," Tim alijaribu kunituliza. "Sote tumepoteza."
>
> "Mama alikufa ajalini," nilisema baina ya kwikwi za kilio.
>
> "Ndugu zangu walionitangulia hata sikuwahi kuwaona. Sasa baba, mboni ya jicho langu jamani….Sina wazazi sina ndugu…"
>
> "Sikiza Akida," alidakia Tim. "Mimi ndugu yako. Ndugu kuliko ndugu."

(Walibora 2003: 198)

### 4. 4 Nafasi ya Mwanamke Katika Jamii

Lyatuu (2011), anaeleza kuwa mwanamke bado amesawiriwa kama kiumbe duni mbele ya mwanamume na kwa jumla mwanamke amesawiriwa kwa hali hasi zaidi kuliko anavyosawiriwa katika hali chanya. Katika utafiti huu ilibainika kuwa, baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuwa wahusika wa jinsia ya kike ambao walikuza na kuendeleza suala la nafasi ya mwanamke katika jamii. Kupitia kwa wahusika wa kike tulibaini kwamba mwanamke amepewa nafasi mbalimbali kutegemea na mitazamo ya kijamii.

Kwa mujibu wa Maobe (2011), mwanamke anastahili kuchukua mstari wa mbele katika kupigania haki zake ili kupunguza ukandamizaji unaoelekezwa kwake na mwanamume. Mwanamke anafaa ajikomboe katika hali zote za maisha kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, Umulkheri, Kairu na Mwanaheri ni wahusika wa kike walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii ambao wamekuza madhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Kupitia kwao, tulibaini kuwa mwanamke ni mtu mwenye bidii katika jamii. Licha ya wao kupitia changamoto mbalimbali, wanatia bidii katika elimu ili kujikomboa kutoka kwa maisha magumu yaliyowaandama. Wasichana hawa walikuwa wanafunzi katika shule ya upili ya Tangamano walikokuwa wakisomea baada ya vita kuisha katika nchi ya Wahafidhina. Umulkheri alikuwa mwenye bidii katika masomo

ambapo aliweza kuhitimu na kujiunga katika chuo kikuu katika taaluma ya uhandisi katika masuala ya kilimo. Mwandishi ananukuu;

> Siku zile baada ya kuchukuliwa na Mwangeka na Apondi, Umu alijifunga nira masomoni, akafuzu vyema katika mitihani yake. Aliamua kuwa mhandisi katika uwanja wa kilimo, bila shaka anafuata nyayo za babake ambaye alikuwa mtaalamu katika uwanja huu. (Matei, 2014: 15-126)

Kutokana na nadharia ya uhalisia; sanaa iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku, utafiti wetu ulibaini kuwa Kairu na Mwanaheri ni wahusika wa jinsia ya kike walioathirika lakini walipevuka kiakili. Licha ya wao kuathirika na ghasia za kisiasa na kijamii, waliamua kutia bidii masomoni ili kujinusuru kutoka kwa changamoto za maisha. Mamake Kairu alikuwa maskini na alikosa karo ya shule, lakini akazungumza na mwalimu mkuu aliyemruhusu kulipa karo kidogo kidogo hadi mwisho wa mwaka. Kairu na Mwanaheri walikuwa wakisoma katika shule ya upili ya Tangamano. Mwandishi anasema;

> Mwanaheri alimaliza usimulizi wake ghafla na kushusha pumzi nzito. Matone mazitomazito ya machozi yalikuwa yakimdondoka. Umu na Kairu walimwacha autue mzigo wake. Hadithi yake Mwanaheri ilisomeka kama ya Umu, tofauti ni kwamba Naomi, mama yake Umu, hakumjuza kuwa ameondoka. Sasa Umu alianza kuhisi mzigo wake ukiwa mwepesi zaidi. (Matei, 2014:97)

Kupitia kwa mhusika Naomi, tulibaini kuwa mwanamke ni saliti katika mapenzi ambaye anaweza kuwasaliti hata watoto wake. Kudhihirika kwa hulika hii ya Naomi, kunawiana na uamilifu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia kuwa, wahusika lazima wasawiriwe kama

walivyo katika jamii. Naomi alikuwa mkewe Lunga Kangata na pia mamake Umulkheri, Dickson na Mwaliko. Mumewe, Bwana Lunga Kangata, aliachishwa kazi kutoka shirika la Fanaka na vilevile akafurushwa kutoka Msitu wa Mamba alipokuwa amewekeza na kushiriki shughuli za kilimo. Kufuatia kufurushwa huku, mali aliyokuwa amechuma yaliharibiwa na wakahamishwa kwenda mlima wa Simba kulikoaminiwa kuwa mababu zake walitoka. Naomi alipoona maisha yamekuwa magumu, aliamua kumuandikia mumewe ujumbe kwenye simu ya rununu na kumuambia kwamnba ameenda kutafuta kazi yoyote ili aweze kumsaidia. Akatoroka na kumuachia mumewe ulezi wa watoto; Umu, Dick na Mwaliko. Ujumbe wa simu unasema;

> Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao.
>
> Kwaheri. Naomi. (Matei, 2014: 81)

Ekuam (2006), akifafanua kuhusu migogoro mbalimbali inayovuruga amani katika bara la Afrika, anasema kwamba migogoro inapozuka, wahusika wanaoathirika mno ni watu wasio na uwezo katika jamii kama vile watoto, wanawake na wazee. Wanawake huathirika kwa kubakwa, kupigwa na hata kunyimwa huduma za kimsingi kama vile chakula, malazi na maji.

Kitendo cha ubakaji wa mabinti wa Kaizari kilikuwa zao la kumdunisha mwanamke katika jamii. Mwanamke alionekana kama chombo duni cha kufanya mapenzi na kudhulumiwa. Mabinti wa Bwana Kaizari, Lime na Mwanaheri, walibakwa na vijana mabarobaro watano waliokuwa wakiandamana wakipinga ushindi wa Mwekevu Tendakazi kama kiongozi.

Vita vya kisiasa na kimbari vilikuwa vimetokea katika nchi ya Wahafidhina baada ya Mwekevu kutangazwa kama kiongozi wa taifa hilo.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, mwanamke amepewa nafasi mbalimbali katika jamii. Mhusika Tamari, bintiye Mzee Sululu, amechangia kukuza na kuendeleza maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Kupitia kwa mhimili wanadharia ya Uhalisia unaosema; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, tulibaini kwamba jamii ya Kiwachema ilikuwa inawadunisha na kuwakandamiza wanawake kimapenzi. Vita vilipozuka wilayani Korosho,Wakorosho na Wakanju waliuana huku wengine wakifurushwa kwenda maeneo walikozaliwa. Tamari aliathirika kwa kunusurika kubakwa na vijana waliokuwa wakizua fujo wilayani Korosho. Alitorokea vichakani ambapo alishuhudia maovu yakitendewa binadamu. Baadaye Tamari alipata mhisani ambaye alimnusuru na kumchukua kwa gari hadi mlangoni mwa Tim, jijini Tandika. Pam anasema;

> "Msichana wa watu mzuri kaponea tundu la sindano: Walijaribu kumnajisi akajinasua na kuwakwepa. Ametembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa. Ameona maiti ngapi sijui? Ameona watu wakiuawa mtoto mdogo pale alipo." (Walibora, 2003: 67-68)

Mwandishi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)* anaonyesha mwanamke kama mtu mpyaro, mwenye kiburi na madharau. Haya yanabainika kupitia kwa hulka za Tamari.Tamari alipofika chumbani mwa Tim, alimkuta Akida chumbani humo.Tamari alianza kumtolea matusi ya kumdhalilisha kwa misingi ya kikabila. Alimwona Akida kama

mjinga, asiyestahili na mtu baki. Wakati mmoja Tamari alishikwa na uchu wa kimapenzi, akaenda usiku alipokuwa amelala Akida na kuanza kumchochea. Akida alipokataa, asubuhi yake Tamari alimzingizia uongo kwa nduguye, Tim, kwamba Akida alitaka kumbaka. Alimtolea matusi na kumwita mbakaji. Tamari anasema;

> "Nenda huko bwege wewe," alinitupia tusi. "Mwanzo unafanya nini katika nyumba ya kakaangu?" (Walibora, 2003: 63)

Mwandishi anabaini kwamba Tamari alikuwa na tabia hii tangu alipokuwa mwanafunzi katika shule ya Baraki, kabla ya vita kuanza nchini Kiwachema. Mwandishi anafafanua ifuatavyo;

> "…Alikuwa na ushari, sikuambii kureresha ambako kuliwashangaza watu wa Baraki. Alikuwa wa kutilika shaka tangu umri wa msichana kukumbushwa tena na tena "Kaa vizuri" Binti ya Zablon anautukanisha uke. "Watu walipita wakisema. Alifika jijini bado ananiona adui. (Walibora, 2003:)

**4. 5 Siasa**

Masaku na Kilonzo (2018), wanafafanua kwamba siasa ni mfumo wa kijamii unaohusu kutumikiza sheria ili kutoa maamuzi ya uongozi katika asasi mbalimbali za jamii. Naye Sheikha (2018), anasema kwamba uwezo wa kuwa na viongozi bora upo mikononi mwa raia kwa sababu raia ndio wenye wajibu wa kuwateua viongozi. Raia wakiteua viongozi wema, watapata maendeleo endelevu, wakiteua viongozi wabaya athari hasi zitawaendea raia wenyewe.

### 4.5. 1 Athari za Migogoro ya Kisiasa

Soo (1981), anasema kuwa migogoro ni mikinzano, kutoelewana na misuguano kati ya pande mbalimbali katika jamii. Migogoro inaweza kuwa ya kimawazo, migogoro kati ya mtu na mtu, migogoro kati ya mtu na jamii au migogoro kati ya jamii na jamii. Riwaya teule za Kiswahili zilidhihirisha migogoro ya kisiasa na kijamii ambayo ilikuwa na athari nyingi kwa waathiriwa.

Mauaji ya watu ilikuwa mojawapo ya athari za ghasia za kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Kama unavyosema mhimili wa nadharia ya uhalisia; sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, imtambua wahusika mbalimbali waliofariki kufuatia ghasia za kisiasa na kijamii. Mzee Sululu aliyekuwa Mkanju na mkaazi wa wilaya ya Korosho aliuawa na Wakorosho. Kuuawa kwake kulitokana na chuki baina ya Wakorosho na Wakanju. Vita hivyo vilichochewa na viongozi wa kisiasa na wa kidini walioendeleza chuki baina ya makabila haya. Mbunge wa eneobunge la Korosho, Johnstone Mabende, aliwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju. Ni katika ghasia hizi ambapo Mzee Sululu aliuawa. Akida ansema;

> "Mama alikufa ajalini," nilisema baina ya kwikwi za kilio.
>
> "Ndugu zangu walionitangulia hata sikuwahi kuwaona. Sasa baba, mboni ya jicho langu jamani…sina wazazi sina ndugu…" (Walibora, 2003:198)

Wahusika wengine walioangamia katika ghasia hizo ni Mzee Mangala na Mzee Zablon. Mzee Mangala alikuwa Mkanju aliyeishi wilayani Korosho. Wakanju na Wakorosho walishambuliana kwa sababu ya tofauti za kisiasa na kijamii. Kufuatia vita hivi,

Wakorosho na Wakanju wengi waliuawa. Mzee Mangala aliuawa na genge la wapiganaji kutoka jamii ya Wakorosho. Mwanawe, Tom, alipopata habari kuhusu kifo cha Mzee Mangala, aliuachukua mwili wake kutoka chumba cha kuhifadhi maiti na kuupeleka nyumbani kwao kijijini Nduchi kuuzika. Baada ya kumzika babake, Tom alishambuliwa na genge la wapiganaji Wakorosho, akaachwa yu mahututi. Genge linanong'ona;

> "Wenzake wamemwacha," nilisikia sauti za kiume kutoka kiamboni.
>
> "Wacha alale hapo aoze au aliwe na mbwa, hakuna wa kumzika."
>
> "Naam. Ati aje amzike babake kwetu Baraki? Wakanju wana haki gani kumzika mtu Baraki. Wao ni magugu sharti wang'olewe,zao linawiri. (Walibora,2003:106)

Genge hili linasema maneno haya baada ya kumshambulia Tom, aliyekuwa ameupeleka mwili wa babake kuuzika wilayani Korosho, kijijini Nduchi. Tom alishambuliwa akaachwa yu hali mahututi.

Waandishi wa riwaya teule za Kiswahili wamedhihirisha ukweli kama ulivyo katika mazingira ya kawaida jinsi inavyoeleza nadharia ya uhalisia. Kwa mfano, utafiti wa Ondoro (2021), unaonyesha kwamba vita vya kisiasa na kijamii huwa na athari hasi kwa wananchi. Mzee Zablon Mapisi ni mhusika mwingine wa watu waliohusika na kuathirika katika vurugu na mauaji ya Wakanju. Mapisi alikuwa Mkorosho na alikuwa mmojawapo wa genge lililoshiriki katika mauaji ya halaiki ya Wakanju. Kupitia utafiti huu, tulibaini kwamba familia yake iliangamia katika machafuko ya kijamii isipokuwa Tim na Tamari. Maafa haya yalimsababishia Zablon kihoro na simanzi kuu moyoni. Alijutia matendo yake ya mauaji. Akajuta kumuua Mzee Sululu mtu ambaye hakuwa na dosari. Alipozidiwa na kihoro, Zablon alijitia kitanzi. Aliwaacha wanawe wawili, Tim na Tamari. Tim anasema;

> “Baba aliporudi kwa mjomba akawa anajifungia ndanindani, hatangamani na yeyote. Ipo siku hakutoka kabisa. Wajua tena aila ya mjomba wanavyomvalia mtu miwani na kujipurukusha. Hawakushughulika. Ndipo mjomba mwenyewe alipokwenda chumbani. Akamkuta baba ananing’inia darini kwa kamba shingoni.” (Matei, 2014: 197)

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, sanaa inafaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii, Minerba (2018), anafafanua kuwa, mauko ni mojawapo wa athari zinazowakumba waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii. Wananchi huangamizana wao kwa wao au wanaweza kushambuliwa na vikosi vya serikali.

Mhusika mwingine aliyeuawa kwa sababu ya tofauti za kisiasa na kijamii ni mwalimu Alex. Mwalimu huyu alikuwa Mkorosho na alikuwa akifundisha katika shule ya msingi ya Baraki wilayani Korosho. uhakiki huu umebaini kwamba mwalimu Alex alikuwa anapinga vikali uchochezi wa kisiasa na kijamii wilayani Korosho. Alimkashfu mbunge wa eneobunge la Korosho dhidi ya kuwachochea Wakorosho kuwashambulia Wakanju. Mheshimiwa Johnstone Mabende aliwarejelea Wakanju kama ‘madoadoa’ ambao hawakustahili kuishi wilayani Korosho. Baada ya siku chache, Mwalimu Alex aliugua ugonjwa wa akili na hatimaye akapatikana ameuawa na mwili wake umetupwa kando ya Mto Kibisi. Jarida moja linanukuu;

> Mauaji ya mwalimu Alex yalipangwa yaonekane kama kitendo kilichotekelezwa na Wakanju na hivyo kuhalalisha hatua ya Wakorosho kuwakomoa katika kulipiza kisasi. Mbunge Mheshimiwa Johnstone Mabende, wakereketwa wake na viongozi

> wa kidini Wakorosho na wasiokuwa Wakorosho walikuwa watuhumiwa wakuu katika mauaji hayo ya halaiki. (Walibora, 2003: 160)

Mheshimiwa Johnstone Mabende aliuawa kwa kupigwa risasi na Jerumani. Mabende alikuwa ameteuliwa kama waziri wa usalama wa ndani wa nchi ya Kiwachema. Mabende alionekana akiwachochea Wakorosho kuwashambulia Wakanju. Alitoa maneno ya kuchochea vurugu za kijamii na kisiasa kwa kuwaita Wakanju kama ‘madoadoa’. Alipoteuliwa kama waziri wa usalama wa ndani, wananchi wengi walilalamika. Baadaye alishambuliwa na kuuawa. Akida anasema;

> Siku moja katika mwaka wangu wa pili wilayani Sangura, nilikuwa nikiisikiliza redio ya Mzee Muyaka nje ya nyumba yake. Redio ikitangaza kuwa Waziri Johnstone Mabende ameuawa kwa kupigwa risasi na mtu asiyejulikana. Alikuwa anahudhuria dhifa ya jioni katika hoteli moja kubwa jijini Tandika wakati wa kufikwa na maafa haya. (Walibora, 2003: 173)

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii waliathiriwa kwa kuuawa katika ghasia zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Kuna vifo ambavyo vilitokana na migogoro ya kisiasa. Kuna waandamanaji ambao walifyatuliwa risasi na polisi wakapoteza maisha yao. Aidha, kuna vifo vingine vilivyotokana na kukata tamaa kwa baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii. Vita hivi vilichochewa na masahibu yaliyowakumba wahusika hawa katika jamii ambayo yalipelekea waishi kwa msongo wa mawazo na hatimaye wakapoteza maisha yao.

Familia ya Ridhaa iliwapoteza watu katika vita vya kisiasa na kijamii katika nchi ya Wahafidhina. Katika mauaji haya, mkewe Ridhaa, Terry, bintiye, Anatila, mkaza mwanawe, Lily Nyamvula na mjukuu wake, Becky waliteketezwa kwa moto. Moto huu uliwashwa na vijana wakiongozwa na Mzee Kedi. Genge hili la waandamanaji lilikuwa likipinga uteuzi wa Mwekevu Tendakazi kama kiongozi wa nchi ya Wahafidhina. Mwekevu alipoteuliwa kama kiongozi wa nchi ya Wahafidhina, wapinzani wake waliokuwa wanamuunga mkono mwanamume mpinzani wake, walipinga matokeo haya, wakaanzisha vujo na maandamano. Katika ghasia hizo, watu wengi waliuawa huku wengine wakiachiwa majeraha na kufurushwa kutoka makazi yao. Mwandishi anasema;

> Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake, Becky. (Matei, 2003:5)

Subira ni mwathiriwa mwingine wa ghasia za kisiasa na kijamii aliyefariki kutokana na kufanyiwa ubaguzi wa kimbari. Subira alitengwa na wakwe zake kwa sababu ya tofauti za kimbari. Subira alitoka katika ukoo tofauti na wa mumewe. Mama mkwe wake alimuona Subira kama chanzo cha familia yao kushambuliwa. Alimrejelea Subira kama muki yaani 'huyo wa kuja.' Subira alipoona kuwa ubaguzi umekithiri, alimwandikia mwanawe; Mwanaheri, barua na kumwambia kwamba ametoroka. Alitorokea mji wa Karaha ambapo alijihusisha na unywaji wa pombe haramu. Tabia hii ya ulevi ilimfanya Subira kuaga dunia. Mwanaheri anasema;

> "Kama mama yangu angetafuta mikakati bora zaidi ya kuhusiana na wakwe zake badala ya kukata tamaa, kuukebehi utu wake kwa kututelekeza na kujikabidhi kwa

> mauti, huenda maisha yangu na ya ndugu yangu yangekuwa bora zaidi.” (Matei, 2014: 97-98)

Chanzo cha kifo cha Lunga Kiriri Kangata kilitokana na mizozo ya kisiasa na kijamii. Lunga alikuwa ameachishwa kazi kutoka shirika la nafaka. Alihamia Msitu wa Mamba, akaanzisha shughuli za kilimo. Kufuatia juhudi zake, Lunga aliinukia kuwa mkwasi. Hata hivyo wakazi wa Msitu wa Mamba walikumbwa na mzozo wa kijamii na tofauti za kitabaka. Sehemu hii ya Msitu wa Mamba ilikuwa inakaliwa na wakimbizi waliokuwa wamefurushwa kutoka maeneo mbalimbali.

Baadaye serikali iliwahamisha Lunga Kangata na wenzake kwenye Mlima wa Simba ambako iliaminika kulikuwa kwao. Lunga alikumbwa na ufukara na pia akakosa marafiki. Fidia aliyopewa na serikali haikutosha kuwalipia wanawe karo. Mkewe, Naomi, alipoona mambo yamewaendea mrama, alimwandikia ujumbe kwenye rununu na kumwambia kwamba ametorokea mjini kuzumbua riziki. Lunga alipatwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na mwaka mmoja baadaye, akaaga dunia. Naomi anasema;

> " .. nilipata hapakuwa nyumbani tena bali mahame yenye kaburi ambalo lilijikita ardhini kunikebehi kwa unyama niliowatendea nyinyi. Nilikifyeka kichaka cha magugu kilicholibana kaburi la maskini mume wangu..." (Matei, 2014:192)

Athari nyingine iliyowakumba waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii ni ubakaji wa watoto wa  kike. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, sanaa  iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, Ekuam (2006) anaeleza kuwa migogoro ya kijamii na kisiasa inapotokea, wale wanaoathirika mno ni watu wasio na uwezo katika jamii kama vil

watoto, wazee na wanawake. Wanawake huathirika kwa kukosa chakula, kupigwa, kubakwa na pia kuadimikiwa na huduma nyingine za kiafya.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), wahusika, Lime na Mwaliko, wameendeleza maudhui ya siasa na athari zake. Vita vilitokea katika nchi ya Wahafidhina baada ya Mwekevu Tendakazi kuibuka mshindi katika uchaguzi. Lime na Mwanaheri waliathirika kwa wabakwa na vijana mabarobaro watano waliovamia familia ya Mzee Kaizari na kumkata mkewe, Subira, kwa sime akazirai. Baadaye vijana hawa walifululiza hadi chumbani walimokuwa Lime na Mwanaheri na kuwabaka mbele ya baba yao pasiwe na wa kuwasaidia. Kaizari anasema;

> "Sijui ilikuwaje, lakini baada ya dakika chache nilijipata nje ya nyumba yangu, wanangu wawili wamezirai ubavuni mwangu..." (Matei, 2014:25)

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), Tamari Mapisi naye alinusurika kubakwa na vijana waliokuwa wakiandamana. Tamari alitorokea mstuni na kutembea mwendo mrefu kabla ya kuokolewa na wahisani. Ghasia za kisiasa na kijamii zilikuwa zimetokea nchini Kiwachema ambapo Wakorosho na Wakanju walikuwa wakipigana. Ni katika machafuko haya ambapo mhusika Tamari alinusurika kubakwa na genge la wapiganaji. Pam anasema;

> " Walijaribu kumnajisi akajinasua na kuwakwepa." (Walibora, 2003: 67-68)

Athari nyingine ya machafuko ya kisiasa na kikabila katika nchi ya Wahafidhina ni uharibifu wa mali. Ghasia hizi mara nyingi huchochewa na hali fiche ya masuala ya ugavi usiosawa wa ardhi katika maeneo mbalimbali ya nchi huska. Kama wanavyoeleza wanauhalisia kuwa, sanaa iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa

chuku, mtafiti alitambua kuwa vijana waliokuwa wakiandamana, walizua fujo, wakaharibu mali ya watu pamoja na kuteketeza mazao shambani. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), mmojawapo wa wahusika aliyeharibiwa mali yake ni Ridhaa. Jumba lake la kifahari liliteketezwa na waandamanaji likabaki kiunzi. Mwandishi anasema;

> Alipozinduka alijipata palepale katikati mwa kiunzi cha sebule ya lililokuwa kasri lake. (Matei, 2014: 37)

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), uharibifu mkubwa wa mali ulishuhudiwa wilayani Korosho baada ya vita kuzuka wilayani humo. Jamii ya Wakorosho na Wakanju walikumbwa na mizozo ya kijamii baada ya wao kuchochewa na viongozi wao. Matokeo ya uchochezi huu yakawa vita baina ya makabila haya huku mali nyingi ikiharibiwa. Akida, Tom na Tim walipokwenda wilayani Korosho kumzika Mzee Mangala aliyeuawa katika ghasia hizo, walishuhudia uharibifu mkubwa wa mali. Akida anasema;

> Mabaki ya nyumba zilizoteketezwa moto ndiyo mandhari yaliyolaki macho yangu. Kuta zilizogeuka nyeusi kwa masizi, zilisimama wima bila paa kama viwiliwili vya binadamu visivyokuwa na vichwa. (Walibora 2003: 93)

Kuchipuka kwa hali ya ukimbizi ni athari nyingine iliyosababishwa na ghasia za kisiasa na kijamii. Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), anaeleza kuwa watu walitorokea kambi za wakimbizi kujinusuru. Barabara za vijiji na miji zilijaa misongamano ya watu wakiwa na mizigo. Ridhaa na aila ya Kaizari ni baadhi ya wahusika waliosongamana katika kambi za wakimbizi. Hali hii inadhihirisha, uamilifu wa mhimili unaosema mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake, tulibaini kwamba kambi za wakimbizi zilikuwa na matatizo tele. Kulikuwa na ukosefu wa maji safi na misala.

Wakimbizi walitumia karatasi za plastiki kwenda haja kubwa na ndogo. Aidha kulikuwa na njaa pamoja na mlipuko wa magonjwa. Daktari Ridhaa na wenzake walikaa katika kambi za wakimbizi mpaka vita vilipokwisha ambapo baadaye walihamishwa kwenda katika Msitu wa Mamba. Kaizari anasema;

> Kadiri idadi ya wakimbizi ilivyozidi kuongezeka ndivyo hali ya maisha ilivyokuwa ngumu. Vijumba vichache tulivyovijenga havikutosha kuhimili idadi ya watu walioongezeka kila mawio. Huduma za kijamii ziliadimika. Ukosefu wa misala ulipelekea kuzaliwa kwa vyoo vya kupeperusha. (Matei, 2014:28)

Kutokea kwa ukimbizi vilevile kunadhihirika katika riwaya ya *kufa kuzikana* (2003). Ghasia za kisiasa na za kijamii zilikuwa zimezuka wilayani Korosho nchini Kiwachema. Makabila ya Wakanju na Wakorosho yalishambuliana. Katika machafuko haya, waja wengi walitoroka makwao kuenda mijini na katika kambi za wakimbizi kujinusuru. Jarida moja limeripoti kuwepo kwa ukimbizi katika nchi ya Kiwachema. Jarida hili liliandikwa kisiri mno kwani uchapishaji wa magazeti na majarida ulilikuwa umepiwa marufuku na serikali ya Kiwachema. Jarida linanukuu;

> Matokeo yakawa uharabu mkubwa. Kiwachema ikapata wimbi kubwa la ‘wakimbizi’ wa ndani kwa ndani ya nchi. Wengi wao wakikimbilia mijini na majijini. Barabara za miji ya kiwachema sasa zimejaa ombaomba mpaka zikatabika wengine. (Walibora 2003:160)

Athari nyingine ya ghasia za kisiasa na kikabila ilikuwa ni kusambaratika na utengano wa kifamilia. Utafiti uliofanywa na Cummings (2001), unadhihirisha kwamba kunapotokea

ghasia za kisiasa na kijamii, familia huathirika kwa namna mbalimbali. Familia zinazokumbwa na mitafaruku ya kijamii zinasawiriwa kuwa na migogoro ya hali ya juu na ukosefu wa mshikamano. Kutokana na hali kama hii familia nyingi hutengana huku nyingine zikiathirika ambapo watoto wanatelekezwa kutokana na kutokuwepo kwa wazazi wote au kuwepo kwa mzazi mmoja.

Mwandishi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, amebaini kuwa baadhi ya wahusika waliathiriwa kwa kutengana na jamaa zao. Mzee Sululu alitengana na mwanaye, Akida, hadi mauko yalipompata. Baada ya Akida kwenda jijini Tandika kuzawadiwa kama mmojawapo wa wanafunzi watatu bora katika mtihani wa kitaifa, vita vya kijamii na kisiasa vilizuka wilayani Korosho. Mzee Sululu alikuwa amebaki nyumbani katika kijiji cha Baraki naye mwanawe akashindwa kurudi nyumbani kutoka jijini Tandika. Akiwa huko kijijni, babake, Mzee Sululu aliuawa. Baadaye, Akida, alifanyiwa mpango wa kwenda kusomea nchini Canada na rafiki yake Tom Mangala. Akida anasema;

> Mbona ninalia tena? Naiacha nchi yangu ambapo mimi ni mwananchi kindakindaki. Naichukie nchi yangu Kiwachema? Ninalia kwa sababu naipenda nchi yangu. Nchi yangu inaniliza. Punde si punde tuliketi na kujifunga kanda za viti. Mashalla! Tuliruka angani kama tiara ilhali wahka umenijaa tele. (Walibora, 2003: 222)

Familia ya mzee Zablon Mapisi nayo inatengana kutokana na vita vilivyotokea wilayani Korosho. Wanawe, Tim na Tamari, walikuwa jijini Tandika vita vilipoendelea wilayani Korosho. Bintiye, Tamari, alitorokea jijini Tandika kumfuata nduguye baada ya yeye kukabiliwa na wapiganaji wa kisiasa na kijamii. Pam anaeleza;

> "... Ametembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa. Ameona maiti ngapi sijui? Ameona watu wakiuawa, mtoto mdogo pale alipo. Anasema alipata lifti kwa lori ya wafadhili wengine waliomleta mpaka hapa kwenye geti…" (Walibora, 2003: 68)

Mzee Zablon alisalia kijijini Nduchi akiongoza genge la wapiganaji ambapo baadaye mkewe na watoto wake wengine waliuawa katika ghasia hizo. Mwishowe, Mzee Zablon Mapisi alijitia kitanzi kwa sababu ya majuto ya kuwaua Wakanju na vilevile kwa kuangamia kwa familia yake.

Mwenda (2020), anasema kuwa wazazi wanapotengana ama familia inaposambaratika, watoto ndio huathirika mno. Anadai kwamba watotowanakosa malezi bora na mapenzi ya wazazi wao. Familia ya Mzee Sululu ilitengana kutokana na ghasia za kisiasa na kikabila zilizotokea wilayani Korosho. Ghasia zilizuka nchini Kiwachema ambapo makabila ya Wakorosho na Wakanju walipigana. Katika vita hivyo, watu wengi waliuawa, akiwemo,mzee Sululu, babake Akida .

Kifo cha Mzee Sululu kilimwacha Akida kuwa yatima. Alianza kufanya vibarua katika majumba ya watu kama vile kwa Mzee Muyaka ambapo alifanya kazi za nyumbani kwa miaka mitatu. Aliporudi jijini Tandika kutoka wilaya ya Sangura, alitiwa gerezani baada ya kujishitaki kwamba alikuwa amemshambulia mlevi mmoja aliyemfananisha na mzee Zablon Mapisi. Alipofunguliwa kutoka seli, aliandamwa na vijana waliotaka kumpiga kwa sababu alikuwa amemshambulia Tito Tembo katika danguro moja. Mwishowe Akida anabahatika kupata msaada wa kwenda nchini Canada kusoma. Rafikiye, Tom Mangala

alikuwa amemfanyia mpango wa kwenda kusomea nchini Canada kupitia kwa juhudi za mkewe, Jenelle.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya wahusika waliathiriwa na ghasia za kisiasa na kijamii na familia zao zikasambaratika kwa kutengana. Kama wanavyoeleza wanauhalisia kuwa, mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika ukawaida wake, utafiti huu ulibaini kwamba familia ya Lunga Kangata ni mojawapo ya familia ambazo zilisambaratika. Lunga Kangata alifurushwa kutoka Msitu wa Mamba hadi Mlima wa Simba kwa kile kilichodaiwa kuwa walikuwa wakiishi katika ardhi ambayo haikuwa yao. Kufuatia hali hii, maisha yalimbadilikia Lunga Kangata. Akakosa marafiki na hali ya umaskini ikamkumba. Wanawe waliosomea shule za kifahari wakaanza kusoma katika shule za kutwa. Mkewe, Subira,akamwandikia barua na kumwambia kuwa ametorokea mjini kutafuta riziki. Mwandishi anasema;

> Lunga alihisi kama aliyechomwa kwa joto la tanuri. Hili ni pigo la tatu kutoka kwa walimwengu. Tofauti ni kwamba hili linauma na kudhalilisha zaidi kwani Lunga alijisabilia kwa hali na mali kumpendeza mkewe. Kwamba analilipa penzi lake kwa kumwachia adha za malezi ni jambo ambalo Lunga hakuweza kulistahimili. (Matei, 2014: 81)

Kutoroka kwa Naomi kulisambaratisha familia ya Mzee Lunga Kangata kwani alimwachia ulezi wa watoto. Lunga alijaribu kutekeleza majukumu kama mama na baba lakini akalemewa na msongo wa mawazo. Lunga aliathiriwa na uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo akafariki.

Kutoroka kwa Naomi na kifo cha Lunga Kangata, kuliisambaratisha familia hii huku wanao wakibaki wametelekezwa. Watoto wa Lunga Kangata, Mwaliko, Umulkheri na Dickson wakapitia changamoto nyingi baada ya familia yao kusambaratika. Kijakazi wao, Sauna, aliwatorosha Dick na Mwaliko na kuwauza kwenda kulangua dawa za kulevya. Sauna alimuuza Mwaliko kwa Bi. Kangara ili atumike kulangua dawa za kulevya. Mwandishi anasema;

> Muda umepita tangu Sauna kuwatorosha Dick na Mwaliko. Amefanikiwa kumbadilisha Dick kwa kitita cha pesa. "Dick sasa ni mali ya Mzee Buda. Yatakayomfika ni yake na malaika wake," aliwaza Sauna siku alipomkabidhi Dick kwa Mzee huyu. (Matei, 2014: 155-156)

Bi. Kangara alipokamatwa na polisi, Mwaliko alipelekwa kwenye makao ya watoto ya kituo cha Benefactor kilichomilikiwa na watawa wa mtakatifu Teresia. Baadaye Mwaliko alichukuliwa na Mwangemi na Neema kama mtoto wao wa kupanga. Dickson naye alitoroshwa na Sauna na kuuzwa kwa Buda kulangua mihadarati. Alitumikishwa kusafirisha dawa za kulevya. Alinusurika mara nyingi kukamatwa na askari wa forodhani. Baada ya kupata fedha za kutosha, Dick aliacha biashara hii na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya kutengeneza simu.

**4.6 Umaskini**

Waandishi wa riwaya teule za Kiswahili wamebaini kuwa baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii wamekuza maudhui ya umaskini. Justino (2012), anasema kwamba baadhi ya watu hujihusisha na vita kwa sababu ya kuhiniwa nyenzo za kujiinua kiuchumi.

Kutokana na nadharia ya uhalisia katika mhimili unaosema; sanaa iwe ya kuaminika katika kuonyesha hali halisi, isiwe inatiwa chuku, mwandishi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003)*, ameonyesha baadhi ya waathiriwa walikumbwa naumaskini. Akida, Tim na Tamari waliendeleza maudhui ya umaskini kufuatia vita vya kisiasa na kijamii vilivyotokea nchini Kiwachema. Tim na Tamari walikuwa Wakorosho ilhali Akida alikuwa Mkanju. Makabila haya yaliizozana wilayani Korosho baada ya kuchochewa na viongozi wa kisiasa na kidini. Mbunge wa Korosho, mheshimiwa Johnstone Mabende, ni mmojawapo wa viongozi waliochochea Wakorosho kuwashambulia Wakanju.

Akida alipoenda jijini Tandika alikaa kwa Tim kwa muda kwa sababu kijijini mwao kulizuka vita vya kisiasa na kikabila vilivyochochewa na wanasiasa. Mjombake Tim, Samson Tungu, alipogundua kwamba Tim anaishi na Mkanju chumbani mwake alijawa na hamaki. Baadaye Tungu alimsimamisha kazi Tim kutoka kiwanda cha kusindika mafuta. Hali ngumu ya maisha iliwakabili Tim, Akida na Tamari. Tim aliuza kila kitu alichokuwa nacho chumbani mwake ili kulipia madeni pamoja na kugharamia mahitaji yao. Aidha, Tim alihama kutoka mtaa wa Milimani hadi mtaa wa Falkland. Mtaa huu ulikuwa wa walalahoi. Chumba kidogo alichopanga Tim, kilikosa vyombo na bidhaa muhimu vya kutumia. Aidha vijana hawa walifanya kazi za sulubu ili kujikimu. Akida anasema;

> Hapakuwa na nafasi ya kuzembea. Kila mtu alipaswa kuchangia kuzumbua riziki. Tim na mimi tukiraukia kila alifajiri kwenda kukoroga zege, kuchimba mitaro, kubeba magunia ya mazao sokoni, kusukuma rukwama, kufanya utopasi na kadhalika, muradi turejee nyumbani na chochote. (Walibora, 2003: 119)

Haya ni sawia na ufafanuzi wa nadharia ya uhalisia kuwa sanaa iwe inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake. Kwa mfano, Nyong'o (2001), anaeleza kuwa uongozi bora ndio mkakati bora wa kumaliza umaskini katika jamii. Kila msimu wa uchaguzi,wapiga kura hujitokeza kuwateua viongozi ambao watawawakilisha serikalini.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*, baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuza na kuendeleza maudhui ya umaskini. Wahusika hawa ni pamoja na Lunga Kangata, Mzee Kaizari na Kairu. Lunga Kangata alikuwa mkaazi wa Msitu wa Mamba. Baada ya kuachishwa kazi kutoka shirika la Fanaka, alihamia Msitu wa Mamba ambapo alijishughulisha na kilimo. Aliondokea kuwa tajiri mkubwa kutokana na faida aliyopata kutoka kwa kilimo hicho. Hata hivyo, Msitu wa Mamba, ulikumbwa na vujo zilizotokana na tofauti za kitabaka na kiusuli. Kupitia utafiti huu tulibaini kwamba sehemu hii ilisheheni wakimbizi waliotoka maeneo tofauti tofauti. Mizozo hii ilipokithiri, chama tawala kiliwahamisha Lunga Kangata na wenzake hadi Mlima wa Simba. Hali ya ufukara ilimkabili Lunga. Fidia aliyopewa na serikali haikumwezesha kulipia karo za wanawe. Mwandishi anasema;

> Alikumbuka mali yake ambayo aliichuma kwa viganja vyake katika Msitu wa Mamba. Sasa ameipoteza. Ameyapoteza maisha yake, amewapoteza ndugu na marafiki zake. Wanawe waliosomea katika shule za kifahari, sasa fidia aliyopewa na serikali haitoshi hata kuwapeleka katika shule za watu wa kima wastani. (Matei, 2014:79)

Mhusika mwingine aliyekuza na kuendeleza maudhui ya umaskini katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)* ni Kairu. Vita vilipozuka katika nchi ya Wahafidhina, Kairu na mamake walifurushwa kutoka makazi yao. Wakiwa njiani kuelekea maeneo salama, ndugu yake mdogo aliathiriwa na maradhi ya mabafu. Kitoto hiki kilifariki na mamake akakizika katika kaburi la kina alilolichimba kichakani. Baadaye, Kairu, mamake na ndugu wengine walipelekwa katika kambi za wakimbizi. Vita vilipokwisha, mamake Kairu alirejelea biashara ya kuuza samaki. Matokeo ya mzozo huo yakawa masikitiko kwa familia nyingi; mamake Kairu akakosa karo ya shule na ikabidi azungumze na mwalimu mkuu amruhusu alipe kidogo kidogo hadi mwisho wa mwaka . Kairu anasema;

> Kwa mtu maskini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzishia biashara nyingine, maisha yamekuwa magumu zaidi. (Matei, 2014: 93)

Aidha, Bwana Kaizari ni mwathiriwa mwingine aliyekuza na kuendeleza maudhui ya umaskini katika riwaya teule ya Kiswahili. Vita vilipoisha, Mzee Kaizari na familia yake walirudishwa katika Msitu wa Mamba ambapo waliishi kwa muda. Baadaye, mizozo ilianza kutokea kwa sababu ya tofauti za kitabaka na kiusuli. Mizozo hii ilipokithiri, Kaizari na Wenzake walihamishwa kutoka msitu huo hadi Mlima wa Simba. Kaizari alijenga nyumba kufu yake pale katika ganjo la nyumba zilizokuwa zimeteketezwa vita viliposhuka katika nchi ya Wahafidhina. Wanawe, Lime na Mwanaheri wakarudi shuleni pale kijijini. Mzee Kaizari aliendelea kuishi maisha ya kimaskini hadi Daktari Ridhaa alipojenga kituo afya cha Mwanzo Mpya. Alimwajiri Kaizari kama afisa wa matibabu. Mwanaheri anasema;

> "Baada ya kurudishwa nyumbani kutoka Msitu wa Mamba, baba yangu, Mzee Kaizari, aliweza kuyajenga maisha yetu upya. Alijenga nyumba kufu yetu pale pale penye lile ganjo," (Matei, 2014: 93)

### 4.7 Elimu

Kwa mujibu wa Millet (1969), elimu ndiyo humpa binadamu nguvu ya kujiendeleza. Elimu huwasaidia vijana katika kuona uhalisia wa maisha na kujijenga kimaadili na kuwa na utu wema. Meyer (1977) anasema kwamba elimu huwawezesha watu kujikomboa kimawazo na kuwafanya wajitegemee. Utafiti huu umebaini kwamba baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuza na kuendeleza maudhui ya elimu. Wahusika hawa walikuwa wamepata viwango mbalimbali vya elimu katika shule na vyuo.

Msimamo wa mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri (2014)* kuhusu elimu ni kwamba elimu ndiyo silaha ya kumletea mtu mabadiliko. Wanauhalisia wanaamini kwamba, fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka. Elimu inaweza kumpandisha mtu ngazi akawa mmiliki wa mali au kiongozi mashuhuri. Daktari Ridhaa ni mmojawapo wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa na elimu ya kiwango cha juu iliyomwezesha kujiendeleza na kuihudumia jamii katika vitengo mbalimbali.

Daktari Ridhaa alitia bidii masomoni na akahitimu shahada ya uzamili katika taaluma ya udaktari. Hii ilitokana na ushauri wa mamake na walimu wake shuleni. Baada ya kuhitimu masomoni, alifanya kazi katika mashirika mbalimbali yanayohusiana na taaluma ya afya.

Ridhaa anajenga na kuendeleza maudhui ya elimu katika riwaya teule ya utafiti. Ridhaa anasema;

> "... Hapa nilipo nina uzoefu mkubwa katika utabibu. Nimewaokoa wagonjwa wengi kutokana na magonjwa sugu. Nimewatoa wengi mikononi mwa Izirail..." (Matei, 2014:56)

Vita vilipokwisha na mwanawe kurudi kutoka ughaibuni, Ridhaa alijenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Katika hospitali hii, aliwaajiri Kaizari na Selume kama wahudumu. Kaizari aliajiriwa kama afisa wa matibabu huku Selume akiwa muuguzi mkuu. Kupitia kwa elimu aliyoipata Ridhaa, alikuza maudhui ya elimu.

Mhusika mwingine ambaye alikuwa amepata elimu ya chuo ni Kaizari. Mwandishi anaeleza kwamba, baada ya vita kuisha, Kaizari aliajiriwa kazi katika kituo cha Mwanzo Mpya. Kaizari alifanya kazi kama afisa wa matibabu na aliweza kuwahudumia wagonjwa kwa juhudi kubwa. Ni kutokana na elimu aliyokuwa nayo ndipo aliweza kuajiriwa kama afisa wa matibabu. Mwandishi ananukuu;

> Selume na Kaizari waliomba kazi, Selume akaajiriwa kama muuguzi mkuu, naye Kaizari kama afisa wa matibabu. Huu ni mwaka wa tatu tangu kuanza kazi hapa chini ya usimamizi wa Ridhaa ambaye ndiye mkurugenzi. Yeye na Kaizari hawaachi kumshukuru Ridhaa kwa kujenga kituo hiki. (Matei, 2014:141)

Mwangeka aliyeathirika na ghasia za kisiasa na kijamii alikuwa msomi. Mwangeka alikuwa mtoto wa kiume wa Daktari Ridhaa na Bi. Terry. Mwangeka alisomea taaluma ya uhandisi. Baada ya kuhitimu masomo, alijiunga na kikosi cha wananamaji; kikosi

kilichoshughulika na kudumisha usalama wa nchi. Kutokana na juhudi zake, Mwangeka aliweza kupandishwa vyeo katika kikosi hiki hadi alipoelekea katika mataifa ya ughaibuni kudumisha amani. Mwandishi anasema;

> Baada ya kipigo hiki cha babake, Mwangeka aliapa kuwajibika zaidi. Aliinamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. (Matei, 2014: 61)

Mwangeka akiwa ughaibuni, aliwajibika kazini walipokuwa wakidumisha usalama. Vita vilipozuka nchini mwao, mkewe, Lily Nyamvula, na mwanawe, Becky, waliteketezwa motoni na genge la waandamanaji.

Wahusika wengine walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii ambao walikuwa wamepata elimu katika riwaya hii ni Umulkheri, Dickson na Mwaliko. Wahusika hawa walikuwa watoto wa Lunga Kangata na Bi. Naomi. Baada ya ufukara kumkumba Lunga Kangata, mkewe Bi. Naomi alimtoroka mumewe kwa kizingizio kuwa anaenda mjini kutafuta chochote cha kumsaidia mumewe. Kutokana na kitendo hiki, Lunga alishikwa na kihoro ambacho kilimsababishia ugonjwa wa mogo akafariki.

Umulkheri alisomeshwa na baba wa kupanga, Mwangeka, akahitimu masomo yake katika taaluma ya uhandisi katika masuala ya kilimo. Hapo awali alisomea katika shule ya upili ya Tangamano iliyokuwa inawafundisha watoto mayatima. Mwalimu Dhahabu alimsaidia Umulkheri kwa kumtafutia wazazi wa kupanga ambao wangempa malezi na mapenzi ya wazazi. Mwalimu Dhahabu alimpeleka Umulkheri kwa rafiki yake wa utotoni, Mwangeka. Mwangeka alikuwa amemwoa Rachael Apondi kama mke wa pili baada ya mke wa kwanza kuaga. Mwangeka na Apondi walikuwa na watoto wawili, Sophie na Don Ridhaa. Wazazi

hawa walimlea na kumsomesha Umulkheri hadi akahitimu shahada katika taaluma ya uhandisi. Umulkheri anasema;

> Usiku nilipotoka Mlima wa Simba nilijua kuwa maisha yangu yameingia katika mkondo wa maangamizi. Nilidhani kuwa huo ndio uliokuwa mwisho wa masomo yangu. Sikuotea kukamilishi hata kidato cha pili. Lakini nitazameni hapa nilipo. Nina familia. Nina shahada ambayo nyinyi wenyewe ndio mlioidhamini. Ndugu yangu huyu, Dick, ameweza kujiendeleza kimasomo kwa msaada wenu. (Matei, 2014:172)

Mwaliko na Dick ni waathiriwa wengine wa ghasia za kisiasa na kijamii waliokuwa na elimu ya chuo. Baada ya Mwaliko kutoroshwa na Sauna kutoka kwao, aliokolewa na maafisa wa polisi kutoka kwa Bi. Kangara aliyekuwa akiwatumia watoto kulangua dawa za kulevya. Mwaliko alilelewa na kuelimishwa katika kituo cha Benefactor. Utafiti huu, ulibaini kwamba Mwaliko alichukuliwa kama mtoto wa kupanga wa Mwangemi pamoja na mkewe Neema. Neema hakuwa na mtoto kwani kila alipojifungua, mtoto alikufa kwa ugonjwa wa selimundu.  Alipompanga Mwaliko, alimlea na kumwelimisha hadi kiwango cha uzamili. Mwandishi anasema;

> Miaka mitatu imepita baada ya Mwaliko kukamilisha masomo yake ya chuo kikuu. Amejisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu. Ameajiriwa na kampuni ya magazeti ya Tabora kama mhariri katika kitengo cha biashara. Mwaliko anaifanya kazi yake kwa bidii ya mchwa. (Matei, 2014: 168)

Dick, naye amechangia kukuza na kuendeleza maudhui ya elimu katika riwaya ya *Chozi la Heri (2014)*. Baada ya mamake, Naomi, kutoroka na babake, Lunga Kangata, kufariki,

Dick alitoroshwa na kijakazi wao, Sauna. Aliuzwa kwa Bwana Buda ambaye alimtumia kulangua mihadarati. Dick aliacha biashara hiyo akaanzisha biashara ya kuuza vifaa vya kutengeneza simu na vyombo vya mawasiliano. Aidha kwa usaidizi wa Mwangemi, Dick alijisajili katika stashahada ya mawasiliano. Masomo yake yalimwezesha kufanikiwa katika biashara. Umulkheri anasema;

> " Ndugu yangu huyu, Dick, ameweza kujiendeleza kimasomo kwa msaada wenu. Sasa anajitegemea. Sina cha kuwapa nyinyi. Nawaombea thawabu za Mungu."(Matei, 2014: 172)

Dick aliondokea kuwa mfanyabiashara mashuhuri katika biashara ya kuuza na kutengeneza bidhaa za TEKNOHAMA. Biashara hii ilibuni nafasi za kazi kwa vijana ambao wangekuwa mawindo rahisi ya wahalifu.

Kairu ni mwathiriwa mwingine wa ghasia za kisiasa aliyekuwa mwanafunzi katika shule ya upili ya Tangamano. Familia yake iliathirika na ghasia zilizotokea katika nchi ya Wahafidhina. Vita vilipokwisha nchini humo, Kairu alirudishwa katika shule ya Tangamano. Kama unavyoeleza mhimili wa nadharia ya uhalisia, sanaa inamulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake, tulibaini kuwa mamake alikuwa mfanyabiashara wa kiwango cha chini. Alikuwa muuza samaki na biashara hiyo ilikuwa imeathirika kufuatia mizozo ya umiliki wa maji na ardhi ya ziwa. Karo ya kumlipia Kairu ilikuwa ngumu na ikabidi mamake azungumze na mwalimu mkuu ili aweze kulipa karo kidogo kidogo hadi mwisho wa mwaka. Babake Kairu hakumlipia karo kwani alidai kwamba Kairu hakuwa mtoto wake halisi, alikuwa mtoto wa kupanga. Kairu anasema;

> "...Mara mojamoja nimewahi kumuuliza mama kwa nini asimwombe baba, ambaye nasikia ni mwenye chake na lake, anilipie karo. Hata hivyo, mama huwa hanijibu, anachonipa ni mtazamo unaouliza swali..." (Matei, 2014: 93)

Naomi, mkewe Lunga Kangata, ni mwathiriwa mwingine aliyekuza na kuendeleza maudhui ya elimu. Naomi alikaa katika mji wa Karaha kwa muda huku akifanya kazi za sulubu. Aliajiriwa kwa Bwana Kimbaumbau ambaye alianza kumdhulumu kijinsia. Baadaye, Naomi aliacha kazi ya kuuza nguo kuukuu. Stashahada aliyokuwa nayo ya uhazili hakuwa amefaidika kupata nayo kazi nzuri ya kumsaidia. Alikuwa na matarajio kwamba hali yake ya kiuchumi ikiimarika angerudi katika mlima wa Simba kumsaidia mumewe. Mwandishi anasema;

> Kile ambacho Mwangeka hakujua ni kwamba Bi. Naomi, baada ya kurudi kwao, hakuishi na wazazi wake. Uso una haya ati! Alijiambia kwamba atatumia stashahada yake ya uhazili kutafuta kazi huko huko adunduize pesa kidogokidgo. (Matei, 2014: 191)

Hata hivyo baada ya kuacha kazi ya Bwana Kimbaumbau, alirudi katika Mlima wa Simba ambapo alipata kwamba mumewe alikuwa ameaga dunia na wanawe asijue waliko. Alipanda maua katika kaburi la mumewe kisha akaendelea kuwatafuta wanawe; Umu, Dick na Mwaliko.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana (2003),* baadhi ya waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuwana viwango mbalimbali vya elimu ambavyo viliwawezesha kujiendeleza kimaisha na pia kuhudumu katika nafasi mbalimbali. Kupitia utafiti huu, tulibaini kwamba

Tom Mangala, Jenelle Mangala, Mwalimu Alex, Tim, Tamari, mzee Sululu na Akida ni baadhi ya wahusika ambao viwango vyao vya elimu vimewekwa bayani.

Tom Mangala alikuwa mtoto wa pekee wa Mzee Mangala kutoka kijiji cha Baraki wilayani Korosho. Kwa mujibu wa mwandishi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), Tom alikuwa amefuzu vyema katika masomo na akapata ufadhili kwenda kusomea shahada ya uzamili nchini Marekani. Baada ya kuhitimu masomo, Tom alirejea nyumbani na mke mzungu; Jenelle. Kijijini mwao, Tom alikuwa simulizi kwa wengi kwa sababu ya kitengo chake cha elimu na vilevile kitendo chake cha kumuoa mke mwenye asili ya kizungu. Mwandishi anasema;

> Mradi Tom alikuwa simulizi kwetu kijijini. La kwenda ng'ambo kusoma ni jambo la namna yake kwa watu wa kwetu, kaifa ya kumwoa au kuolewa na Mzungu. (Walibora, 2003: 80)

Tom aliajiriwa katika shirika moja lisilo la kiserikali liitwalo Anken. Aliweza kutumia pesa alizopata kujiendeleza kabla ya vita vya kijamii na kisiasa kuzuka wilayani Korosho. Alimjengea babake, Mzee Mangala, jumba la kifahari na pia akajenga majumba yake mawili ya kifahari. Jumba moja alijenga nyumbani kwao Baraki huku lingine akajenga katika mtaa wa Milimani jijini Tandika.

Mzee Sululu, babake Akida, alikuwa na masomo ya gumbaru. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia, wahusika wasawiriwa kama walivyo katika jamii, tulibaini kwamba Sululu alitumia masomo yake kutunga diwani ya ushairi iitwayo *Kero za Mkiwa*. Aliandika kitabu hiki licha ya kuwa na kiwango cha chini cha elimu, masomo ya gumbaru. Diwani hii ilichapishwa na kampuni ya uchapishaji ya Hatubaguani. Sululu anasema;

> “Tafuta ofisi za Hatubagui Publishers,” aliongeza. “Kaniulizie mhariri wa Kiswahili, au meneja wa uchapishaji wamefikia uamuzi gani kuhusu mswaada wa diwani yangu. Waulize kwa nini wanakawia na miswaada ya watu hivyo. Nitakufa jamani bila kukiona kitabu changu cha mashairi kwenye chapa?” (Walibora, 2003: 11)

Akida naye alikuwa amekamilisha masomo ya darasa la nane na alikuwa miongoni mwa wanafunzi tatu bora katika mtihani wa kitaifa nchini Kiwachema. Kufuatia matokeo haya, Akida alisafiri kwenda jijini Tandika katika makao makuu ya wizara ya elimu kuzawadiwa na waziri wa elimu, Bwana Kato. Hata hivyo, Akida hakuweza kuendelea na masomo ya shule ya upili kwani vita vilizuka wilayani Korosho na ufadhili wa masomo yake ukapotea. Mwishoni mwa riwaya hii tunaelezwa kwamba, Tom Mangala, alimfanyia Akida mpango akasafiri kwenda nchini Canada kusoma. Tom alisema;

> “N’takufanyia mpango uje usomee Canada. Wewe ni mtu mwenye vipawa. Vitapotea bure hapa. Nani anajali mtu mwenye vipawa hapa? Vinaoza na kuozeana tu kwenye mabua shambani.” (Walibora, 2003: 101)

Halikadhalika, Tamari Mapisi alikuwa mwanafunzi katika shule ya msingi ya Baraki vita vilipotokea wilayani Korosho. Alitoroka kutoka kwao Korosho, akanusurika kunajisiwa na waandamanaji. Utafiti huu ulitambua kwamba Tamari alisafirishwa hadi jijini Tandika ambako alistakimu na nduguye;Tim Mapisi. Vita vilipokwisha, Tim alimrudisha Tamari katika Shule ya Mumbaimbai alipoanzia masomo katika darasa la sita akaendelea na masomo hayo hadi shule ya upili. Tim anasema;

> “Nilipata kazi kule Anken,” aliendelea Tim. “Kule alikokuwa akifanya kazi Tom. Basi nikaamua kumrudisha dadangu shuleni. Anasoma shule ya kutwa ya Mumbaimbai hapa jijini.” (Walibora, 2003: 194)

Mwandishi anaeleza kwamba, Akida aliporejea kutoka wilaya ya Sangura alipokuwa ametorokea, baada ya kutoka gerezani, alipata Tamari amefikia kidato cha pili shuleni.

## 4.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia jinsi ambavyo waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyokuza na kuendeleza maudhui katika riwaya teule za Kiswahili. Baadhi ya maudhui waliyokuza na kuendeleza ni pamoja na Tatizo la ubaguzi wa kimbari na kikabila, nafasi ya vijana katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, siasa na athari zake, umaskini na elimu. Sura inayofuata inashughulikia muhtasari, matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mapendekezo, mchango na changamoto za utafiti. Utafiti huu ulihusu usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Lengo la pili lilikuwa kuchunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* (2003) na *Chozi la Heri* (2014). Lengo la tatu lilikuwa kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kikabila katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umegawika katika sura tano. Sura ya kwanza iliangazia masuala ya kimsingi ya utafiti. Sura hii ilielezea usuli wa utafiti ambao uliweka msingi wa utafiti tuliofanya ambao unahusu usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Masuala mengine yaliyojadiliwa katika sura ya kwanza ni suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti. Aidha, yaliyoandikwa kuhusu mada yamefafanuliwa na kubaini mchango wa utafiti wetu. Halikadhalika, tulijadili msingi wa nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilihusu kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana (2003)* na *Chozi la Heri (2014)*. Mtafiti alibaini waathiriwa akitumia vigezo mbalimbali kama vile utabaka, jinsia, elimu, taaluma na hadhi za ndoa. Aidha, aliwabaini waathiriwa wengine kwa kigezo cha umri, uongozi na wale wenye matatizo ya kiafya. Katika kuwabaini wahusika katika vigezo hivi, mhimili unaeleza kuwa fasihi inapaswa kueleza ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii na sio vile msanii anataka yawe ulitumika. Aidha mhimili unaoeleza kuwa msanii kumulika maisha halisi ya jamii katika mazingira yake ulitumika. Vilevile mhimili unaoeleza kuwa mtunzi kutumia mandhari asili na kuyaendeleze katika hali ya ukawaida wake ulitumika. Mhimili wa mwisho uliotumika kubaini waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii ni ule unaofafanua kwamba mtunzi anapaswa afanye utafiti juu ya yale anayotaka kuandika ili aweze kuandika ukweli unaokubalika kifasihi.

Sura ya tatu ilihusu kuchunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Tuliwasawiri waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii kwa njia mbalimbali. Kuna waathiriwa walisawiriwa kama watu waliokata tamaa huku wengine wakisawiriwa kama wachochezi na wenye matatizo ya kisaikolojia. Aidha, kuna waathiriwa wengine waliosawiriwa kama wakimbizi, wajane na mayatima. Baadhi ya wahusika walisawiriwa kama watu wenye  chuki na madharau. Mhimili uliotumika katika kuchanganua usawiri wa waathiriwa ni ule unaosema  kuwa wahusika wasawiriwe kama walivyo katika jamii miongoni mwa mihimili mingine.

Sura ya nne ilitathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathiriwa wa ghaia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za kiswahili. Maudhui yaliyokuzwa ni kama vile ubaguzi wa kimbari na kikabila, nafasi ya vijana na nafasi ya mwanamke katika jamii. Vilevile maudhui ya siasa, elimu na umaskini yalijadiliwa. Mhimili wa nadharia ya uhalisia uliotumika katika sura hii ni ule unaoeleza kuwa mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake. Pia mhimili unaoeleza kuwa sanaa imulike maisha halisi ya jamii katika mazingira yake ulitumika miongoni mwa mihimili mingine.

Sura ya tano inahusu muhtasari, matokeo, mapendekezo, mchango na changamoto za utafiti. Muhtasari umeeleza yaliyomo katika sura mbalimbali za utafiti. Matokeo nayo yameonyesha ni data ipi iliyotumika katika kila sura na ilichanganuliwa vipi. Aidha sura hii imeeleza mchango wa utafiti, changamoto za utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Uhakiki huu ulichunguza usawiri wa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana (2003)* na *Chozi la Heri (2014)*. Uhakiki wa riwaya hizi umedhihirisha kwamba suala la ghasia za kisaiasa na kijamiis ni suala nyeti ambalo linahitaji kuzingatiwa kwa uzito na wanajamii. Katika kufanikisha matokeo ya utafiti huu, tuliongozwa na malengo matatu. Uchunguzi wetu uliongozwa na mihimili teule ya nadharia ya uhalisia.

Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana (2003)* na *Chozi la Heri (2014)*. Lengo hili lilitimizwa kwa sababu tulibaini wahusika walioathirika na ghasia za kisiasa na kijamii kwa kutumia vigezo

mbalimbali. Baadhi ya waathiriwa walibainishwa kwa misingi ya matabaka yao, ambapo kulikuwa na wahusika wa tabaka la juu na wa tabaka la chini. Wengine walitambuliwa kwa kigezo cha jinsia ambapo jinsia ya kike na kiume zilibainishwa. Kigezo cha elimu kilitumika kubaini waathiriwa wengine ambapo ilibainika kuwa, kulikuwa na wahusika waliokuwa wasomi. Wahusika wengine walibainishwa kwa kigezo cha umri ambapo kulikuwa na wahusika wazee, wahusika wa umri wa makamo, wahusika vijana na wahusika watoto. Aidha, tulitambua waathiriwa wengine kwa kigezo cha uongozi ambapo kulikuwa na viongozi wa kidini na wa kisiasa walioathirika. Utafiti huu pia uliwatambua waathiriwa kwa misingi ya taaluma na ndoa. Kitaaluma kulikuwa na walimu, madaktari na wauguzi, wahandisi na wanasheria. Aidha katika kigezo cha ndoa, baadhi ya waathiriwa walikuwa wanandoa. Mwisho, mtafiti aliwatambua waathiriwa waliokuwa na matatizo ya kiafya ambao walikuwa na magonjwa ya akili.

Lengo la pili lilikuwa kuchunguza namna waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii walivyosawiriwa katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003)*. Utafiti huu ulitimiza lengo hili kwa kuonyesha namna waathiriwa hawa walivyosawiriwa. Kuna waathiriwa waliosawiriwa kama watu waliokata tamaa huku wengine wakisawiriwa kama wachochezi. Wahusika wengine walisawiriwa kama watu wenye matatizo ya kisaikolojia na wengine kama wakimbizi. Matatizo ya kisaikolojia yalitokana na kuwa na mawazo mengi kufuatia changamoto walizokumbana nazo. Ukimbizi nao ulitokana na wale waliofurushwa kutoka maeneo yao na kutorokea kwenda katika mahali salama. Kuna waathiriwa waliosawiriwa kama mayatima, watu wenye madharau na chuki. Mayatima ni

wale waliofiwa na wazazi wao kufuatia vita vya kisiasa na kijamii vilivyotokea katika mataifa ya Kiwachema na Wahafidhina.

Lengo la tatu lilikuwa kutathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Kufa Kuzikana (2003)* na *Chozi la Heri (2014)*. Lengo hili lilitimizwa kwa kubainisha maudhui mbalimbali yaliyokuzwa na kuendelezwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule za kiswahili. Tulitathmini maudhui kama ubaguzi wa kikabila na kimbari, nafasi ya vijana katika jamii na nafasi ya mwanamke katika jamii. Waathiriwa wengine wa ghasia za kisiasa na kijamii walikuza maudhui kama vile maudhui ya siasa, maudhui ya umaskini na maudhui ya elimu.

## 5.3 Mapendekezo

Katika utafiti huu, tumewabaini waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kikabila katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Katika kuwabaini waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii, tulitumia vigezo mbalimbali kama vile matabaka yao, viwango vya elimu, hadhi ya ndoa, taaluma na ajira, viongozi na wasomi. Tunapendekeza utafiti ufanywe kuchunguza sifa za waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya teule. Utafiti huu vilevile umewasawiri waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Waathiriwa hawa wamesawiriwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile wahusika waliotamauka, wakimbizi, wachochezi, wajane na mayatima, wenye madharau na chuki, wenye matatizo ya kisaikolojia miongoni mwa usawiri mwingine. Tunapendekeza utafiti ufanywe kuchunguza namna mwandishi

alivyowatumia waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii kukuza mtindo na fani katika riwaya teule za Kiswahili.

Aidha, katika utafiti huu tulitathmini maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri* (2014) na *Kufa Kuzikana* (2003). Baadhi ya maudhui yaliyoendelezwa na waathiriwa wa ghasia za kisiasa na kijamii ni kama maudhui ya umaskini, siasa, nafasi ya vijana katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii na elimu. Tunapendekeza utafiti ufanywe kuchunguza namna mandhari yalichangia kukuza maudhui katika riwaya teule za Kiswahili.

**5.4 Mchango wa Utafiti**

Utafiti huu ulibaini kuwa migogoro ya kisiasa na kijamii hutatiza shughuli za masomo katika jamii. Hivyo basi, Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa kuongezea hazina ya usomi wa fasihi. Hii ni kwa sababu utafiti huu utakuwa kazi ya marejeleo kwa wataalamu, wasomi na wahakiki wa fasihi. Aidha, utafiti huu utawafaidi wakuza mitaala ya Kiswahili kwa sababu utafiti huu umeshughulikia suala la ghasia za kisiasa na kijamii ambalo ni suala nyeti linalopaswa kufunzwa katika mtaala wa shule na vyuo.

Aidha, matokeo ya uhakiki huu yatawafaa wahakiki wa masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwani umechanganua athari za vita vya kisiasa na kijamii. Wanajamii wanapoelewa mambo haya, watakuwa makini kunapotokea ghasia za kisiasa na kijamii na kujiepusha na ghasia hizo.

Pia, utafiti huu utawasaidia wasomi na watafiti wa Kiswahili ili waweze kutafiti na kuandika kuhusu masuala yanayoathiri jamii kama vile chuki za kikabila pamoja na ghasia za kisiasa na kijamii. Kupitia kwa utafiti huu na tafiti zingine zinazohusu mada ya utafiti huu, wanajamii watahamasishwa kuishi kwa amani na mshikamano.

**5.5 Changamoto za Utafiti.**

Mchakato wa utafiti huu ambao unahusu usawairi wa waathirwa wa ghasia za kisiasa na kijamii katika riwaya za *Chozi la Heri (2014)* na *Kufa Kuzikana (2003)* ulikumbwa na changamoto kadhaa. Utafiti huu ulifanywa maktabani. Mojawapo ya changamoto zilizokumba utafiti huu ni mlipuko wa UVIKO-19 (ugonjwa wa virusi vya korona-19) ambapo maktaba zote nchini zilifungwa ili kuzuia maenezi ya ugonjwa huu. Mtafiti mara nyingi alisoma maktaba ya mtandaoni. Kutangamana na wasimamizi wa mtafiti kulikuwa na changamoto kwani ilibidi mawasiliano na maelekezo yafanywe kupitia kwa njia ya mitandao na simu. Mawasiliano yaliweza kutatizika kutokana na changamoto za nguvu za umeme, changamoto za mtandao wa 'zoom' na vilevile wavuti.

Aidha kulikuwa na uhaba wa vitabu vya Kiswahili vinavyoeleza kuhusu ghasia za kisiasa na kijamii. Tatizo la ukosefu wa vitabu vya Kiswahili lilitatuliwa kwa mtafiti kutafsiri vitabu kutoka lugha ya Kingereza kuja kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, matatizo haya hayakuathiri matokeo yaliyowasilishwa na mtafiti.

## 5.6 Hitimisho

Kupitia uhakiki huu tumebaini kuwa, wahusika wa aina mbalimbali waliathirika kufuatia ghasia za kisiasa na kijamii zilizotokea katika riwaya teule za Kiswahili. Watunzi wa riwaya hizi wamewasawiri waathiriwa wa ghasia kwa vigezo mbalimbali kutegemea na hali wahusika hawa walizokuwamo. Tumetambua kwamba, utanzu wa riwaya hutumiwa kusawiri matatizo yanayoikumba jamii na hasa yale yanayohusiana na mabadiliko ya kisiasa katika mataifa yanayoendelea. Kwa kutumia utanzu wa riwaya, watunzi wanaweza kuweka wazi matatizo yatokanayo na ghasia za kisiasa na kijamii na hivyo kukuza jamii yenye amani na maridhiano licha ya tofauti za mirengo ya kisiasa.

## MAREJELEO


Becker, E. (2011). "Youth Rights in The Kenyan Constitution. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Uppsala Sweden. (Haijachapishwa)

Bell, F. (1977). *Marxist Theory, Class Struggle and The Crisis of Capitalism*: The Santa Monica: Goodyear.

Brady, D. (2018). *Theories of Causes of Poverty*. California: University of California.

Chumbow, B.S. (1987). *Towards a Language Planning Model for Africa.* Journal of West African Languages XVII/I: 15-22

Cummings, E. na Davies, P. (1994). Marital Conflict and Child Adjustment: An Emotional Security Hypothesis.In: *Psychology Bulletin,* 116(3) pp: 37-411

Dombrowski, N. A. (Ed.). (2005). *Women and war in the Twenthieth century: Enlisted with or Without consent***.** London: Routledge.

Ekuam, E. D.(2006). Conflicts, Conflict Resolution and Peace Building: The Role of Pastoral Women. *In: Creighton, C. S.F Yieke, J. Okely, L. Mareri and C. Wafula (eds.).* Gender Inequalities in Kenya.UNESCO

Enon, J.C. (1998). *Educational Research: Statistics and Measurements.* Kampala. Makerere university press.

Erikson, E. (1959). *Identity and The Life Cycle*. New York: Norton.

Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke Katika riwaya ya Utengano na Kamwe Si Mbali Tena. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Felman, S. (2003). *Writing and Madness*.California: Stanford University Press.

Gachukia, D. (2005). Government by Tribe or Government by Political Parties? In Wanjohi, G. J. and Wanjohi, G.W.(Eds). *Social and Religious Conerns of East Africa*, Uk. 101-107

Gahnstrom, C. (2012). *Ethnicity, Religion and Politics in Tanzania: The 2010 General Elections in Mwanza Region*. Helsink University: Helsink University Press

Gastil, D. (1985). *Freedom in the world: political Rights and Civil Liberties 1984-1985. West Port***,** CT: Greenwood Press.

Haji, Ali Vuai (2018). Kutathmini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu: Utafiti Linganishi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.(Haijachapishwa)

Hemed, S. (2018). Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya yaMfadhili.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Hill, J. S. (1977). *The Romantic Imagination. London*: Macmillan Press Ltd

Hogan, P. (2003). *The mind and its stories: Narrative Universals and Human Emotion***.**

Justino, P. (2012). *War and Poverty*. London: Micron Publishers.

Kasomo, D. (2006). *Research Methods in Humanities and Education*. Egerton: Egerton University Press.

Khadijat, K. R. (2003). Ethics *Politics and Ethnic Conflict*. Cambridge: Cmbridge University Press.

Kierkgaad S, (1843). *Fear and Trembling*. Denmark: Pseudonymous.

Kohrs–Amissah, (2003). *Aspect of Feminist and Gender in the Novels of Three West African Women Writers (Aidoo, Emecheta, Darko)***.** Heidelberg: Books on African Studies.

Kothari, R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. (Second Revised Edition). New Delhi: New Age International Publishers.

Lukacs, G. (1962). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

Lyatuu, J. (2011). “Usawiri wa Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa Kike na Kiume: Uchanganuzi katika Riwaya Teule,” Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

M’Ngaruthi, T. K. (2015). Usawiri wa Mwanasiasa wa Afrika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Chuka.(Haijachapishwa)

Mackenzie, P. (2014). *Psychopathy, Antisocial Personality and Sociopathy: The basics, Historical Review***.** Illinois: The Forensic Examiners. 53/1, 198-207. Dar es Salaam: TUKI.

Magnarella, P. (1994). *Explaining Rwanda’s 1994 Genocide in: Areview of Mahmood Mamdanii, when victims Become Killers: colonialism, Navitism and the Genocide in Rwanda.* Princeton, N.J: Princeton University Press, 2001. Pp. 364.

Mandela, N. R. (1994). *Long Walk to Freedom*. London: Abacus.

Maobe, (2011). Ukombozi wa Mwanamke Katika Riwaya za Habwe. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Marx K. (1983). *Alienated Labour*: The Portable Karl Marx (E. Kamenta, ed.). New York: Penguin Press

Masaku, G. M. na Kilonzo, P. K. (2018). *Mwongozo wa Riwaya ya Chozi la Heri.*Nairobi: Global Link Publishers Ltd

Masango, M. (2002). *Leadership in the African Context*. Verbum Et Eclesia jrg, 23 (3), 707-718

Maslow, H. (1987). *Motivation and Personality*. Delhi: Pearson Education.

Matara, P.N. (2014). Uchanganuzi wa Lugha ya Amani na Maridhiano katika Muziki nchini Kenya (2008-2012). Tasnifu ya shahada ya uzamili. Chuo Kikuu Cha Moi. (Haijachapishwa)

Matei, A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi kamili wa Sarufi ya Kiswahili, Maswali na mazoezi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Moran Publishers (EA)

Matei, A. (2014). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishers

Matei, A. (2018).*Kurunzi ya Kiswahili*. Nairobi: Focus Publishers.

Mavisi, R. (2011). Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Riwaya za Zainabu Burhani.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Meyer, J. and Rown, B. (1977). *The Structural Dimensions Of Political Institutions of The State; Theorizing through Management and Institutional Theory*. American journal of Sociology, 83, 340-363.

Millett, K. (1969). *Sexual Politics*. Urbana and Chicago: University of Illinois.

Minerba, E. (2018). *Mayai-Waziri wa Maradhi, kitisho Kinachosimulia Siasa.*University of Bayreuth: Nordic Journal of African Studies –Vol.27 No.3 (2018).

Mlacha, K.(1985). *Wahusika wa Riwaya za Kiswahili Tanzania (1970-1982). MULKA17*, TUKI.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki. Dar es Salaam: Ecumnical Gathering* (EGYS).

Mosha, P.G. (2013). Usawiri wa Mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi: Uchanganuzi katika Rosa Mistika, Gamba la Nyoka na Nagona. Tasnifu ya shahada ya uzamili. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.(Haijachapishwa)

Mugenda na Mugenda (2008). *Social Science Research: Theory and Principles*. Nairobi: Arts Press.

Muindi, C. (1990). Usawiri wa wanawake Katika Vitabu vya S. A. Mohamed. Tasnifu ya shahada ya uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Munyasya, R. (2017). Mchango wa Vijana katika Kuleta Mabadiliko katika Riwaya ya Kufa Kuzikana na Kidagaa Kimemwozea. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mutugu, B. N. (2019). Taswira za Ulemavu kama Mtindo katika Riwaya teule za Said Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya uzamivu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mwenda, A. (2020). Taswira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya za Tumaini (2006) na Dunia Mashaka Makuu (2004). Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Nindi C. (1987). *The problem of Refugees in Africa*: A case study, Institute of Muslim Minority Affairs. Journal, 8:2, 387-396

Njenga, W. A. (2021). Uongozi Unavyojitokeza katika Fasihi ya Kisasa: Uchunguzi wa Riwaya Mpya ya Miaka ya 2000. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nock, S. (2009). *The Growing importance of Marriage in America***.** Columbia: Columbia University Press.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island, IL61201: Augustana College publishers

Nyong'o, A. (2001).*Government and Poverty in Africa. The African Academy of Sciences*. Nairobi: Development Bank Press.

Oettler, A. (2006). Guatemala in 1980's: *A Genocide Turned into Ethnocide.* Germany Institute of Global and Area Studies (GIGA) Working Papers No.19

Okwengu, N. M. (2010). *The Role of Government and Media Conflict in War: A case of The Kenyan 2007/2008 election violence*. New York: Lund University press.

Ondieki, F.M. (2015). Usawiri wa Watoto katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili zilizoandikwa na Mohamed Suleiman na Euphrase Kezilahabi.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa)

Ondoro, J. V. (2021). Maudhui ya Siasa na Athari zake katika Jamii:Mifano kutoka Diwani ya Kaza Macho. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Osango, D.S. (2015). Ukombozi wa Kisiasa na Kiuchumi katika Mkamadume. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Panagloti,M. Gooding, P. na Tarrier, N. (2012). Hopelessness, Defeat and Entrapment in Postraumatic Stress Disorder. Their Association with Suicidal Behaviour and Severity of Depession.In: *The Journal of Nervous and Mental Disease*, 200(8), pp: 676-683

Prendergast, C. (2001). *On the Rhetorics of Mental Disabiility, in Wilson, C. J. and Lewieck, C. (Eds.), Embodied Rhetorics: Disability in Language and Culture: 45-60*. Edwardsville: Southern Illinois University Press.

Scott, G. O. (2020). Migogoro ya Kisaikolojia katika Riwaya za Mkamadume na Unaitwa Nani. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Hajichapishwa)

Senkoro, F.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Sheikh, S. H. (2018). Uchanganuzi wa maudhui ya siasa katika hadithi mbili, Kikaza ya Robert Oduori na Uteuzi wa Moyoni ya Rayya Timamy. Shahada ya Uzamili. Mombasa. (Haijachapishwa)

Simiyu, M. (2020).*Citation: Analysis of selected Kiswahili Literary texts*- International Journal of Humanities and Social Sciences, vol.11 (1), pg 42-50.

Stewart F, Fitzgerald V, (2001). *War and underdevelopment: The economic and social Consequences of Conflict*. Oxford: Oxford University Press.

Syambo, K. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

TUKI, (2012). *Kamusi Sanifu ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Waki and Krieglar, (2009). *Krieglar and waki Report on Post Election Violence of 2007*. Nairobi. Printmark Ventures.

Waliaula, K. W. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Waliaula, K. W. (2003). *Kufa Kuzikana. Nairobi*: Longhorn Publishers.

Waliaula, K. W. (2003). *Ndoto ya Amerika*. Nairobi: Sasa Sema publishers.

Waliaula, K. W. (2005). *Innocence Long Lost*. Nairobi: Sasa Sema Publication.

Waliaula, K. W. (2006). *Ndoto ya Almasi*. Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Waliaula, K. W. (2007). *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University Press.

Waliaula, K. W. (2009). *Upande Mwingine*. Nairobi: Oxford University Publisher.

Waliaula, K.. W. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Spotlight Publishers (EA)

Waliaula, K. W. (2012). *Waja Leo*. Nairobi: Oxford University Press.

Waliaula, K. W. (2012). *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford university Press.

Waliaula, K. W. (2012). *Chapuchapu*. Nairobi: Moran Publishers.

Waliaula, K. W. (2013). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Moran Publishers

Waliaula, K. W. (2014). *Nasikia Sauti ya Mama*. Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Waliaula, K. W. (2014). *Narrating Prison Experience*. New York: Common Ground Publishing.

Wanjiku, T. (2018). Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule mbili za Said A.Mohamed: Utengano na Dunia

Wanjiru, A. N. (2021). Uongozi unavyojitokeza katika fasihi ya Kisasa; Uchunguzi wa Riwaya Mpya ya miaka ya 2000. Tasnifu ya shahada ya uzamili. Chuo kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Winerman, L. (2005). *Helping men to Help Themselves*. https:// www.apa.org (Accessed on 3rd March 2022)

Woloch, A. (2003). *Minor characters and The space of The Protagonist in The novel***.** Princeton: University Press New Jersey

# VIAMBATISHO

## Kiambatishi A: Barua ya NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 188527

Date of Issue: 02/June/2022

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. ERICKSON Okora MOGONDO of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nyamira on the topic: USAWIRI WA WAATHIRIWA WA GHASIA ZA KISIASA NA KIKABILA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI for the period ending : 02/June/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/18021**

188527

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**Kiambatishi B: Kibali cha kufanya utafiti**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

*OUR REF:* C50/CE/34433/16

Date: 8th July, 2021

The Director General,
National Commission for Science, Technology & Innovation,
P.O. Box 30623,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MOGONDO E. OKORA REG. NO. C50/CE/34433/16

I write to introduce **Mr. Okora** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A. Degree programme in the **Department of Kiswahili & African Languages in the School of Humanities & Social Sciences.**

Mr. Okora intends to conduct research for a M.A. Project Proposal entitled **"Usawiri wa Waathiriwa wa Ghasia za Kisiasa na Kikabila Katika Riwaya Teule za Kiswahili."**.

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHIBA KIMANI
DEAN, GRADUATE SCHOOL

HI/cao

**Kiambatishi C: Idhinisho la kufanya utafiti**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 8th July, 2021

TO: Mogondo Erickson Okora
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/CE/34433/2016

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 25th June, 2021 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Usawiri wa Waathiriwa wa Ghasia za Kisiasa na Kikabila Katika Riwaya Teule za Kiswahili".

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

HARRIET ISABOKE
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Daktari Beth N. Mutuga
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

HI/lnn